Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 18 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report of Tanzania Revenue Authority for the Year 2001/2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko Unaotokana na Ubinafsishaji kwa Mwaka ulioishia Tarehe 14 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of Privatization Trust for the Financial Year ended 14th June, 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation* kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2002 *(The Annual Report and Audited Financial Statements of the Consolidated Holding Corporation for the Year ended 31st December, 2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Ukusanyaji Madeni Sugu ya Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Loans and Advances Realization Trust for the Year ended 30th June, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 140

### Utaratibu wa Kusherehekea Sikukuu ya Uhuru

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa sherehe za kuadhimisha Sikukuu ya Uhuru wa nchi yoyote ni miongoni mwa matukio adimu sana ambayo kimsingi viongozi wa nchi husika huyatumia kukumbushana juu ya historia na kwamba lengo sio kukumbusha juu ya dhiki na machungu ya utawala wa kikoloni bali ni kwa namna gani wananchi waitumie siku hiyo kama kielelezo muhimu cha maendeleo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa pana haja ya kubadili au kurekebisha muundo wa kusherehekea siku hiyo ili iadhimishwe kwa matukio muhimu ya kukumbukwa kwa nchi nzima kama majengo yakafanyiwa usafi na kupakwa rangi, wananchi kuandamana na michezo mbalimbali kuliko ilivyo sasa ambapo sherehe hizo hufanyikia mahali pamoja tu?

(b) Kwa kuwa Dar es Salaam sio sehemu pekee Tanzania; je, Serikali ina mpango gani wa kufanya sherehe hizo muhimu kwenye Makao yote Tanzania kwa zamu kama ukumbusho?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa wabunifu kwa lengo la kufanya sherehe hizo zijenge fikra sahihi na historia kwa jamii ya Watanzania hasa watoto ambao kwa sasa hawajui vizuri maana ya sherehe za uhuru wa nchi yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mbunge wa Busega, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sherehe za Uhuru husherehekewa nchini kote katika ngazi tatu ambazo ni Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya. Kitaifa, sherehe hizi zinahudhuriwa na Viongozi wa Kitaifa na hata wageni kutoka nje ya nchi kwa mwaliko wa Mheshimiwa Rais na kuhitimishwa kwa Mheshimiwa Rais kukagua gwaride rasmi la vikosi vya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Kimkoa na Kiwilaya sherehe hizi zinahudhuriwa na viongozi wa Mikoa na Wilaya zinazohusika ambapo Wakuu wa Mikoa na Wilaya husika huhutubia mikutano ya hadhara baada ya maandamano na wanafunzi kutoka shule mbalimbali hualikwa kuhudhuria na kushiriki michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu uliopo ni mzuri kwani unahusisha wananchi katika Wilaya na Mikoa yote pamoja na shughuli zao kama michezo, usafi wa mazingira, maandamano na kadhalika. Wananchi kupitia viongozi wao, wanayo fursa ya kuandaa ratiba za sherehe za uhuru kwa namna wapendavyo wao wenyewe.

(b) Mheshimiwa Spika, jambo hili linazungumzika na hasa kutokana na uzoefu tulioupata mwaka 2003 wa maadhimisho ya sherehe hizo hapa Dodoma. Serikali itatafakari ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge ikiwa ni pamoja na kuainisha faida na gharama zake kabla ya kutoa uamuzi. Kwa sasa utaratibu uliopo utaendelea.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua haja ya kujenga fikra sahihi na historia ya Uhuru wa Tanzania kwa Watanzania hasa watoto kwa kuhusisha katika mitaala ya shule mafunzo ya uraia mashuleni na vyuoni kwa lengo la kuwafanya vijana wetu kujua maana ya uhuru wa nchi yao.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa sherehe hizi mwaka2003 zilifanyika hapa Dodoma na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kulikuwa na hamasa ya kutosha. Je, Serikali pamoja na kwamba imekubali kufikiria suala hili, inaonaje sasa sherehe za mwaka huu wa 2004 zikafanyike Mwanza, za mwaka 2005 Kigoma na za mwaka 2006 Shinyanga? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, nimeshasema kwenye jibu la Mheshimiwa Dr. Chegeni, jambo hili ni jema, linazungumzika na hayo yote yanawezekana. Tupeni muda tutafakari ili tuone uwezekano wa kutekeleza hayo anayotaka Mheshimiwa Musalika. *(Makofi)*

Na. 141

**Barabara ya Ubiri-Kwagunda**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Kijiji cha Ubiri, Kata ya Kwagunda wanapotaka kwenda Makao Makuu ya Wilaya - Korogwe Mjini (kwa gari) kwa shida zao mbalimbali kama kusafirisha wagonjwa ni lazima wapitie Muheza umbali wa kilomita 130 kwa mwendo wa gari ambao ni zaidi ya saa tatu na nusu kuweza kufikia Korogwe Mjini; na kwa kuwa kutokana na adha hiyo, wananchi wameamua kuchimba barabara kutoka Ubiri, Kwagunda yenye urefu wa kilomita nane baada ya kupata ushauri, Idara ya Ujenzi, Wilaya na Mkoa; na kwa kuwa kazi ya kuchimba barabara hiyo imemalizika lakini haiwezi kupitika kwa urahisi kwa sababu ya makorongo, vidaraja vidogo vidogo ambavyo vitahitaji kuwekwa makaravati; na kwa kuwa makadirio ya kumalizia sehemu hizo yamefanyika na kufikia kiasi cha shilingi 39 milioni makadirio ambayo yamepelekwa Serikalini kuomba msaada wa Serikali kwa sababu nguvu za wananchi zimekomea hapo:-

Je, Serikali itasaidiaje katika kufanikisha nguvu za wananchi hao ili barabara waliyoichimba iweze kukamilika na kupitika kwa urahisi na kuwaondolea kero na adha wanayopata kuzungukia Muheza wanapofuata huduma kwenye Makao Makuu ya Wilaya Korogwe Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza wananchi wa Kijiji cha Ubiri, kwa juhudi walizokwisha kuchukua katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Moyo huu wa kujitolea tunaomba uendelezwe na pia kuigwa na wananchi wa maeneo mengine. Serikali inatambua matatizo ya usafiri yanayowakabili wananchi wa Kijiji hicho na kwa kutambua hilo na pia juhudi za wananchi ambazo wamekwishazionyesha, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, makisio ya kuifanyia matengenezo barabara ya Ubiri hadi Kwagunda yaliingizwa kwenye mpango wa Wilaya kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara zitolewazo na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mpango huu ulikwishaidhinishwa na awamu ya kwanza kiasi cha shilingi 16.7 milioni kimetengwa kwa matangenezo maalum yenye urefu wa kilomita 2.5. Naomba tuendelee kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba, Halmashauri yake inaendelea kutenga fedha kila mwaka chini ya mpango wa matengenezo ya barabara.

**MHE. JEOL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa kutenga shilingi milioni kumi na sita kwa barabara hiyo na nina swali moja tu.

Kwa kuwa barabara za aina hii *(Feeder Roads)* kama vile ya Ubiri-Kwagunda ni nyingi katika Vijiji vyetu ambazo hazipati mafungu mara kwa mara kutoka katika Wizara na ndiyo barabara muhimu katika Vijiji vyetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia barabara hizi za Vijijini ambazo ndizo zinasaidia wananchi zaidi katika kupeleka mazao yao kwenye barabara kuu kwa kutoa fungu maalum, kwa sababu hakuna fedha maalum zinazotolewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa chanzo kikubwa cha fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu Vijijini ni zile zinazotokana na Mfuko wa Barabara ambao TAMISEMI wanapewa asilimia thelathini kati ya asilimia mia moja zinazopatikana kila mwaka. Fedha hizi zinagawiwa kutokana na mipango inayoandaliwa na Halmashauri zenyewe. Sisi kazi yetu ni kusimamia ugawaji na hatimaye matumizi.

Kwa hiyo, kwa maana hiyo Serikali haina chanzo kingine ambacho tunaweza tukakitegemea kwa sasa kuimarisha barabara zingine. Lakini naomba nikumbushe tu kwamba, juzi katika semina iliyofanyika hapa, yapo mawazo mazuri tu yaliyojitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, ambayo tunajaribu kuyazingatia tuone kama yanaweza kutusaidia katika eneo hili. *(Makofi)*

Na. 142

**Wanunuzi wa Muhogo Toka India**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kwamba wanunuzi wa Muhogo toka India waliwasili hapa Tanzania kuona mazingira ya uzalishaji na uwezekano wa kununua zao hilo:-

(a) Je, hali ya ununuzi wa Muhogo na wafanyabiashara hao ikoje?

(b) Kama sio nzuri Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la kudumu la zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ujumbe wa Wafanyabiashara kutoka India ulikuja Aprili, 2003 ili kuangalia uwezekano wa kufanya biashara ya zao la muhogo kwa kupitia Kampuni ya *Afro Centre Tanzania Limited.* Wafanyabiashara hao walitaka kununua tani 100,000 za muhogo kwa bei ya Dola za Marekani 45 - 50 kwa tani ambayo ni sawa na takriban shilingi 45 - 50 kwa kilo. Kwa vile bei iiyopendekezwa na wafanyabishaara hao ilikuwa ni ya chini ukilinganisha na bei iliyopo ambayo ni zaidi ya shilingi 100 kwa kilo, ununuzi wa muhogo kupitia wafanyabiashara hao haukuweza kufanyika.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kueleza wakati najibu Swali Na. 4 la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, mwaka 2001 na Swali Na. 64 la Mheshimiwa Lydia Boma mwaka 2003, soko la zao la muhogo linakabiliwa na vikwazo vingi vikiwemo vifuatavyo:-

(i) Kushindwa kuhimili ushindani utokanao na nafaka zenye matumizi sawa na muhogo kama vile mahindi, mpunga na mtama;

(ii) Ukosefu wa teknolojia rahisi Vijijini za kukausha na kusindika muhogo ili iwe rahisi kuusafirisha kwenda kwenye masoko ya nje na ya ndani; na

(iii) Uduni wa makopa yanayozalishwa hususan katika Mikoa ya Kusini ambako makopa huanikwa ardhini na hivyo kusababisha unga utokanao na makopa hayo kuwa na mchanga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizi pamoja na ongezeko la uzalishaji wa muhogo katika nchi za Thailand na Malaysia katika miaka ya hivi karibuni ambapo nchi hizo zinayo ziada ya muhogo unaozidi takriban tani 1,000,000, soko dogo la muhogo wa Tanzania ambalo lilikuwa linapatikana katika nchi za Ulaya limekufa kabisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa matatizo hayo yanayoathiri upatikanaji wa soko la kudumu la zao la muhogo, Serikali kupitia Wizara yangu inayo mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, wakulima wa zao la muhogo wanapata soko la kuaminika kwa zao lao. Mikakati hiyo inajumuisha mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa taarifa za bei ya zao la muhogo katika masoko makuu nchini ili kuwawezesha wafanyabiashara kufahamu ni wapi mazao yanapatikana na wapi masoko yake yalipo;

(ii) Kuhamasisha taasisi zilizo na teknolojia ya kisasa iliyofanyiwa utafiti kama vile *Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), National Resources Institute (NRI), Institute of Productivity and Innovation (IPI)* na *International Crop Research in Semi-*

*Arid Tropic (ICRISAT),* ili ziweze kueneza teknolojia ya kukausha makopa na kusindika muhogo katika Mikoa ya Kusini ukiwemo Mkoa wa Mtwara kwa lengo la kuongeza thamani ya muhogo na hivyo kuweza kuwapatia wakulima soko la uhakika zaidi;

(iii) Kutoa elimu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji juu ya njia bora za kuzalisha na kuandaa mihogo yenye ubora unaohitajika hususan katika masoko ya nje ya nchi kwa lengo la kupanua wigo wa soko la mihogo;

(iv) Kukuza soko la ndani kwa kuhamasisha wasindikaji wa vyakula vya mifugo na watengenezaji wa bidhaa nyingine kama *biscuit* kwa kutumia zao la muhogo kama inavyofanyika katika nchi za Botswana na Afrika ya Kusini; na

(v) Tanzania ikiwa mwanachama wa *SADC,* imo katika mpango kamambe wa kuendeleza zao la muhogo kuwa zao linalozalishwa kibiashara chini ya mpango unaosimamiwa na *NEPAD.* Chini ya mpango huo wakulima wadogo wadogo wa muhogo watahamasishwa kuunda umoja wao kwa ajili ya kuwezeshwa ili wawe na mbinu za kuzalisha muhogo kwa wingi na wenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya soko katika nchi za *SADC* na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mbinu hizi, Serikali itaendelea kuhimiza wananchi waongeze uzalishaji na matumizi ya muhogo kwa chakula chao wakati wote badala ya kutumia muhogo kama zao la kinga ya njaa wakati wa upungufu wa chakula.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa ametaja mikakati mbalimbali ya kuboresha zao la muhogo ili lipate soko, je, mikakati hiyo itaanza lini tusije tukawa tumesahau kulima na muhogo wenyewe kama mikakati itachukua muda mrefu kutufikia?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mikakati niliyoieleza hapa ni mikakati ambayo imeshaandaliwa na kwa maana hiyo imekwishaanza kwa sababu kufanya tu maandalizi ni tayari imekwishaanza kwa hiyo ipo katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona ili niulize swali dogo la nyongeza. Zao la muhogo ni zao la kinga ya njaa na linatumika sehemu nyingi katika nchi yetu, lakini hivi karibuni tuliambiwa kwamba Mtwara kule watu walikuwa wanapooza viungo kutokana na sumu ambayo ilijulikana kama *Xyonide*, sina hakika kama kupooza huko kumenusuru kizazi lakini ninachotaka kusema ni kwamba, je, inawezekana Serikali katika utafiti huo basi ikaondoa mbegu ile ambayo ni mbaya, pengine ikapata sehemu nyingine mbadala kutoka sehemu nyingine kama Morogoro? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kwamba, tunajaribu kuhamasisha watu waelewe kwamba zao la muhogo lisisubiriwe tu kama ni zao la kinga ya njaa badala yake liwe ni zao la chakula kama yalivyo mazao mengine. Kwa mfano, hapa Dodoma tayari tumeshaweka azimio kwamba muhogo ni zao la chakula kama mazao mengine. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba liwe ni la kinga ya njaa nadhani itakuwa siyo dhana sahihi.

Lakini Mheshimiwa Spika, kuhusu sumu ambayo inapatikana katika baadhi ya mihogo, ndiyo hiyo baadhi ya mikakati niliyosema kwamba, hizi taasisi za utafiti ambazo tunashirikiana nazo na Serikali zitahakikisha kwamba, mbegu bora inapatikana ili mihogo inayolimwa isiwe na madhara kwa wananchi. *(Makofi)*

Na. 143

**Soko kwa Ajili ya Zao la Mpunga**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga ni moja ya Mikoa inayozalisha zao la mpunga kwa wingi hasa katika Tarafa za Isagehe na Msalala na kwa kuwa zao hilo sasa limekuwa ndilo zao pekee la biashara katika maeneo niliyoyataja:-

(a) Je, Serikali inafahamu shida kubwa waliyonayo wakulima wa mpunga ya kukosekana kwa soko la uhakika la zao hilo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haina mkakati kamambe wa kulitafutia zao hilo soko la uhakika badala ya kuwaachia wananchi peke yao kujihangaikia kutafuta soko?

(c) Endapo kuna ufanisi wowote katika bodi nyingine za mazao, je, ni lini Serikali itaanzisha bodi ya kushughulikia uzalishaji, ubora na upatikanaji wa soko la mpunga kama ilivyo kwa mazao ya pamba, korosho, kahawa, pareto, chai, mkonge na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Enock Kipole, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tofauti na mazao mengine ya biashara ambayo soko lake hutegemea zaidi wanunuzi wengine, zao la mpunga huweza kutumiwa na wazalishaji moja kwa moja kama chakula na kiasi kinachobaki ndiyo hutafutiwa soko kwa ajili ya kuuza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizo nazo kwa mfano, mwaka 2001/2002, Mkoa wa Shinyanga ulizalisha tani 188,709 za mpunga. Kati ya hizo tani 141,531 ambayo ni sawa na asilimia sabini na tano, zilitumiwa na wazalishaji moja kwa moja kama chakula baada ya kuvuna na tani 47,178 tu ndizo zilibaki kwa ajili ya kuuza sokoni. Wanunuzi kutoka soko la ndani wamekadiriwa kuwa walinunua tani 31,845 kati ya tani 47,178 zilizosalia kwa ajili ya soko. Vile vile soko la nje ya nchi hususan Zaire, Burundi, Rwanda na Kenya walinunua tani 4,718 za mpunga na kufanya Mkoa wa Shinyanga kubakiwa na tani 10,615 za mpunga ambao haujauzwa, sawa na asilimia tano ya uzalishaji katika mwaka 2001/2002. Hali hii inafanana sana na ilivyo katika miaka mingine. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa biashara isiyo rasmi *(Informal Cross-Border Trade),* kuna uwezekano mkubwa kuwa mpunga mwingi zaidi unauzwa nje ya nchi na kwa hiyo kwa juhudi kidogo za kuimarisha zaidi soko la ndani na nje, tatizo la ukosefu wa soko la mpunga Mkoani Shinyanga litatoweka.

(b) Mheshimiwa Spika, zao la mpunga kama mazao mengine ya chakula, yamekuwa yakinunuliwa na watu binafsi kufuatana na mwenendo wa bei uliopo pamoja na hali halisi ya soko. Serikali kwa upande wake imekuwa ikitoa taarifa za bei katika masoko mbalimbali kila wiki kwa mazao ya chakula likiwemo mchele kwa lengo la kukuza uwezo wa sekta binafsi katika kununua na kuuza mazao ya wakulima katika masoko.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, ilikwishafanya uchunguzi juu ya uwezekano wa kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa lengo la kuratibu shughuli za mazao mchanganyiko. Hata hivyo, utekelezaji kutokana na uchunguzi huo umesitishwa kwa muda hadi hapo Sera ya Masoko inayoandaliwa na Serikali itakapokamilika. Kutokana na sera hiyo, Serikali itaweza kuamua ni mazao gani yanafaa kuundiwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na ni yapi yatahitaji kuwa na Bodi yake peke yake.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, napenda niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja, kwa kuwa juzi juzi hapa tumepitisha sheria ya *Anti-dumping* inayojaribu kulinda viwanda vyetu hapa nchini kutokana na wazalishaji ambao katika nchi zao hupata *subsidy* na kwa kuwa tunafahamu vile vile katika nchi zingine wakulima hupewa *subsidy* katika uzalishaji na hivyo kuzalisha kwa gharama ya chini na mazao hayo huletwa katika nchi yetu kwa mfumo

ule ule kama wa *Anti-dumping* ambao tulikuwa tunauzungumzia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta sheria ya kuwalinda wakulima hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Bodi za Mazao kama nilizozitaja pareto, pamba, kahawa na kadhalika ni mashirika ya umma ambayo hupata wakati mwingine ruzuku za Serikali kuweza kuwasaidia wakulima wanaohusika; na kwa kuwa wakulima wa mpunga wengine hawanufaiki na *subsidy* za Serikali zinazokwenda kwenye mashirika hayo na vile vile hata huduma za ugani zinazokwenda kwa wakulima wa mpunga hazipati sana sana huduma za ugani kama zinazopelekwa kwenye pamba na tumbaku; je, wakulima wa mpunga wataishukuru Serikali kwa jambo lipi ililowafanyia?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la kuomba Serikali ifikirie kuleta sheria ya kuwalinda wakulima. Niseme tu kwamba, jitihada zote za Serikali ambazo zinafanywa sasa hivi zina lengo la kumlinda mkulima. Jitihada ambazo zinafanyika kwa mfano sasa hivi Sheria za Bodi za Mazao ambazo zilipitishwa mwaka 2001, Sheria ya Ushirika ambayo imepitishwa hivi karibuni, zote hizo zina lengo la kumlinda mkulima ili aweze kupambana na tatizo la anayoyapata katika soko huria. Kwa hiyo, suala la kuleta sheria mpya ya kuwalinda wakulima nataka niseme kwamba, Serikali inaendelea kufanya jitihada hizo kwa kuleta sheria hizo ambazo nimekwishazitaja pamoja na sera zingine ambazo zipo katika utekelezaji hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu Bodi za Mazao kupata ruzuku ya Serikali na hivyo kutoa huduma kwa mazao yale ambayo yanazihudumia niseme tu kwamba hata mazao haya mengine ambayo hayana bodi maalum ikiwemo mpunga, mahindi na kadhalika licha ya kwamba bado tunaandaa huu utaratibu wa kuundia chombo maalum hivi sasa wataalam wa ugani wanatoa huduma kwa mazao yote yakiwemo haya ambayo hayana bodi maalum. Kwa hiyo, wakulima wanapaswa waishukuru sana Serikali kwa huduma ambazo zinatolewa na Serikali za kuwasaidia wakulima kuzalisha zaidi.

Na. 144

**Soko la Hisa - Stock Exchange**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa Soko la Hisa *(Stock Exchange)* pamoja na ofisi zake liko Jijini Dar es Salaam lakini biashara ya kuuza na kununua hisa inahitajika nchini kote na kwa kuwa soko hilo halina matawi kwenye Mikoa au kwenye maeneo ya Kanda nchini. Je, soko hilo linatoa nafasi zipi kwa wananchi wa maeneo niliyoyataja katika kushiriki kikamilifu wakati wa kuuza hisa unapofanyikia Dar es Salaam mara zote?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ununuzi na uuzaji wa hisa nchini hufanyika katika hatua mbili ambazo ni kama ifuatavyo:-

(a) Soko la Awali yaani *Initial Public Offering (IPO),* yaani kuuzwa mara tu inapoamuliwa kuwa kampuni fulani iwe na wenye hisa kutokana na umma *(Public Company).* Hapa wanahisa wanatakiwa wasipungue saba na wasizidi hamsini kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura 212 ya Sheria za Tanzania. Katika soko hilo la awali, uuzaji na ununuzi wa hisa hufanyika kupitia kwa madalali wa soko la hisa *(brokers)*, kupitia Shirika la Posta nchini na mabenki yenye mtandao mkubwa kama *NBC Limited, CRDB Limited, NMB Limited* na *Standard Chartered Bank Limited.*

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya hisa kuuzwa kwenye soko la awali, hisa hizo huorodheshwa kwenye soko la pili ambalo ni Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuanza kuuzwa na kununuliwa kupitia madalali wa soko hilo pekee. Kwa sasa kuna makampuni sita ya udalali yaliyopewa

leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA),* ambayo huuza na kununua hisa kwa niaba ya wateja. Makampuni hayo ni *Tanzania Securities Limited, Solomon Securities Limited, Raslimali Limited, Orbit Securities Limited, Vertex International Securities Limited* na *Core Security Limited*. Makao Makuu ya Makampuni haya yote yako Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi walio nje ya Dar es Salaam wanaotaka kununua au kuuza hisa zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, hutumia mojawapo ya njia mbili zifuatazo:-

Kwanza, muuzaji au mnunuzi anaweza kununua au kuuza hisa kwa kutumia mawakala wa madalali wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wafuatao:-

(i) Shirika la Posta Tanzania. Kwa kutumia matawi yote yaliyoko nchini (Tanzania Bara na Visiwani). Shirika hili ni Wakala wa *Tanzania Securities Limited;* na

(ii) Mawakala wa madalali walioko Mikoani. Baadhi ya madalali tayari wana mawakala kwenye baadhi ya Mikoa. Kwa mfano, *J.B. Capital Limited* wa Mwanza Mjini ni wakala wa kampuni ya udalali ya *Raslimali Limited.*

Pili, muuzaji au mnunuzi anaweza kuwasiliana moja kwa moja na dalali aliyeko Dar es Salaam kwa njia ya simu au barua pepe na kutoa maagizo yake *(order)* ya kununua au kuuza hisa. Kisha malipo hufanyika kupitia benki. Yaani mteja anayenunua hisa huweka kiasi kinachotakiwa kwenye akaunti maalum ya wateja benki na yule anayeuza hisa hutumiwa fedha zake kupitia akaunti yake katika benki husika. Baada ya dalali kununua hisa humtumia mteja cheti cha hisa *(Depository Receipt)* kwa njia ya rejista ya posta.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imeidhinisha utaratibu wa kuyawezesha makampuni ya udalali kuwa na mawakala *(agents)* Mikoani. Siyo makampuni yote ya udalali wa hisa yana mawakala Mikoani na siyo kila sehemu hapa nchini ni mawakala wa Soko la Hisa. Kabla ya kuwa na wakala, dalali anahitaji apate kampuni au mtu mwaminifu na mwenye kuelewa taratibu na miiko ya uuzaji na ununuzi wa hisa. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA),* inaendelea kuwahimiza madalali wote kuwa na mawakala wanaofaa kote nchini ili kuwafikia wananchi walio nje ya Dar es Salaam. Ni vizuri ieleweke pia kuwa dalali huteua wakala mahali anapoona kuna wateja na kwamba atapata biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi walio nje ya Dar es Salaam kuweza kushiriki katika kununua na kuuza hisa kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam, mipango iko mbioni kuanzisha ununuzi na uuzaji wa hisa zilizoorodheshwa kwa kutumia mtandao wa kompyuta *(Electronic Trading),* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *Financial Institutions Development Programme II (FIDA II).*

Upembuzi yakinifu unafanywa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)* kupitia Kampuni ya ushauri ya *DCDM* ya Dar es Salaam ili kutoa mpendekezo ya kuanzishwa mfumo na taratibu za kuwezesha ununuzi na uuzaji wa hisa kwa njia ya mtandao wa kompyuta. Mfumo huu unatarajiwa kuanza kufanya kazi ifikapo Desemba, 2004, jambo ambalo litasaidia kusogeza huduma hii karibu zaidi na wananchi na kuweza kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo ambalo Mheshimiwa Stephen Kazi, amelizungumzia.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na ya wazi kutoka kwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Hayo aliyoyasema na kuyaeleza naona hayawafikii na hayajafahamika vizuri kwa watu hasa wafugaji wakubwa wakubwa ambao wangeweza kuuza mifugo yao na kununua hisa, hawa wanapanga kuwafikia namna gani?

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa tu kufahamu kwamba, mpaka sasa hawa watu wenye migodi yote nchini ya dhahabu, almasi, wanauza hisa wanapohitaji kuboresha mitaji yao na wanafanya hivyo kwenye maeneo yao, nchini kwao, ambako wamejiandikisha wanafanya hivyo huko Bangkok, London, sehemu nyingine huko *South Africa,* wanauza hiyo.

Kwa vile sisi Watanzania tuna nia ya kununua hisa na kuingia na kuwa wamiliki katika migodi hii na kushiriki kiuchumi ndani ya migodi hii, sasa ningependa kufahamu Serikali ina mipango gani kupitia Wizara ya Fedha pia Wizara ya Viwanda na Biashara, ili hao wenye migodi waweze kuuza hisa zao kupitia kwenye *Dar es Salaam Stock of Exchange*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, kuna njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika ili watu wanaohitaji kushiriki katika ununuzi na uuzaji wa hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam wanaweza kuzitumia. Wanaweza kutumia mawakala ambao nimesema wengine wako Mikoani. Lakini pia utaratibu ambao nimesema unaandaliwa ambao utaanza Desemba, 2004 ambao ni wa kutumia kompyuta, utasaidia sana kuwafikia wananchi wengi. Lakini itakuwa vigumu kuwafikia wafugaji ambao hawana elimu ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, biashara hii ya soko la hisa ni biashara mpya katika nchi yetu na taratibu wananchi watazielewa vizuri na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amewahi kusema hapa kwamba, biashara ya hisa siyo kama benki unaweka fedha zako unasahau mpaka mwisho wa mwaka ndiyo unakwenda kuangalia. Inatakiwa unaangalia bei imepanda, unauza, ikishuka unanunua na kadhalika. Kwa hiyo, taratibu wananchi wote wa Tanzania wataelewa soko la hisa la kununua na kuuza hisa na watashiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pili, Watanzania kushiriki katika biashara ama katika makampuni ya migodi. Kuna namna mbili ya hisa. Kwanza, kuna *Private Placement* kwenye kuuza hisa, makampuni binafsi yanauza hisa zao, lakini siyo kwa kupitia katika soko la mitaji na katika *Stock Exchange.* Kwa hiyo, hao wenye migodi ni makampuni binafsi ambao wao wenyewe wanajua namna ya kutafuta mitaji yao na wakipenda kama walivyofanya *BIDCO,* jana *BIDCO* wameingia kwenye soko la mtaji na hisa na watu wamekwenda na wananunua hisa katika Kampuni hiyo. Kwa hiyo, mgodi wenyewe utakapofikia mahali sasa unataka kuuza *share* kwa sababu mbalimbali aidha, za kupata mtaji na kadhalika, watafanya hivyo na wataleta kwenye soko la hisa. Kama Mheshimiwa Stephen Kazi na Waheshimiwa Wabunge wengine wanataka kununua hisa, basi waonane wenye migodi hiyo moja kwa moja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kufafanua zaidi kwamba wafugaji wanaweza wakanunua hisa za kampuni yoyote kama Mawakala hao waliotajwa kwenye jibu letu wangeenda minadani na kuwabembeleza wafugaji wakiwa mnadani ili fedha zao zinunue hisa. Kwa hiyo, ningependa kuchukua fursa hii kuwaomba Mawakala wawe na mitandao ya kuwafikia wafugaji na wakulima vijijini kule waliko. *(Makofi)*

La pili, kampuni za madini zinaweza zikauza hisa kwenye soko la hisa kwa njia mbili wakati wanapotafuta mitaji mikubwa ya kuanzishia migodi yao kule mwanzo. Hiyo imekwishafanyika kwa migodi yetu iliyoko sasa hivi maana walishapata mtaji na shughuli zimeanza. Mara ya pili ni wanapotaka sasa kupanua na kupata mitaji zaidi ya kuendeleza migodi iliyopo. Hivyo, kwa mujibu wa sheria inafanywa pale ambapo migodi yenyewe inatoa faida. Huwezi kwenda kwenye soko la hisa, kuuza hisa kwa mgodi ambao haujaonyesha faida nzuri kwa sababu hutapata bei nzuri. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa kwamba, migodi yetu itakapofikia kiwango cha kutengeneza faida nzuri na juzi tulisikia hapa yule *Manager* wa Kahama alisema bado hajapata faida, ninahakika siku wakipata faida nzuri wataenda kwenye soko la hisa na wananchi wanaweza wakanunua hizo hisa kwa mujibu wa soko hilo la wakati huo. *(Makofi)*

Na. 145

**Mikopo ya Mabenki**

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na tuhuma za rushwa katika utoaji wa mikopo katika Mabenki na Taasisi mbalimbali za fedha hapa nchini:-

(a) Je, katika Benki ya Posta ni mikopo ipi ya muda mfupi na mrefu imewahi kutolewa na imetolewa kwa kuzingatia vigezo gani?

(b) Je, ni kweli kwamba katika Benki ya *Savings and Finance Limited* mikopo imetolewa kwa Watanzania wenye asili ya Kiasia na watu wenye nyadhifa kubwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya Benki hiyo na kama ni kweli, ni mikopo ipi hiyo na ni ya kiasi gani cha fedha?

(c) Je, ni kwa nini fedha zilizopo *FEDA/SATF* zimekwama kuchukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara , lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Wizara yangu haina taarifa kwamba kumekuwepo na rushwa katika utoaji wa mikopo katika mabenki na taasisi mbalimbali za fedha hapa nchini. Lakini kwa kuwa tatizo la rushwa lina athari kwa uchumi na kuleta madhara kwa jamii, Serikali inamwomba Mbunge na Mtanzania mwingine yeyote kama ana taarifa zozote zinazohusu suala la rushwa katika mabenki na taasisi za fedha, aziwasilishe Serikalini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Desemba, 2003, Benki ya Posta imekwishatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.3 kwa sekta na watu binafsi. Vigezo vinavyotumika ni vilevile vinavyotumiwa na Mabenki yote ya kisasa ikiwa ni pamoja na uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo, riba, historia ya mkopaji, mtaji wa mkopaji na dhamana. Benki ya Posta pia inazingatia taratibu za ukopeshaji kama zilivyoainishwa kwenye sera na kanuni za utoaji mikopo, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa mikopo, kama zilivyoelezwa na Benki Kuu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina taarifa kwamba katika Taasisi ya Fedha, *Savings and Finance Limited*, mikopo imekuwa ikitolewa kwa Watanzania wenye asili ya Kiasia na watu wenye nyadhifa kubwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya taasisi hiyo. Sera na taratibu za utoaji mikopo hupitiwa na Benki Kuu kuhakikisha kuwa hakuna vipengele vya aina yoyote vya ubaguzi au upendeleo. Hivyo, Taasisi hii inazingatia taratibu zote pamoja na sheria na kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa mikopo kama zilivyotolewa na Benki Kuu. Hata hivyo, kama nilivyosema, kama Mheshimiwa Mbunge ana uthibitisho wa kuwepo kwa ubaguzi na upendeleo katika utoaji mikopo katika Taasisi hiyo na nyingine yoyote, namwomba aiwasilishe katika Serikali ili hatua zipasazo ziweze kuchukuliwa?

(c) Mheshimiwa Spika, *Social Action Trust Fund (SAFT)* ni Mfuko ulionzishwa mwaka 1998 kama mradi ambapo Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Misaada *(USAID)* ilitoa msaada wa shilingi bilioni 7.6 ambazo zilitumika kwa mtaji wa Mfuko huo. Mfuko huo uligawanywa katika mifuko midogo miwili.

Mheshimiwa Spika, Mfuko mdogo wa kwanza ulipewa shilingi bilioni 6.3 ikiwa ni kwa ajili ya kusaidia kukuza uchumi wa Taifa kwa kuwekeza katika sekta binafsi kwa njia ya kutoa mikopo kwa

wafanyabiashara. Kiwango cha mikopo ni kati ya shilingi milioni 10 na milioni 800. Fedha inayopatikana kama faida kutokana na kuwekeza huko inatumika katika maeneo mawili yafuatayo:-

(i) Kusaidia watoto yatima waliopoteza wazazi wao kutokana na janga la UKIMWI; na

(ii) Kununulia hisa katika makampuni ambayo yanayouza hisa na yana uwezo wa kulipa gawio zuri.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia 31 Desemba, 2003 mikopo 26 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.9 ilikwishatolewa na Mfuko ulinunua hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.9. Aidha, Mfuko umepata faida ya shilingi bilioni 4.4 ambazo kati yake shilingi bilioni 1.9 ziliidhinishwa na Bodi ya Wadhamini zitumike kuwasaidia watoto yatima. Mfuko huu unaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko mdogo wa pili ulitengewa shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa miradi midogo midogo kwa masharti nafuu ikiwa ni pamoja na kuweka rehani mali inayonunuliwa na fedha za mkopo huo. *SATF* iliingia Mkataba na Kampuni inayoitwa *Finance and Enterprise Development Associates (FEDA),* ambao wamepewa kazi ya kuendesha Mfuko huo mdogo ili kuweza kuwafikia wananchi wengi. Kiwango cha mikopo ni kati ya shilingi milioni 2.4 hadi milioni 80. Hadi kufikia 31 Januari, 2001 fedha zote shilingi bilioni 1.3 zilikwishatolewa katika Mikoa ifuatavyo: Arusha, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Mwanza, Pwani , Ruvuma , Shinyanga , Tanga na Dar es Salaam 48.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kulegalega kwa urejeshaji wa mikopo, Mfuko huu ulisimamishwa na *FEDA* wakaagizwa kuwachukulia hatua waliokiuka masharti ya ukopaji. Aidha, sasa mikopo itatolewa kwa masharti mapya yenye lengo la kuhakikisha kwamba, Mfuko unakuwa endelevu. Wananchi watatangaziwa pindi Mfuko utakapoanza kutoa mikopo.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia nakubali ushauri wake kwamba, kama kutakuwa na hoja yoyote kuhusiana na hii Benki ya *Savings and Finance Limited* nimletee ikiwa ni pamoja kuhamisha fedha kwenda nje kinyemela, nitazifanyia utafiti na nitampa jibu.

**SPIKA:** Oho! *(Kicheko)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali lifuatalo. Kwa kuwa akinamama na vijana wamekuwa wanashindwa kukopa katika mabenki au kushindwa kurejesha fedha wanazokopa kutokana na riba kubwa ambayo ni asilimia 2 kwa mwezi, ikiwa ina maana kwamba ni asilimia 24 kwa mwaka. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kukaa na haya mabenki ili wateremshe riba iwe ndogo ili kuwawezesha vijana na akinamama kupata mikopo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali, haipangi riba na riba inapangwa na soko. Serikali inachofanya ni kuweka mazingira ambayo yatawezesha riba kushuka. Tatizo mabenki yanasema gharama za kuendesha mikopo ni kubwa na fedha nyingi kama ninavyofahamu bado ziko kwenye mabenki hazikopeshwi. Kwa hiyo, Serikali imechukua hatua za makusudi ili kuziondoa zile fedha kwenye mabenki ili ziweze kuzunguka. Mojawapo ni kwa kutumia hizi *Credit Guarantee Schemes,* ambapo Bunge lilipitisha mwaka 2003 shilingi bilioni 6.5 na mwaka 2004 shilingi bilioni 13 ili wafanyabiashara waweze kukopa. Lakini riba hizi zinatofautiana kati ya mkopaji na mkopaji, kutoka mkopaji mmoja kwenda mkopaji mwingine. Kuna wengi wanapewa riba ndogo kutegemea na jinsi gani wanarudisha kama nilivyosema kwamba, inategemea mkopaji uwezo wake wa kurejesha mkopo, historia yake na dhamana aliyonayo. Kwa hiyo, kutegemeana na vitu hivi, riba zinashuka.

Mheshimiwa Spika na *trend* tuliyonayo sasa, riba zinateremka. Miaka mitano iliyopita riba zilikuwa juu zaidi kuliko ilivyo hivi sasa na tunategemea kwamba zitaendelea kushuka.

Na. 146

***Tuition***

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna tuhuma kwamba walimu wa shule za msingi na sekondari hasa za mijini nchini hawafundishi kwa kiwango kinachotakiwa katika masomo mbalimbali kwa lengo la kuwavutia wanafunzi washiriki katika madarasa yao ya *Tuition*:-

(a) Je, ni nini sababu za kushamiri kwa madarasa hayo ya *Tuition* kwa wanafunzi wa shule hizo?

(b) Je, kuna athari gani kwa mfumo wa utoaji wa elimu kwa utaratibu huo?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kurekebisha na kudhibiti madarasa hayo ya *Tuition* kote nchini?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kushamiri kwa madarasa ya *tuition* ni ufundishaji na ujifunzaji hafifu madarasani uliokuwa katika shule zetu kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Mlundikano wa wanafunzi madarasani kutokana na uchache wa madarasa, kwa mfano, nilipotembelea Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2001, nilikuta wastani wa kimkoa ulikuwa wanafunzi 140 kwa darasa badala ya unaotakiwa wa 40 kwa darasa;

(ii) Uhaba wa walimu kutokana na ufinyu wa bajeti mpaka ilifikia tulikuwa hatuajiri walimu. Walimu 15,000 walikuwa wanasubiri kuajiriwa; na

(iii) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kwa hiyo, kwa kuwa watoto hawakushiba ufundishwaji wa darasani wazazi wao waliwatafutia mafundisho ya ziada kwa njia ya *tuition,* ambayo wenye uwezo wa kifedha walikuwa tayari kuilipia. Lengo mojawapo la MMEM ni kurekebisha kasoro hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, athari kubwa ya mfumo huo ni kuwa ulikuwa wa ubaguzi kati ya wenye uwezo wa kulipia *tuition* hizo na wale wasio na uwezo na hivyo kuwa na mwelekeo wa kujenga matabaka katika jamii. Aidha, baadhi ya walimu walianza kutojali sana kufundisha vizuri madarasani ili kupanua soko la *tuition* kama njia ya kujiongezea mapato. Katika baadhi ya shule *tuition* ilianza kuendeshwa kwa mfumo wa pili wa shule, kwa malipo na mahudhurio ya lazima na walioshindwa kulipia walirudishwa nyumbani au waliacha shule na kusababisha *drop out rate* kuongezeka.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ilipiga marufuku *tuition* tangu mwaka 1990 na mwaka 1991 Afisa Elimu Kiongozi alitoa Waraka Kumb. Na. ED/OK/C.2/4/11 uliotoa ufafanuzi kuhusu taratibu za utoaji masomo ya ziada ya marekebisho *(Remedial Teaching),* bila malipo ikiwa ni hatua ya kurekebisha na kudhibiti hali hiyo. Tangu wakati huo, Wizara imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa Waraka huo na mpaka sasa kuna mafanikio ya karibu asilimia 98. Hata hivyo, yawezekana wapo wachache ambao wamekaidi agizo la Wizara hivyo, tunaomba ushirikiano wa kila Mheshimiwa Mbunge, endapo anafahamu shule ambazo zinaendesha *tuition* kinyume na utaratibu uliowekwa na Waraka huo. Tunaomba atoe taarifa Wizarani ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa dhidi ya wakiukaji.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Walimu katika shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Rufiji kwa kuzingatia maadili ya kazi yao ya ualimu hujitolea kufundisha mafunzo ya ziada kwa wanafunzi wao bila malipo. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwa walimu hao na wengine nchini wa aina hiyo ambao wanazingatia maadili ya kazi yao, kinyume na wale ambao wanaendesha biashara ya madarasa ya *tuition.?* *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niwapongeza sana walimu hao wa huko Rufiji, ambao wanajitolea kufundisha wanafunzi wao mafunzo ya ziada ya marekebisho ambayo kama nilivyosema ni *remedial teaching*, kufanya hivyo ni sahihi kabisa na ningependa walimu hao wachukuliwe kama mfano na wengine wawaige. *(Makofi)*

Napenda katika kujibu swali hili nichukue nafasi hii kuwakumbusha Maafisa Elimu na walimu kwamba, kushamiri kwa *tuition* katika maeneo yao iwe Wilaya au iwe shule ni dalili mbaya ya kwamba, kushamiri kwa *tuition* ile ya malipo ni dalili mbaya, inaonyesha wanafunzi wengi hawashibi madarasani. Kwa hiyo, ni vizuri kufanya jitihada kuhakikisha silabi yote inafundishwa kwa ukamilifu madarasani ili iwe kama wakati tuliposoma sisi wengine hapakuwa na *tuition* za namna hiyo. Kwa hiyo, naomba mfano huo wa Wilaya ya Rufiji uigwe nchini nzima. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Katika mazingira haya ambayo mwalimu mmoja ana wanafunzi 100 mpaka 200 na uhaba wa walimu tulionao, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba angefuata ule usemi wa Kiingereza usemao: *" Don't trouble trouble until trouble troubles you?"* Kwa maana ya kwamba, hali hii inastawi sana mijini siyo Rufiji na kwamba kutokana na *tuition* asilimia 70 mpaka 80 ya wanaofaulu kwenda katika shule za sekondari ni wale wenye mazingira ya kimji mji wanaofanya mambo haya na wenye walimu wengi; je, lini Mheshimiwa Waziri kwa uchambuzi wake anadhani atakuwa na uwiano mzuri wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40 ili angalau akaweza kukanzia maelekezo yake wakati amepunguza mzigo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hali hiyo anayoizungumzia ya wanafunzi hadi 200 darasani ilikuwepo. Kwa mfano, nimesema nilipotembelea Mkoa wa Dar es Salaam wastani ulikuwa 140 kwa darasa. Hii inamaanisha yalikuwepo madarasa mengine yenye wanafunzi karibu 200 katika Jiji la Dar es Salaam. Ni kweli kwamba, hali hiyo wakati huo ilikuwa imeshamiri katika miji mingi madarasa yalikuwa ni makubwa mno. Hii inatokana na sababu za kihistoria tukikumbuka katika sera zetu za kuhimiza elimu, wakati wa Awamu ya Kwanza ya *UPE* tulikuwa na sera iliyokuwa *very clear* kwa vijijini kwamba, shule ya msingi ijengwe katika kila kijiji, lakini hatukuwa na *formular* na msukumo wa ujenzi wa shule katika miji. Kuna miji mingi niseme hawakujenga shule kabisa, kwa mfano, Jiji la Dar es Salaam tangu uhuru kusema kweli hazikujengwa shule nyingine mpaka ilipokuja Tume ya Jiji, iliyoongozwa na Mheshimiwa Charles Keenja, ndiyo iliyokuja kujenga shule 18 pale Dar es Salaam.

Lakini napenda kusema kwamba, kutokana na mpango huu wa MMEM, hali hiyo kwa kweli ni historia. Jiji la Dar es Salaam sasa ambalo limelichukulia kama mfano ni wastani wa wanafunzi 90 kwa darasa, tumeteremka kutoka 140 mpaka 90, na katika hao wanafunzi 90, wastani wa mwalimu kwa wanafunzi ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50. Kwa hiyo, Jiji la Dar es Salaam sasa kwa mtindo wa kufanya *double shift* wanaweza kuwa wanafunzi 45 darasani badala ya wale waliokuwa 140. Kwa hiyo, kinachohitajika ni *double shift* na siyo *double shift* ya walimu wale wale ni kwamba, ile *shift* ya pili inakuja nayo ikiwa na walimu wake kwa sababu ya wastani wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50.

Kwa hiyo, hali anayoizungumzia Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa kweli ni historia. Sasa hivi ukiangalia matokeo ya mitihani utaona hata wa vijijini wameanza kufaulu. Kwa hiyo, akifanya *study* ya sasa hivi atakuta hiyo iliyokuwepo kwamba wanaoendelea na elimu ni wa mijini peke yao kwa sababu ya *tuition,* sasa imeanza kubadilika na wanafunzi wa vijijini wanafaulu, ndiyo maana kuna *demand* kubwa ya ujenzi wa shule za sekondari. *(Makofi)*

Na. 147

**Vyeti vya Kuhitimu Elimu ya Msingi**

**MHE. PASCHAL C. DEGEREA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu wahitimu wa Elimu ya Msingi hawapatiwi vyeti vya kumaliza Elimu ya Msingi:-

(a) Je, ni kwa nini wahitimu wa ngazi hiyo ya elimu hawapatiwi vyeti vyao kwa wakati?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kuwanyima vyeti muhimu wahitimu hao kunawanyima haki yao?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani ya haraka kuondoa hali hiyo ya aibu kwa Taifa letu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuanzia mwaka 1993 wahitimu wa Elimu ya Msingi wamekuwa hawapatiwi vyeti vya kumaliza Elimu ya Msingi. Hali hii ilitokana na sababu za kibajeti, katika kutenga fedha za kuchapisha vyeti hivyo. Hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imechukua hatua za kumaliza tatizo hilo, ili kuondoa kero ya kukosa vyeti kwa wanaomaliza Elimu ya Msingi na pia kuwatendea haki wahitimu. Mahitaji halisi kati ya mwaka 1993 hadi 2002 yalikuwa vyeti 4,184,912. Hadi kufikia Juni, 2003 jumla ya vyeti 4,374, 780 vimechapishwa na kupelekwa katika Ofisi za Afisa Elimu Mkoa kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa ajili ya wahitimu wa kipindi hicho cha mwaka 1993 - 2002. Aidha, Wizara yangu inavyo vyeti vya kutosha kwa wahitimu wa 2003 na inaendelea kuchapisha vyeti kwa watakaohitimu mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tatizo la vyeti vya kuhitimu Elimu ya Msingi sasa halipo tena. Aidha, nachukua nafasi hii kuwaagiza Maafisa Elimu wa Mikoa na Maafisa Elimu wa Wilaya na Walimu Wakuu wote nchini kote, kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi aliyemaliza Elimu ya Msingi kuanzia 1993 hadi 2003 anapewa cheti chake haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa matokeo ya mtihani kwa shule za msingi sasa hivi yameendelea kuwa mazuri na kwa kuwa idadi ya shule za sekondari bado haitoshelezi mahitaji haya. Je, Serikali itakuwa ikitoa majibu ya watahiniwa wote ili kuwapa moyo wazazi na watoto kuweza kuwatafutia nafasi katika shule za watu binafsi za kulipia kwa wale ambao watakuwa hawakupata nafasi katika shule za Serikali?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana naye kwa aliyoyasema kwamba, matokeo ya mtihani wa darasa la saba yameboreka na tumekuwa na wanafunzi wengi. Kwa kweli ni chini ya 4,000 tu kufikia 200,000 waliofaulu. Kwa hiyo, hii ni namba kubwa na ni kweli kwamba tunao ufinyu katika shule za sekondari za Serikali. Lakini kutokana na bajeti ya nyongeza iliyopitishwa na Bunge hili, tutaweza kuchukua wanafunzi wengine karibu 20,000. Kwa hiyo, tutapunguza hiyo *pressure* kidogo.

Lakini ili na shule nyingine ziweze kuwachukua wanafunzi hao zisizo za Serikali, nakubaliana kabisa na ushauri wake kwamba ni ruksa matokeo ya mitihani ambayo Maafisa ya Elimu wa Mikoa na Maafisa Elimu wa Wilaya wanayo, waweze kuyatoa kwa wenye shule wengine ili waweze kuyatumia katika ku-*select* wanafunzi. *(Makofi)*

Na. 148

**Mikopo kwa Wazee**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshatamka kwenye vikao vya bajeti vya miaka ya 2000/2001na 2001/2002 kwamba Sera ya Wazee imekamilika na kwamba wangeanza kufaidika na mikopo kama wanavyofaidika akinamama na vijana:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijatekeleza ahadi hiyo ya kuwapa mikopo wahusika kama ilivyoahidi?

(b) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa kivitendo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wazee vitambulisho maalum ili waweze kupatiwa huduma wanazostahili bure kama vile usafiri wa kwenye mabasi na daladala?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilianza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Wazee kwa kuandaa warsha ya Kitaifa ya Wazee iliyohudhuriwa na wazee kutoka sehemu mbalimbali nchini wapatao 140. Aidha, warsha nyingine ya kisekta iliandaliwa ikishirikisha Wizara za Serikali, Asasi na Wakala za Hiari za Kitaifa na Kimataifa. Kutokana na warsha hizo, rasimu ya Sera ya Taifa ya Wazee iliandaliwa ikizingatia maoni ya wadau wote. Baada ya maandalizi hayo kukamilika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Sera ya Taifa ya Wazee ilipitishwa rasmi katika Baraza la Mawaziri Agosti, 2002 na tayari imezinduliwa. Aidha, Wizara iliandaa mikakati ya utekelezaji ambayo ilipelekwa kwa wadau wote. Kutokana na maoni yao mikakati ya utekelezaji sasa inafanyiwa marekebisho yanayozingatia maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa malengo ya Sera ya Taifa ya Wazee ni kutoa mikopo nafuu itakayowawezesha Wazee kushiriki katika uzalishaji mali na hivyo kuwapunguzia umaskini. Kama nilivyoeleza katika utangulizi wangu, Wizara inafanya maandalizi ya utekelezaji wa sera hii kwa kukamilisha mikakati ya utekelezaji. Hatua itakayofuata ni pamoja na Serikali kuridhia mikakati ya utekelezaji na Wizara kufanya majadiliano na Hazina kuhusu uanzishwaji wa Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali zinazolenga katika kuboresha maisha ya Wazee. Hatua hizi ni pamoja na kuongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu, kuwapatia matibabu bila malipo Wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi wasio na uwezo. Pamoja na kutambua umuhimu wa wananchi kuwa na vitambulisho. Wizara kwa sasa haina mpango wowote wa kutoa vitambulisho maalum kwa Wazee kwa lengo la kuwapatia huduma bure.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2001/2002, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akihitimisha hotuba yake ya bajeti aliahidi mpango huo wa kuwasaidia Wazee na alikuwa ananilenga mimi katika jibu hilo kwamba ungeanza mwaka wa fedha huo wa 2001/2002, lakini inapelekea kuwa bado majibu hayajafika popote. Lakini katika bajeti ya mwaka 2001/2002 Waziri alitamka rasmi Bungeni akinijibu kwamba, hiyo mikopo ya wazee ingeanza mwaka huo wa fedha. Sasa majibu ya leo yanaonekana kwamba bado hatujafika huko. Ahsante.

**SPIKA:** Umesikia sawa sawa Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Sikusikia.

**SPIKA:** Hebu rudia tena.

**MHE. PETER KABISA:** Basi naomba nafasi niendelee.

Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza ni kwamba, kwenye bajeti ya mwaka 2001/2002 Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali langu Bungeni alisema kwamba misaada na mikopo kwa Wazee ingeanza kwenye bajeti ya mwaka huo wa fedha. Lakini hapa inaonekana bado hii mikopo haijafikiriwa kuanzishwa hata hivi leo kuanzia 2001/2002.

**SPIKA:** Mmm! Uliahidi Mheshimiwa Waziri, lete jibu sasa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ama binafsi sikumbuki kuwa Mheshimiwa Waziri, alitoa jibu la namna hiyo. Kwa kweli yeye binafsi Mheshimiwa Kabisa, nimeshazungumza naye juu ya kauli hii hii aliyoitoa leo hapa kwamba, hatuikumbuki na isingewezekana tuanzishe mkopo kwa Wazee hata bila ya Serikali kuanzisha mfuko wa namna hiyo na hata bila ya sera yenyewe ya Wazee kukamilika.

Sasa kama Sera hii ya Wazee imekamilika mwaka 2003 na kuzinduliwa Septemba halafu 2001/2002 Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi kwamba, mikopo ingeanza muda huo. Nafikiri pengine labda misaada aliyokuwa anaizungumzia Waziri ni hii ambayo tunaendelea kuongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu, kutoa matibabu bure kwa Wazee na kuendelea kutoa huduma katika majengo ya Wazee kama vile Nunge pale Kigamboni. Nafikiri labda alichanganya kati ya huduma hizo na huduma ya mikopo kwa Wazee.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwanza, naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuongeza malipo ya uzee kwa Wazee waliostaafu. Lakini kuna Wazee ambao walichukua mkupuo uliolipwa kwa kukadiria kwamba wangeishi kwa muda wa miaka kadhaa na kwa bahati Mungu anawalinda wanaendelea kuishi. Wizara inawafikiriaje mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, bila shaka Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, Waziri wa Fedha alipokuwa anachangia hoja yake hapa alizungumzia kwa kirefu suala hili kwamba, Serikali sasa inafanya utaratibu wa kuweza kuwalipa sasa kila mwezi. Lakini utaratibu huo sio kwamba, unaandaliwa siku hiyo hiyo na ni lazima uandaliwe kwenye bajeti. Kwa hiyo, mimi nafikiria kwamba, yale yaliyozungumzwa na Waziri wa Fedha yalizungumzwa kwa niaba ya Serikali yote na yatatekelezwa bila shaka na nitafikisha salamu hizi kwa Waziri wa Fedha leo hii hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa vikao vya bajeti ndogo vimekwisha sasa tumerudi kwenye utaratibu wetu wa kawaida wa kipindi cha saa 1.30 kwa maswali.

Na. 149

**Mkakati Endelevu wa kusaidia Vijana Nchini**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kumekuwepo na wimbi la vijana katika nchi yetu na dunia ya tatu kwa jumla kuhamia mijini kwa matarajio ya kupata maisha bora; na kwa kuwa wafikapo mijini vijana hao ama hujiingiza kwenye vitendo vya ujambazi, wizi, ubakaji, matumizi ya madawa ya kulevya na kadhalika au kujihusisha na shughuli za biashara ndogo ndogo kama uuzaji wa mitumba, uuzaji wa bidhaa za mikononi ambazo hazina mwelekeo wa kuwakwamua kimaisha:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kuwa na mkakati wa kuwaelimisha vijana kujiunga vijijini au kwenye maeneo maalum ili kujishughulisha na kilimo, viwanda vidogo vidogo, uvuvi, ufugaji wa kisasa na kadhalika?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani unaohakikisha kuwa nguvu ya vijana hao inatumika kwa manufaa ya Taifa na maendeleo yao kwa jumla?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wanaohamia mijini kwa matarajio ya kupata maisha bora. Hata hivyo, kinyume na matarajio yao hujikuta katika vitendo vya uhalifu kama ujambazi, wizi, ubakaji, matumizi ya madawa ya kulevya, ushoga na ukahaba. Aidha, kuwaelimisha na kuwahamasisha vijana kujiunga pamoja vijijini na kuunda vikundi vya uzalishaji mali na kuwasaidia kupata mikopo nafuu na nyenzo za kufanya kazi ni mkakati unaoweza kusaidia kupunguza wimbi la vijana kukimbilia mijini.

(b) Serikali inatambua wazi vijana kuwa ndiyo nguvu kazi ya Taifa, hivyo basi, mchango wao katika kuinua Pato la Taifa unahitajika sana. Serikali chini ya programu za vijana kama vile vikundi vya vijana vya uzalishaji mali (VVKM), unawezesha vijana kujiajiri wenyewe na kuchangia Pato la Taifa. Aidha, Programu ya *Vijiwe* iliyoanzishwa na Wizara inalenga katika kupata takwimu za vijana kujua wako wapi, idadi yao na wanafanya nini, ili kuweza kutumia maeneo hayo kama sehemu za kuzalisha mali.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kuuliza tu swali moja la nyongeza.

Nashukuru kwa majibu yake mazuri. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba, kwa kuwa hawa vijana inaonekana hakuna mtu ambaye anawapa elimu ya kutosha ya kwamba biashara hiyo wanayoifanya haiwezi kabisa kuwaletea maendeleo wala kuinua maisha yao, kwa hiyo basi, kuna ulazima au haja ya kuunda chombo maalum kila Mkoa au kila Wilaya ambacho kitatoa ushauri nasaha kwa vijana kuwaelimisha namna gani wanaweza wakaishi maisha mema badala ya kukimbizana na soda na mifuko wanayotumia ili kuweza kuinua maisha yao wakipata elimu hiyo ingewasaidia. Je, Waziri haoni kwamba, ni vizuri kuanzisha kikosi cha kusaidia kuelimisha hawa vijana vijijini na mijini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na wazo lake kama moja ya sehemu ya kutoa elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba, wakati Bunge likijadili bajeti yetu ya 2001/2002, walitoa mapendekezo kwamba ni vyema tukafuata vikundi hivyo vilipo, hivi vinavyoitwa *Vijiwe* ili tuweze kupata maoni ya wadau wenyewe, vijana. Tumeanza kutekeleza agizo lile mwaka 2002/2003 na kwa Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni, tumekamilisha tumegundua aina ya Vijiwe 11 vinavyofanana katika Jiji la Dar es Salaam na kwa ruhusa yako Vijiwe hivyo ni vile Vijiwe vya maongezi ya kawaida, Vijiwe vya kupanga mikakati mbalimbali ya vitendo viovu, Vijiwe vya wavuta bhangi na matumizi ya madawa ya kulevya, Vijiwe vya vibaka na waporaji, Vijiwe vya wapiga debe, Vijiwe vya *day workers*, Vijiwe vya kisiasa, Vijiwe vya michezo, Vijiwe vya biashara ndogo ndogo na Vijiwe vya machangudoa na wanaume wanaouza miili yao. *(Kicheko)*

Tumejaribu kuzungumza nao na kupata mawazo yao. Kwa kweli tumeona ni vyema kuzungumza nao kama wadau na tumeweza kupendekeza njia za kuwasaidia. Hivi sasa uchunguzi huu unaendelea katika Mikoa ya Ruvuma, Kagera, Kigoma na Mbeya. Naamini pamoja na njia uliyopendekeza Mheshimiwa Simpasa, tutapata ufumbuzi wa matatizo ya vijana wetu.

Na. 150

**Mifereji ya Asili ya Umwagiliaji Tarafa ya Sale**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (k.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika zaidi kwani nchi haiwezi kujitosheleza kwa chakula kwa kutegemea mvua tu katika kilimo; na kwa kuwa katika Vijiji vya Sale, Samwange, Digodigo, Kisangiro, Oldonyo-Sambu na Pinyingi, Tarafa ya Sale Wilayani Ngorongoro, ipo mifereji ya asili ya umwagiliaji:-

(a) Je, Serikali ina habari za mifereji hiyo ya asili na inatumika kumwagilia ekari ngapi za mazao?

(b) Je, Serikali itatoa misaada gani kusaidia nguvu za wananchi wanaotumia mifereji hiyo ili kuboresha na kuimarisha mifereji hiyo ya asili, kwa lengo la kuendeleza kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina habari za mifereji ya asili inayotumika kumwagilia maji mashambani katika Tarafa ya Sale, Vijiji vya Digodigo, Mugholo, Kisangiro, Oldonyo-Sambu, Samwange na Pinyingi. Kutokana na uchunguzi uliofanywa chini ya Mpango Kamambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, jumla ya hekta 800 zinamwagiliwa kwa kutumia mifereji hiyo.

Mazao yanayolimwa kwenye eneo hilo ni mahindi, maharage na viazi vitamu kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maji ambavyo ni pamoja na chemchemi za Bisamawe, Bisabwa na Samwange, Mto Tinaga na maji yanayotiririka toka milima ya nchi jirani ya Kenya.

(b) Napenda nikiri kwamba, zaidi ya tathmini iliyotolewa katika Mpango Kamambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji kuhusu mifereji hiyo, Wizara haijaanza kuifanyia kazi ya kuiendeleza. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro inashauriwa kuomba fedha za kuendeleza mifereji hiyo katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa 2004/2005, kupitia Mpango wa Wilaya wa Kuendeleza Kilimo *(District Agricultural Development Plan - DADP).*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro ina Tarafa 3, Ngorongoro, Loliondo na Sale na Tarafa ya Ngorongoro hawaruhusiwi kulima; na kwa kuwa Tarafa zilizobaki hizo mbili zina mifereji ambayo inaweza ikalisha Wilaya nzima ya Ngorongoro wakisaidiwa kwa umwagiliaji; je, Serikali isingewapa kipaumbele Wilaya ya Ngorongoro kutokana na Tarafa moja kunyimwa nafasi ya kulima?

Pili, kwa kuwa Mto wa Harashi unapita karibu na Shule ya Bweni ya Harashi, isingekuwa muhimu kuwasaidia Kijiji cha Hale pamoja na shule ya msingi ili waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama tulivyosema katika jibu la msingi, Ngorongoro wangependa kulima na imekatazwa, naomba Halmashauri husika ya Ngorongoro ilimalize huko huko tatizo hilo. Nikilitatua mimi hapa nitavuruga taratibu za Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, tumesema mipango yote ya umwagiliaji ipitie *District Agriculture Development Fund.* Wafanye hivyo na hivyo tatizo hilo la kulima kwenye shule uliyoitaja litatatuliwa. *(Makofi)*

Na. 151

**Simu katika Jimbo la Chambani**

**MHE. SALIM OMAR ALI (k.n.y. MHE. KARIM SAID OTHMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu; na kwa kuwa Jimbo la Chambani limepakana na Bahari ya Hindi kwa sehemu kubwa ambapo kuna mambo mengi ya hatari ambayo huchukuliwa na maji kutoka Bahari Kuu na kuegeshwa ufukweni mfano, mabomu, mapipa yaliyojazwa mambo yasiyofahamika; na kwa kuwa wananchi hulazimika kutembea km 20 kutoa taarifa kwenye Kambi ya Jeshi au Polisi ili waje kuona ni jambo gani hilo au kutoa ufumbuzi wowote; na kwa kuwa wananchi katika vijiji 35, shule 5 za Msingi na Sekondari, Kambi ya JKU, Zahanati ya Chambani, Ofisi ya *CBO - CHADECO* na Kituo cha Kilimo Chambani ni orodha ya mahitaji ya simu ambayo yana uhakika:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwawekea simu watu hao wa Jimbo la Chambani?

(b) Je, ni lini Serikali itawafungia simu za mitambo ya kisasa na sio simu za karne ya 10 za kukoroga?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania, inauona umuhimu wa kuwapelekea mawasiliano wananchi wa Jimbo la Chambani lakini uhaba wa fedha ndio kikwazo kikubwa. Hata hivyo, kwa kuanzia, Kampuni ya Simu Tanzania itafanya tathmini ya biashara ya simu katika Jimbo la Chambani na zile sehemu zitakazokidhi masharti ya Kibiashara zitaingizwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Kampuni hiyo wa mwaka 2004/2005 kama fedha zitapatikana. Nia ya Kampuni ya Simu Tanzania ni kuboresha mawasiliano ya simu na kufunga mitambo ya kisasa na kuondosha ile mitambo ya simu za kukoroga.

Na. 152

**Meli ya M.V. Liemba**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa meli ya M.V. Liemba iliyoundwa mwaka 1913 ndiyo meli Kongwe duniani kote ambayo bado inafanya kazi ya usafirishaji wa abiria na mizigo; na kwa kuwa meli hiyo kwa upande wa Tanzania ni tunu kwa historia ya nchi yetu; na kwa kuwa kuna mipango ya ubinafsishaji/ama ukodishaji wa *Management;* je, Serikali ina mipango gani juu ya Meli hiyo yenye historia kubwa duniani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, meli ya M.V. Liemba ndiyo meli kongwe duniani ya abiria ambayo bado inafanya kazi ya usafirishaji wa abiria na mizigo na kwamba kwa upande wa Tanzania ni tunu, kwa historia ya nchi yetu. Serikali katika mipango yake ya kubinafsisha Kampuni ya Huduma za Meli, imeamua kuendelea kuwa na hisa chache katika vyombo hivyo ili iwe na sauti juu ya uendeshaji wa vyombo vyenyewe. Aidha, Kampuni ya Huduma za Meli itagawanywa katika vitengo kwa kila Ziwa na kuundwa

Kampuni za Usafiri. Hivyo, suala la meli M.V. Liemba litaangaliwa chini ya Kampuni husika kwa kuzingatia umuhimu wa historia ya meli hiyo kongwe duniani.

Na. 153

**Kugharamia Watuhumiwa**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwananchi yeyote akikamatwa anafanya uhalifu wa aina yoyote na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ni jukumu la Jamhuri kuhakikisha kuwa haki inatendeka hadi mwisho ili mtu huyo aachiwe au kufungwa:-

(a) Je, ni kwa nini hivi sasa umezuka mtindo wa Serikali kuwatupia mzigo wananchi na hasa waliotendewa uhalifu kama kuibiwa, kupigwa au kukosewa haki, kuambiwa wawagharamie wanaotuhumiwa katika Mahakama za Chini ili kupelekwa Gerezani au katika Mahakama ya Juu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huku ni kumkosesha haki yule asiye na uwezo wa kumgharamia mhalifu pale mhalifu huyo anapoachiwa kwa sababu ya kutokuwa na fedha ya kumfikisha katika chombo cha juu kinachohusika?

(c) Je, ni lini hasa Wizara ya Mambo ya Ndani itaondoa kero hiyo kwa wananchi vijijini kwa kuhakikisha kuwa, usafiri wa wahalifu unapatikana wakati wote wakihukumiwa na Mahakama za Mwanzo wanapopelekwa jela ili wasigharamiwe na wanaowashtaki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali ni kwamba, mhalifu anapokamatwa na Polisi au raia wema, jukumu la kugharamia chakula akiwa rumande na la kumsafirisha kumpeleka Mahakamani na hata kumpeleka Gerezani kama atahukumiwa kifungo ni la Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaratibu huu unalenga kuhakikisha kuwa, haki inatolewa sawa kwa wote na siyo kwa wale tu wenye uwezo wa kifedha na kuwagharamia wahalifu. Kwa hiyo, wahalifu vijijini wakihukumiwa kufungwa jela na Mahakama za Mwanzo, Serikali ndiyo inayopaswa kuwasafirisha kwenda jela kutumikia vifungo vyao. Walalamikaji hawawajibiki Kisheria kuwalisha chakula wahalifu wakiwa rumande, kuwasafirisha kwenda Mahakamani, wala Gerezani, hilo ni jukumu la Serikali.

Hata hivyo, kutokana na tatizo la muda mrefu la ufinyu wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, jukumu hili limekuwa halitekelezwi kwa ukamilifu. Hali ya uchumi ikiboreka, Serikali itapata uwezo mkubwa wa kutekeleza jukumu hili kwa ukamilifu zaidi. Hivyo, kero hii itapungua hatua kwa hatua kwa kadri kasma ya kuhudumia wahalifu itakavyoongezwa na Bunge hili Tukufu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ni kazi ya Serikali kufanya shughuli hii ya kuwasafirisha wahalifu na kero hii imekuwa ni kubwa; na kwa kuwa huko nyuma hata Wazee wa Mabaraza ya Mahakama walikuwa na tatizo kama hilo sasa tatizo hilo limeondolewa; je, si wakati muafaka sasa Wizara ikahakikisha katika bajeti ijayo fedha zinatengwa za kutosha ili wafungwa au wahalifu wawe wanasafirishwa bila matatizo katika nchi nzima?

Swali la pili, kama ni suala hili la kusafirisha watuhumiwa au wafungwa ni kazi ya Serikali, je, wale ambao wameshafanya kazi hii ya kuwasafirisha wafungwa na kuwalisha Gerezani wanaweza wakaidai Serikali ili waweze kupata fidia kwa kazi waliyoifanya huko nyuma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba, jukumu la kuwalisha wahalifu wakiwa rumande na kuwalisha au kuwasafirisha kuwapeleka kwenye Mahakama, kimsingi ni jukumu la Serikali na kwamba Wizara yetu ilikuwa inaweka bajeti kusema kweli haitoshi, lakini bajeti ipo kwa ajili ya kazi hii. Kwa mfano, mwaka 2001 zilitengwa shilingi 92.6 milioni kwa ajili hiyo. Mwaka 2002 shilingi 240 milioni kwa ajili hiyo na mwaka 2003/2004 sasa Bunge hili limepitisha shilingi 350 milioni kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, bajeti inayotengwa na kazi hii imeanza kupungua.

Nyongeza tu kwamba, kwa wale ambao wanafungwa kwenye Vituo vya Polisi na Mahakama za Mwanzo huko, utaratibu wa wale ambao wanawapelekea chakula wanarejeshewa zile fedha, isipokuwa wale ndugu wanaojitolea wenyewe. Kama mtoto wangu yuko rumande nampelekea chakula changu pale kwenye Kituo cha Polisi, hiyo inaruhusiwa. Wale ambao wanawalisha kwa mkataba wa fedha, fedha hizi zinatumika kuwarejeshea. Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tatizo hili kwa kweli sasa linapungua kwa kasi kabisa na bajeti inayokuja kama fedha zitakuwa nyingi kama za mwaka huu, tutalimaliza kabisa.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika hali halisi ilivyo ni kwamba hivi sasa mahabusu katika magereza yetu ni wengi kuliko wafungwa, hali inayoashiria kwamba labda yako matatizo ya Kisheria au ugumu wa upatikanaji wa dhamana kwa wakosaji au watuhumiwa. Je, Serikali haioni kwamba, ipo sababu sasa ya kuangalia upya sheria zetu ili wananchi waweze kupata dhamana kwa urahisi na hatimaye tuweze kupunguza msongamano wa mahabusu waliopo magerezani hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza si sawa kabisa kwamba mahabusu ni wengi kuliko wafungwa. Kwa mfano, mwezi Januari, tulikuwa na watu Magerezani karibu 47,000 kati ya hao 26, 000 walikuwa ni wafungwa na mahabusu walikuwa 21,000. Kwa hiyo, idadi ya mahabusu ni wengi lakini haizidi ya wafungwa. Ni wengi kwa sababu nyingi, moja ni hiyo aliyoitaja ya dhamana kwamba ni kweli katika hawa 21,000 ambao walikuwa gerezani mwezi uliokwisha ukienda kuwauliza utakuta karibu asilimia 80 dhamana zao ziko wazi ila wameshindwa kukamilisha yale masharti ya dhamana. Suala hili tunazungumzia kati ya sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na wenzetu wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ili kuona kama tunaweza kuyatimiza yale masharti ambayo yanawashinda wengi kama yanaweza yakalegezwa bila ya kuathiri zile kesi ambazo kisheria hazina dhamana.

Lakini vile vile msongamano unasababishwa na kesi kuchelewa kwa sababu upelelezi umechelewa. Hilo lipo moja kwa moja ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani na tunalifanyia kazi.

Na. 154

**Wahamiaji Haramu**

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE** aliuliza:-

Kwa kuwa uhalifu umekithiri katika Mikoa ya Dar es Salaam na baadhi ya Mikoa ya mipakani mwa Tanzania; na kwa kuwa wengi wa majambazi hao kwa sasa ni wahamiaji haramu kutoka baadhi ya nchi jirani na Tanzania:-

(a) Je, Serikali inaliambia nini Bunge kuhusu wahamiaji wa aina hiyo?

(b) Je, ni nini wito wa Serikali kwa nchi jirani ambazo raia wake wameshukiwa kufanya uhalifu huo hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wimbi la uhalifu limeongezeka nchini na hasa katika Mikoa ya mipakani, ambayo imeathirika zaidi kutokana na uhamiaji haramu na ujio wa Wakimbizi wanaokimbia machafuko katika nchi zao. Mikoa hiyo ni pamoja na Kigoma, Kagera na Rukwa, ambayo inapakana na nchi za Rwanda, Burundi na Kongo *(DRC)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inayajua madhara yanayotokana na wahamiaji haramu. Ni kutokana na ukweli huo, Serikali imekuwa ikiendesha misako madhubuti ya mara kwa mara dhidi ya wahamiaji hao na kuwachukulia hatua kali ikiwa ni pamoja na kuwafungulia mashtaka Mahakamani, kuwafunga na kuwarejesha kwenye nchi zao. Misako hiyo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kati ya Januari na Desemba, 2002 wahamiaji haramu 1,768 walikamatwa na kati ya Januari hadi Agosti, 2003 wahamiaji haramu 3,373 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Serikali itaendelea kupambana na wahamiaji hawa haramu hadi tatizo hili litakapomalizika kabisa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahamiaji haramu wanatokana na wimbi kubwa la Wakimbizi wanaoingia nchini mwetu kufuatia migogoro ya kisiasa na kikabila katika nchi jirani, Serikali itaendelea na ushawishi wake kwa nchi zenye migogoro ya kisiasa ili zikomeshe migogoro yao na hivyo kurejesha amani nchini mwao na hatimaye kuwawezesha wananchi waliokimbilia nchini mwetu kurejea katika nchi zao na hivyo kuinusuru nchi yetu na wimbi la wakimbizi.

Aidha, tunaziarifu nchi majirani zetu ambazo raia wao wanapokuwa hapa nchini kama Wakimbizi au kwa sababu nyingine, wanajihusisha na vitendo vya uhalifu kwamba, tunayo haki kulinda raia wetu na mali zao, hivyo, tunapowashughulikia raia wao kwa kufanya uhalifu, tunalinda maslahi ya nchi yetu na watuelewe hivyo.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekiri kuongezeka kwa wahamiaji wahalifu, je, Serikali iko tayari sasa kuongeza Jeshi katika mipaka yetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ilivyo katika mipaka yetu na hasa uingiaji wahamiaji haramu na Wakimbizi, mawazo aliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuimarishe ulinzi katika maeneo hayo tayari yanatekelezwa. Jeshi la wananchi liko katika mipaka yetu yote likiwa na nguvu ya kutosha kulinda mipaka hiyo. Vile vile Jeshi la Polisi tumeongeza nguvu katika maeneo ya mpakani, tumepeleka vikosi vya ziada katika maeneo ili wasaidiane na Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi kulinda mipaka yetu. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, mipaka yetu inalindwa vilivyo na Watanzania wasiwe na wasi wasi wowote.

**SPIKA:** Samahani nilikosea kutaja jina, Mheshimiwa Salim Omar Ali, nilimwita Mheshimiwa Ali Said Juma. Samahani sana.

Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo, inabidi tuendelee na shughuli nyingine. Matangazo ya vikao. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawakumbusha Wajumbe kwamba Kamati hiyo itakutana leo tarehe 18 kujadili taarifa ya kazi za Kamati kwa mwaka uliopita Chumba Namba 231 na kikao kitaanza saa 5.00 asubuhi hii. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anawatangazia Wajumbe kwamba, kutakuwa na kikao leo tarehe 18 saa saba mchana, Chumba Namba 432 ghorofa ya nne. Hivyo ni vikao vya Kamati. Vikao

vingine ni kama ifuatavyo: Tawi la *CPA Tanzania,* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jackson Makwetta, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* wa Tawi letu kwamba, kutakuwa na kikao leo saa 5.00 asubuhi Chumba Namba 227.

Halafu Chama cha Wabunge cha masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Kimiti, anawatangazia Wanachama wa Chama hicho kwamba, kutakuwa na kikao leo saa 7.00 Chumba Namba 428 ghorofa ya nne.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anawatangazia Wabunge wa Mkoa wa Pwani kwamba, wakutane Chumba Namba 133 leo saa 7.00 mchana. Hayo ni matangazo kwa upande wa vikao.

Kuhusu ratiba inayoendelea ni kwamba, tumekutana na Kamati ya Uongozi na waliamua kwamba, zile taarifa za kila Kamati ambazo zingewasilishwa kwenye Mkutano huu ni bora zisubiri ili kutoa nafasi kwa Hotuba ya Rais iweze kujadiliwa kwa undani, ndiyo maana nikatangaza kwamba, sasa mlango uko wazi kwa wanaopenda kuchangia walete maombi. Mpaka leo tumepata maombi 65. Wabunge 10 walishasema jana, waliobaki ni 55 na tukumbuke kwamba, Bunge litafungwa siku ya Ijumaa ijayo. Kwa hiyo, tutajaribu kuwapa nafasi wote kadri itakavyowezekana ili waweze kutoa michango yao kwenye Kotuba ya Rais.

Mwisho wa matangazo. Katibu, tuendelee na *Order Paper.*

## UCHAGUZI WA KAMISHNA WA TUME YA HUDUMA ZA BUNGE

**ND. KIPENKA M. MUSSA - KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wagombea wawili, Mheshimiwa *Major* Jesse J. Makundi na Mheshimiwa Asha A. Ngede. Ningeomba watoke nje halafu wataitwa kwa ajili ya kujieleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Utaratibu wetu tunaufahamu, watapewa nafasi ya kujieleza hapa mbele, tutawauliza maswali kama yapo, lakini kwa kuwa Tume ya Huduma za Bunge inaendesha shughuli zake kwa Kiswahili, basi watajieleza kwa Kiswahili, siyo kwa Kizungu. *(Makofi)*

Sasa, naomba wote wawili watoke nje ili tumwite mmoja baada ya mwingine kama wamo ndani. *(Makofi)*

*Hapa (Mhe. Asha A. Ngede) Alitoka Nje ya Ukumbi wa Bunge*

**SPIKA:** *Order, order, order. Sergeant-at-Arms* mfungulie mlango Mheshimiwa Jesse Makundi, aingie.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Hebu subiri kwanza, bado *Sergeant-at-Arms* hajaripoti.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Mwite aliyebaki Mheshimiwa Asha Ngede aingie.

*Hapa (Mhe. Asha A. Ngede) Aliingia Ukumbini*

**SPIKA:** Jamani, taratibu za uchaguzi tunazijua, tunawasikiliza kimya tu, halafu kazi unaifanya kwenye karatasi.

**MHE. ASHA A. NGEDE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waheshimiwa Mawaziri wote, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, habari za asubuhi na heri ya mwaka mpya.

**WABUNGE FULANI:** Nzuri, heri na wewe pia.

**MHE. ASHA A. NGEDE:** Mimi naitwa Asha Ali Ngede, nimesimama hapa naomba kura zenu ili niwe Mjumbe miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Bunge na niweze kufanya kazi kwa maslahi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waheshimiwa Mawaziri wote na Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kura zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mara ya pili, kuna maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mara ya tatu, kuna maswali?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngede, rudi kwenye kiti chako.

Waheshimiwa Wabunge, nimearifiwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwamba, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi ni mgonjwa yuko hospitalini ndiyo maana hakuja hapa kujieleza. *Returning Officer,* tuendelee kugawa karatasi.

*(Hapa Karatasi za Kupigia Kura Ziligawanywa kwa Wabunge)*

**SPIKA:** *Returning Officer,* masanduku ya kukusanyia kura yaandaliwe. Yaonyeshwe kama yako wazi, halafu endelea moja kwa moja kukusanya kura.

*(Hapa Kura Zilizopigwa Zilikusanywa kutoka kwa Wabunge)*

**SPIKA:** Kanuni zinanitaka niteue wasimamizi wawili wa kuwa mashahidi katika kuhesabu kura. Kwa hiyo, namteua Mheshimiwa Frank Maghoba na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, njooni msindikize masanduku ya kura kwenda kuhesabiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kura zitahesabiwa *Speaker's Lounge.* Wakati huo huo sisi tunaendelea na *Order Paper*, Katibu endelea.

## HOJA ZA SERIKALI

## HOJA YA KUJADILI HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA BENJAMIN WILLIAM MKAPA

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kama walivyotangulia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kusema hapo jana, nami pia napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake nzuri, ambayo imechambua hali halisi ya Tanzania katika nyanja zote muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais, imeelezea mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na utekelezaji wa Ilani ambao umefanywa na Serikali kutimiza ahadi nyingi ambazo Chama cha Mapinduzi kilikuwa kimeahidi kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi hasa kwenye Jimbo langu la Uchaguzi, kwa kutimiza ahadi kadhaa. Ipo ahadi moja ambayo Marehemu Mheshimiwa Dr. Omar Ali Juma, aliyekuwa Makamu wa Rais, aliyoitoa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, haijatimizwa. Ninaomba nichukue nafasi hii kukumbushia, nayo ni ahadi ya kuleta simu katika Mji wa Sikonge. Tunayo matatizo makubwa sana ya mawasiliano na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninaipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya barabara ya Tabora - Ipole - Koga na Ipole - Rungwa. Lakini naomba yale yanayoendelea katika utengenezaji wa barabara hii, basi ni vizuri na sisi Waheshimiwa Wabunge, tungekuwa tunapata taarifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niende moja kwa moja katika mambo mawili makubwa ambayo nataka nichukue nafasi kuyazungumzia. La kwanza ni suala la kilimo. Kama walivyotangulia kusema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kweli ni kilimo pekee kama tukikipa nguvu ya kutosha basi kinaweza kikatufikisha mahali Wananchi wetu wakaondokana na hali mbaya ya umaskini ambayo wanayo.

Mheshimiwa Spika, ipo lugha ya sasa hivi ya kuzungumzia matrekta, sipingi, lakini ninachotaka kusisitiza ni kwamba, kilimo hata hiki tulichonacho sasa hivi ambacho Wananchi wetu wanatumia jembe la mkono bado hawajaweza kulima vizuri. Tukishaweza kulima vizuri hata kwa jembe la mkono, basi tunaweza tukawa na ufanisi mkubwa sana katika suala zima la kujitosheleza kwa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachukua mfano kidogo tu. Nikiwa kule Jimboni natembea tembea kwenye mashamba na ninajua hili lipo katika maeneo mengi, bado Wananchi wetu hawajapata elimu ya kutosha na tukiwemo humu tunapiga sana kelele kuhusu suala zima la Maafisa Ugani wetu kupita kuwashauri Wananchi wetu. Binafsi nina hakika kabisa bado Wananchi wengi hawajajua wanalima wakati gani, bado hawajajua namna ya kupanda mbegu na bado hawajajua kutumia mbolea. Haya ni matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatujaweza kuwafanya Wananchi wetu waweze kulima kutumia kanuni bora pale ambapo wanatumia jembe la mkono, basi hata huko tunapotafuta kulima mashamba makubwa kwa trekta hakutatusaidia sana. Kwa hiyo, napenda nisisitize kwamba, Serikali ielekeze nguvu sasa hivi ya kuwafundisha wakulima wetu waweze kutumia kanuni bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuzungumzia suala la rushwa. Pamoja na kwamba matatizo kadhaa ya rushwa bado yapo, lakini napenda nichukue nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi hasa katika uchaguzi wa mwaka 2000. Uchaguzi wa mwaka 2000 kura za maoni za watu waliowania nafasi kadhaa hasa za Ubunge, zilituonyesha kabisa kwamba, kuna watu wanataka kutumia fedha kupata uongozi, lakini Chama cha Mapinduzi kilipowabaini kiliwaengua. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kwa kweli kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaelekea kwenye uchaguzi na kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi, ni lazima tuanze kujenga mikakati ya kuondoa rushwa ya siasa. Rushwa ya siasa inafanywa na Wanasiasa. Kwa hiyo, sisi humu tunaweza tukawa miongoni mwao kwa sababu ni wadau wakubwa wa siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenzangu jana, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, sisi vijana tuliolelewa katika misingi ya kisiasa ambayo hasa ilikuwa ya Azimio la Arusha, tunaona utaratibu wa sasa wa kupata viongozi katika nchi yetu unaweza ukafika mahali ukawa uongozi wa watu wenye fedha na hii ni hatari sana. Kiongozi yeyote anayetafuta uongozi kwa fedha yule kwanza hafai, hajiamini na ndiyo maana anatumia fedha ili apate uongozi. Hatari sana, tutaifikisha nchi yetu mahali pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipata nafasi siku moja ya kwenda kusimamia uchaguzi mahali. Kulikuwa na wagombea wawili na mgombea wa kwanza alikuja na mkewe. Kura zilipopigwa pale, yule mgombea

aliyekuja na mkewe alipata kura moja na kwa maana hiyo ilikuwa ni kura ya kwake peke yake. Sasa, baada ya mimi kutangaza matokeo, yule bwana aliyekuja na mkewe alisimama akasema: “Mheshimiwa msimamizi, mimi nakubali matokeo, lakini nataka nimuulize mke wangu, kura ya kwake alimpa nani?” Yule mkewe alisimama pale akasema: “Mheshimiwa msimamizi, ni kweli kabisa mimi kura yangu sikumpa mume wangu. Katika masuala ya kunioa yeye anastahili, lakini katika masuala ya uongozi niliona hatoshi.” *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoelekea kwenye uchaguzi, kama Mheshimiwa Rais, alivyotuonya kwamba, tunatakiwa tuchague viongozi ambao wana uwezo wa kuwakaribia watu, wana uwezo wa kujali shida za watu, wasiwe viongozi ambao kwa kweli wanatafuta uongozi kwa maslahi yao. Hii biashara ya kununua kura ni ya hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara hii ninaifananisha na mnunuzi. Ukienda dukani unatafuta kipande cha sabuni, utatoa fedha yako na yule mwenye duka atakukabidhi kile kipande. Biashara yako wewe na yule anayeuza huwa imeishia hapo, haiendelei. Hata watu wanaotafuta uongozi kwa fedha ni hivyo hivyo, akishawanunua watu kwa fedha hatakuja kuwasaidia Wananchi na kujali matatizo yao kwa sababu alikwishatoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli napenda nisisitize kabisa kwamba, huyu mdudu rushwa Serikali na Vyama vyote vya Siasa visimame imara kuhakikisha kuwa chaguzi zetu zinakwenda katika utaratibu ambao hatutaruhusu mwanya wa rushwa uingie. Sasa, rushwa za kisiasa zipo nyingi na napenda nitoe mfano mwingine. Sasa hivi kumezuka utaratibu, wewe una Jimbo lako la uchaguzi, unaondoka unakwenda kugawa chakula kwenye Jimbo la mtu mwingine, hivi Wananchi wako wewe hawana shida? Ni jambo la hatari sana hili! Tukienda kwenye Jimbo lako hatutakuta watu ambao hawana chakula? Tutawakuta wengi hawana chakula wanashinda na njaa, unatoa chakula unakwenda kugawa kwenye Jimbo la mtu mwingine, hii ni rushwa ya kisiasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujenge mazingira ya kuwasaidia Wananchi ambao umegawiwa kwenye mipaka yako ya kazi.

**WABUNGE FULANI:** Ni akina nani?

**MHE SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, siwataji, ila nilikuwa nasisitiza haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika hali ya kisiasa kumekuwa na manung’uniko mengi kabisa kwamba, Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi, kimekuwa kinaingia kuharibu taratibu za Vyama vya Upinzani. Si kweli, kwa sababu kama Vyama vya Kisiasa haviwezi kujenga demokrasia ndani ya Vyama hivyo, bado tutaendelea kuwa na migogoro kwa Vyama vya Upinzani siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, nimewasikia baadhi ya watu wamekwishajitangaza kuwa wagombea. Unajitangaza kuwa mgombea Urais hata mkutano ambao uko kwa mujibu wa Katiba haujakupigia kura! Pia, kuna matatizo mengi sana ya ruzuku. Juzi juzi kulikuwa na uchaguzi hapa, Chama kimoja kilifanya uchaguzi. Watu walirudi nyumbani wana matatizo makubwa. Mtu anatoka anasema anaenda kwenye Mkutano Mkuu, walifikiri ni Mkutano Mkuu kama ule wa Chama Tawala, akifika huko mtu anapata shida, analala siku nne bila kula, anarudi nyumbani yuko hoi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kusema kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Rais, imelenga Watanzania wote, haikumlenga mtu yeyote. Kwa hiyo, nilipokuwa nasikia kwamba wako baadhi ya Viongozi wa Vyama wanalalamika kuwa imewalenga wao, nataka kusema kwamba, imetulenga sisi wote

kwa sababu miongoni mwetu wote wapo ambao vile vile huwa wanakosea wanaingia kwenye viti vya nyuma, wapo vipofu na wapo walevi. Kwa hiyo, haikumlenga mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kama wewe mwenyewe ulivyosema, kwanza ameonyesha uwezo kabisa wa kuongoza na kutawala. Ni Hotuba ambayo imelenga maudhui ya mambo ambayo yanahusu nchi kwa ufasaha na usahihi kabisa. Pia, ni Hotuba ambayo ilikuwa na ushawishi mkubwa, ya kusisimua na kwa kweli ilikuwa inaelekeza. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Kwa ujumla Hotuba imetutolea kabisa uvivu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea mambo mawili tu kwa sababu mengi yameongelewa. Moja, niongee kuhusu kazi ya kubadili mtazamo wa watumishi wa umma ili waweze kuwasaidia Wananchi kujiendeleza, kuwawezesha na kuondoa kero zao na nichukue eneo dogo tu nalo ni Sekta moja ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, jana tumepitisha hapa bajeti ndogo ambayo itasaidia kupunguza ukali wa njaa iliyopo. Sasa, zile Shilingi bilioni 24 ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumeshampa, kama hatutafanya kazi mwaka huu sasa na mwaka unaofuata kuzitafuta ardhini, basi inawezekana kabisa tutakuwa na matatizo makubwa katika miaka ijayo, kwa sababu tutapata wapi?

Mheshimiwa Spika, chakula hakipatikani mahali pengine popote isipokuwa ardhini. Kwa hali hiyo basi, tunahitaji kusimamia kilimo kwa nguvu zetu zote na katika kusimamia kilimo tunayo mifano mingi tu ya kutosha. Mfano, ukiondoka kilomita moja kwenye Manispaa hii ya Dodoma ukielekea upande wa Mashariki karibu kabisa na Jengo la Bunge, tunaweza tukaangalia jinsi watu wanavyopanda mazao. Utasikitika, hakuna hata kanuni moja bora ya kilimo inayofuatwa. Watu wanapanda mazao kwa namna ambayo kwa kweli haizingatii kabisa kanuni za kilimo bora.

Mheshimiwa Spika, tunao Mawaziri wa Kilimo na sisi tupo, tunao Wataalam wa Kilimo, lakini ukiangalia hicho kilimo hapo si kilimo bora. Huo ni mfano tu wa sehemu nyingi katika nchi hii, kwamba hakuna kanuni bora za kilimo zinazofuatwa. Sasa, nafasi ya Wataalam iko wapi hapa? Tutabadilisha namna gani mtazamo wa Watumishi hasa Wataalam wa Kilimo? Hili ndiyo jambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba wenzetu Mawaziri wa Wizara hii ya Kilimo na Chakula wanapopita kwenye maeneo, tuwasikie na wao wakikemea mambo haya, hatuwasikii hata kidogo.

Kwa hiyo, watu wanapanda ovyo hawaweki kingo, ardhi haihifadhiwi, lakini wote tunasema kwamba, kilimo ndiyo uti wa mgongo, tutatoka hapo namna gani, chakula tutakipata wapi hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na watu kupanda mazao yanayostahimili ukame kwenye kanda zinazotakiwa. Unaweza ukajiuliza hivi inakuwaje kama Serikali ikisema kwamba, ukanda huu watu wapande mtama halafu matokeo yake baada ya kila mtu kusema hakuna mtama unaopandwa kwenye eneo hilo.

Sasa tunasimamia namna gani, maana yake ni nini? Tukiendelea na mtindo huu hatutaweza kabisa kuikomboa nchi yetu kutokana na aibu ya kuombaomba chakula, haiwezekani ni lazima tusimamie kilimo kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, baada ya kusema hilo ambalo kwa kweli linauma sana kama hatuwezi kusimamia kilimo na huku tutabaki kuombaomba itakuwa tatizo kubwa sana, ni suala la miundo mbinu. Kwenye ukurasa wa 60 wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba ninukuu sehemu ndogo tu, Mheshimiwa Rais amesema: "Miundo mbinu bora ya kiuchumi ni ya lazima ikiwa tunataka kuvutia wawekezaji na kuwawezesha wananchi kushiriki uchumi wa soko". Akaendelea katika sehemu nyingine akasema uchumi wa soko ndani na nje ya nchi hauwezi kutengemaa bila barabara nzuri zinazowezesha watu, mazao, bidhaa na huduma kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine".

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka niseme juu ya eneo hilo la miundo mbinu. Nataka nizungumzie juu ya barabara moja inayoitwa Barabara Kuu ya Kaskazini *(The Great North Road),* barabara hii ambayo inatoka Cape Town mpaka Cairo au kutoka Cape Town kwenda Cairo ambako karibu nchi nane inapita

barabara hii na barabara hii ambayo miji yake mikuu iko katika barabara hii. Sehemu pekee ambayo barabara hii tumeiacha na tunajenga historia mbaya ni Tanzania peke yake. Ni kati ya Minjingu, Dodoma mpaka Iringa, tumeiacha kabisa, ndiyo sehemu ya vumbi tu, sehemu zingine ni lami. Hapa ndiyo tumekubali Makao Makuu ya nchi yawe Dodoma, hatutaki kuyaunganisha kwa barabara hii Kuu ya Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe historia fupi kwamba, kwa sasa Makao ya Afrika Mashariki yapo Arusha. Viongozi wakitaka kutoka hapa kwenda Arusha wengi wanapitia Morogoro, Chalinze, Mkoa wa Pwani kule, Tanga, Kilimanjaro ndiyo wanakwenda Arusha. Lakini sehemu ambayo ingekuwa fupi sana ni kutoka hapa Dodoma kupitia Mkoa wa Manyara na unafika Arusha kama km 437 huku unapita karibu nadhani mikoa kama 4 ndiyo unafika Arusha. Sasa na sisi tumeamua Dodoma iwe Makao Makuu lakini kuiunganisha na Makao Makuu ya Afrika Mashariki na Miji mingine ambayo ipo kwenye barabara hii ambapo nchi zingine zote zimeunganishwa kwa lami, wala hatuoni umbali huu una athari gani kwa uchumi wa Taifa, muda tunaopoteza kuzunguka pote huko, usafirishaji wa mazao, uchakavu wa magari na mafuta, pamoja na haya wala barabara hii hatuitengenezi kwa kiwango hicho hicho cha changarawe lakini kwa kiwango kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe historia fupi. Nimepitia *Hansard* kwa miaka michache ya nyuma, mwaka 1984/85 Waziri wa Ujenzi, alipoingia hapa ndani alizungumza tu kwamba, uchunguzi na usanifu wa barabara ya Arusha - Dodoma unaendelea. Mwaka 1989/90 Waziri wa Ujenzi, alisema malengo ya kazi hayakufikiwa. Mwaka 1993/94 imetajwa tu barabara kuanzia Namanga, Arusha, Dodoma na Iringa. Mwaka 1994/95 Waziri wa Ujenzi, alilipoti hapa Bungeni kwamba, wahisani wameweka kipaumbele kwenye barabara zingine.

Sasa hivi bajeti huwa tunapangiwa na wahisani. Mwaka 1995/96 Waziri wa Ujenzi, alitoa ripoti kwamba, Serikali imekiri ubovu wa barabara hii ya kutoka Minjingu, Dodoma, Iringa na kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili barabara hiyo ya Minjingu, Dodoma na Iringa itengenezwe. Mwaka 1996/97 Waziri wa Ujenzi, alitoa taarifa Bungeni kwamba, watalaam wetu watafanya mapitio ya upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 1991/92 ili kupata mhisani na kweli barabara hii ilishafanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 1991/92. Mwaka 1997/98 Waziri wa Ujenzi aliripoti kwamba, barabara ya Arusha, Dodoma, Iringa ina umuhimu mkubwa sana katika kuvutia watalii na kutuunganisha na nchi jirani na kwamba Wizara inakusudia kufanya tena mapitio ya upembuzi yakinifu. Mwaka 1998/99 Waziri aliripoti kwamba, tunafanya tu matengenezo kwa ajili ya mvua za *El-Nino*. Matengenezo ya dharura, kuziba mashimo, kalvati na kadhalika. Mwaka 1999/2000 matengenezo maalum yanaendelea. Mwaka 2000/2001 *TANROADS* imeanzishwa, ndiyo ukatolewa mradi maalum na uko ukurasa wa 63 kwenye Hotuba ya Waziri wa Ujenzi wakati ule na kwamba zinatengwa shilingi bilioni 1.8 kwa mwezi.

Lakini barabara hii bado haipo katika mradi wa barabara maalum. Mheshimiwa Rais ametaja kwenye ukurasa wake wa 93 barabara hizi maalum zinazotengezwa sasa. Mwaka 2001/2002 Waziri wa Ujenzi aliripoti kwamba, barabara hii imewekwa kwenye mtandao wa *East African Community* na kwamba, hakuna wahisani. Mwaka 2002/2003 bado tumeambiwa kwamba, iko kwenye mtandao wa *East African Community.* Lakini mwaka 2003/2004 ndicho kipande kidogo hiki cha Minjungu, Babati, Singida, kimefanyiwa *feasibility study* na shilingi milioni 200 zimetolewa, *contract* imesainiwa Mei, 2003. Hicho ni kipande ambacho kinachepuka, ni kipande ambacho kinakwenda Singida lakini ni sehemu ya barabara hii. Sasa juzi Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, wakati anajibu swali hapa, kwa miradi hii ambayo ni miradi maalum inayoendelea, alijibu swali la Mheshimiwa William Shija kwamba, barabara ambazo Mheshimiwa Rais ametaja kwenye ukurasa wa 93, upembuzi yakinifu wa barabara ya Mwanza, Usagara, Chato, Kyamiorwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania utaanza Juni.

Hapo hapo kwenye ukurasa huo wa 93 upembuzi yakinifu wa barabara ya Minjingu, Babati, Singida km 223 imetajwa vile vile chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania. Sasa kama hii nyingine ambayo imetajwa vile vile ambayo imejibiwa na Waziri wa Ujenzi inaanza Juni ambayo najua ipo ukanda wa Magharibi. Je, hii nayo ambayo vile vile inaendelea na upembuzi yakinifu itaanza kujengwa lini, itakuwa Juni nayo hii au vipi, maana zote ni upembuzi yakinifu na zote ziko kwenye utaratibu mmoja?

Mheshimiwa Spika, inaonesha kwamba kwa kweli hatutendi haki tunapotengeneza barabara zetu. Tutaendelea kufanya utafiti wa kuona kwamba tunagawa namna gani miradi yetu katika nchi yetu na tunatoa kipaumbele namna gani. Hatuwezi kuona Makao Makuu hapa hayaunganishwi kwa barabara ya lami ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu tangu mwaka 1991/1992, majibu ni hayo hayo mpaka leo. Basi tunaomba hata hili tawi basi la Minjingu, Babati lianze basi.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Rais wa Nchi yetu. Vile vile kabla sijaendelea, napenda kuwapongeza wale wote waliobahatika kuchaguliwa na kuingia katika Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Rais kwa Hotuba yake nzuri na iliyo makini kwa ujasiri wake mwenyewe. Napenda kumpongeza sana kwamba, Rais amelihutubia Bunge hili kwa muda mrefu takribani saa mbili na dakika kadhaa hivi, lakini hakuweza kugusa hata glasi ya maji. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, Rais huyu ni jasiri na anaipenda nchi yake. Naomba kufanyike uchunguzi duniani kote kwamba, kuna Rais gani aliwahi kuzungumza saa mbili na zaidi ya dakika kumi na tano lakini bila kugusa hata glasi ili tuweze kumweka katika sehemu fulani ya heshima ya pekee. *(Makofi/Kicheko)*

Nimesimama hapa nitazungumza mambo machache tu. La kwanza ni kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kutimiza ahadi mbalimbali zikiwemo ahadi ambazo zilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu wa nchi nzima hasa upande wa barabara. Kule Buchosa watu walikuwa wanaweza kusafiri km 70 kwa saa 10/12, lakini sasa hivi Buchosa watu wanasafiri kwa saa moja na nusu. Kwa hiyo, ni jambo la kuishukuru sana Serikali, kupitia Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Pamoja na kuishukuru Serikali, ninakumbushia tu na ninaomba kwamba, kuna kipande cha barabara cha kutoka Nyakalilo kwenda Lushamba, Rais mwenyewe na Waziri Mkuu, wakati ule wa uchaguzi walitoa ahadi kwamba, barabara hii ni tatizo la muda mrefu, karibu km 33 haijatengenezwa, ni tatizo sugu ambalo Waziri Mkuu pamoja na Rais, waliahidi kwamba, barabara itakuwa imetengenezwa mapema iwezekavyo. Naomba tu kumkumbushia Waziri Mkuu kwamba, barabara hii hadi leo bado haijatengenezwa na ni kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Buchosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze kwenye jambo jingine ambalo ni wimbi la ujambazi. Kweli Buchosa sasa hivi mchana Serikali inatawala, hasa kwenye Visiwa vya Zilagula, Mchangani, Bugombe na Kisiwa kizima cha Maisome, ambapo kuna shughuli nyingi za wavuvi. Kuna wavuvi wengi sana. Sasa mchana Serikali inatawala, usiku majambazi yanatawala moja kwa moja. Hivi ninavyozungumza ni kwamba, siku tano zilizopita kuna watu walinyang'anywa Ziwani *boat engines*, nyavu zao na vifaa mbalimbali vya uvuvi kwa unyang'anyi wa ukatili wa hali ya juu kabisa na waziwazi. Hili limekuwa siyo jambo la mara moja ni jambo la mara kwa mara. Hivi kilio hiki tumpelekee nani? Nchi ni yetu. Hapo tu Buchosa mchana Serikali inatawala usiku majambazi yanatawala halafu baadaye tunasema nchi hii tunaitawala sisi wote. *(Makofi)*

Hivi ninavyozungumza kuna zaidi ya majambazi 21 wamekamatwa. Hata jana nilimwambia Naibu Waziri wa Ulinzi, kuna majambazi 21 yamekamatwa yakiwa na vidhibiti vya nyavu pamoja na *engines.* Hivi tunavyozungumza wamepelekwa pale, ni wananchi wenyewe ndiyo wamekamata wale watu, wameletwa pale Sengerema sasa hivi. Ninaomba jambo hili lishughulikiwe mapema iwezekanavyo. Hili ni tishio hata Mbunge anaweza kushindwa kufanya ziara zake kwenye sehemu hizo. Nina visiwa 11 ndani ya Jimbo la Buchosa, nina Kata mbili zinaishi ziwani kwenye Visiwa vya Maisome, pamoja na Kome. Sasa hili ni tishio kama majambazi yanaanza kutishia raia namna hii hata Mbunge kufanya ziara huko si utakuwa mwoga?

Naomba jambo hili liwe *serious,* ni jambo ambalo tunatakiwa kusaidiwa na Serikali. Nikiangalia katika Hotuba ya Rais, ukurasa wa 26 kama sikosei, anasema nchi hii anatambua kwamba ni nchi yenye wavuvi, wakulima na wafugaji na ni haki ya Serikali yenyewe kulinda raia wake. Ninaomba jambo hili lishughulikiwe mapema. Kuja kusimama hapa mimi mwakilishi wa wananchi na kuzungumza haya mjue

kwamba ni mambo ambayo siyo ya kawaida. Nimejaribu kuripoti sehemu nyingi lakini nimeshindwa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri na Serikali nzima, iangalie kwa umakini suala hili, Buchosa ni tishio kule Ziwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, ninaomba niiambie Serikali kwamba, kuna sehemu ambazo hata wananchi wenyewe wanajua kwamba majambazi yapo yamejiegesha. Kuna sehemu inaitwa Kabiga kwenye Kisiwa cha Maisome na sehemu ya Migongo. Hizi sehemu hawa wavuvi wanaofanyia shughuli pale hawana mitaji, wao ndiyo kazi yao kwenda kuiba na kurudi. Nasikia siku moja maaskari walitumwa kutoka Mwanza kwenda kwenye Kisiwa cha Maisome kufanya upekuzi pale Migongo lakini maaskari wenyewe walirudi mbio baada ya kuambiwa kwamba, kuna silaha kali kuliko za wale majambazi. Sasa kweli Serikali tumefikia hapo?

Mimi nimeona na nimetumwa na wananchi wenyewe sasa ninaomba jambo hili na nalirudia sana kwamba lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo. Nimesimama hapa kutoa hii ripoti na kutoa haya maelezo. Muda mwingi nilishasema kwamba, sitapenda kuzungumza maneno mengi sana kwa sababu wenzangu nao wameshazungumza sana. Ninaomba mawazo haya yachukuliwe kwa umakini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Hotuba ya Rais alitamka maneno yafuatayo: "Demokrasia ni madaraka kwa wananchi". Mheshimiwa Spika, ibara ya 14 (e) ((1) ya Katiba, inaeleza wazi kupeleka madaraka kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuboresha Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha kuwa Halmashauri zinawajibika moja kwa moja kwa wananchi na zinatoa huduma kwa wananchi na pia zinawaendeleza wananchi walioko kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kwenye Katiba kinaonyesha wazi kwamba, Serikali haitekelezi ipasavyo Katiba inavyotakiwa kutekelezwa. Kwa mfano, Sheria Namba 8 ya mwaka 2002 ilikuwa na kifungu namba 6(6) kinachotoa madaraka kwa Halmashauri za Wilaya, kumiliki watumishi wake. Lakini hicho kifungu kikaja kikafutwa na kifungu namba 6 (1) (b) cha Sheria Namba 25 ya mwaka 2002. Kwa hiyo, kunyang’anya madaraka Halmashauri zetu zilizokuwa nayo na kuweka madaraka ya kuajiri, kuadhibu na kumpa madaraka mtu mmoja anayeitwa Mkurugenzi, hii ni kukiuka ibara ya 6 ya Katiba ya Nchi na kuwafanya Watumishi wa Serikali za Mitaa wawajibike Serikali Kuu badala ya kuwajibika kwa Serikali za Mitaa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii kitu imeleta athari kubwa sana kwa sababu dhana ya kupeleka madaraka kwa umma kwa mujibu wa Katiba kupitia Halmashauri za Wilaya imekiukwa. Vile vile Sera ya Chama cha Mapinduzi iliyofafanuliwa mwaka 1995 na mwaka 2000 kuhusu uimarishaji wa Serikali za Mitaa imepuuzwa na sasa inasambaratishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu anatambua hili. Hebu sisi ambao tunamsaidia, askari wa miavuli, tunakutana na kuamua mambo tuyatekeleze kama inavyotakiwa. Kwa kweli inasikitisha sana kuona kwamba, Halmashauri zetu hazitendewi haki. Mfano mmoja hai, baada ya kuanzishwa hii Tume ya Utumishi, Kitengo cha Tume Ajili ambacho ni kitengo muhimu sana kwenye Serikali za Mitaa kimeondolewa watumishi wake wote mpaka sasa hawana kazi. Sijui watapelekwa wapi kama watapewa *redundancy* na hiyo ni hatari kwa maendeleo ya nchi hii.

Ningeshauri kile kifungu ambacho kinazipa mamlaka Halmashauri za Mitaa, kirudishwe mara moja kwa sababu kuondolewa kwa kifungu hicho maana yake ni kuzinyima uwezo Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hili na ibadilishe mara moja. Kwenye Katiba imeandikwa kabisa kutakuwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Sasa hapo ambapo Serikali inaingilia Serikali za Mitaa, kwa kweli haipendezi na inaleta sura mbaya kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wananchi wanapokaa mahali wakasema kwamba sasa huyu kiongozi basi aende atoe na huduma kwingine, tunaomba wasikilizwe. Si vema mtumishi kukaa kituo kimoja miaka ya zaidi ya minane, kilio kinakuja kutoka Mikoa mbalimbali kuwepo Mkoa wa Singida, hebu Serikali inayo mapendekezo, inayo maombi kutoka kwa wananchi, kutoka hata kwenye Chama cha Mapinduzi, kwamba kuna viongozi wamekaa pale wameshazoea wanaanza kuwa kama raia wa eneo hilo kwa hiyo kutofanya kazi yao vizuri. Tunaomba Serikali iangalie hili na isaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la njaa limeshazungumzwa sana bado tunaikumbusha Serikali kwanza, tutafute njia za kuondokana na hii kitu inayoitwa njaa. Njia tunazo ni Serikali kuwawezesha wakulima wake, ni Serikali kuwawezesha wananchi wake wapate vifaa vinavyofaa kwa kilimo ili tuepukane na njaa. Ni aibu kwa kweli kila mwaka tunalia njaa na uwezo tunao wa kuweza kuikomesha njaa.

Naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha mradi mkubwa ambapo kwa kushirikiana na wananchi imekuwa inakwenda vizuri. Kwa mfano, mradi kama wa MMEM, upande wa elimu, mradi wa *TASAF*. Kwa upande wa *TASAF* sasa tunaomba Serikali ipeleke huu mradi kwenye Wilaya zote na ipeleke kabla Serikali ya Awamu ya Tatu haijakabidhi madaraka kwa Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali hapa Bungeni nikaambiwa kwamba, Wilaya ya Iramba mwaka huu wa 2004 iko kwenye huo mpango, sasa sijui kama kweli ipo. Lakini nina imani kwa sababu Serikali yetu inatekeleza ahadi zake, nina imani Iramba mwaka huu itaingia kwenye mpango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali upande wa maji kwa kweli Serikali inajitahidi sana, inawashirikisha wananchi na inasaidia sana. Mimi nimetumwa na wananchi wa Iramba ya Mashariki, niiambie Serikali kwamba, kweli tumepokea kwa mikono miwili ufadhili wa *World Bank* na tutahakikisha tutashirikiana nao, tutahakikisha wananchi wanakuwa bega kwa bega ili tuondokane na tatizo la maji ambalo limekuwa linatusumbua kwa muda mrefu.

Vile vile niipongeze Serikali kwa kuleta mradi wa barabara kwenye barabara, kuna barabara kama nne Iramba ya Mashariki. Wafadhili wameshakuja, ninapongeza sana hatua hiyo ya Serikali. Ila niiombe Serikali kwenye barabara hizo kuna barabara moja inayounganisha Mkoa wa Singida na Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara, ile haikupata fedha kama km 40. Naomba Serikali isaidie juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie mwaka 2003 nilikutana na Mheshimiwa Rais na nikamweleza juu ya wafadhili walioko Iramba ya Mashariki, wanaojenga Hospitali ya Nkungi na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, umeme utakwenda huko mapema iwezekanavyo.

Namshukuru Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alinikutanisha mimi na *management* ya Shirika la Umeme, akiwemo Meneja Mkuu na Msaidizi wake. Mbele yake wakaahidi kwamba, wametenga shilingi milioni 320 kwa kazi hiyo na mimi nilipeleka taarifa hiyo kwa wafadhili, nikawaambia jamani msiwe na wasiwasi sasa endeleeni umeme unakuja, lakini karibu miezi saba imepita hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Sasa kwa kweli sisi hatupendi, tusimtie aibu Rais wetu, Rais wetu anafanya kazi nzuri na inaonekana na hawa watendaji wa chini wamsaidie Rais. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nirudie kumpongeza kwa sababu kila wakati ananipa taarifa. Kwa hiyo, naomba hiyo shughuli jamani tusijitie aibu kwa wafadhili, hiyo shughuli ikamilike mara moja na humu ndani kuna Wajumbe wa Bodi ya Shirika la Umeme sijui wanatusaidia nini?

Wafadhili wameshaleta makontena zaidi ya 20 yako pale lakini hawawezi kuyafungua kwa sababu hakuna umeme kwa hiyo, nawaomba sana, kazi nzuri inayofanywa na Serikali hii, iendelee na ikamilishe haya mambo ambayo imeahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi huwa sipendi kuzunguka, nimezungumza haya, nina imani Serikali itazingatia na itatekeleza yale mapengo yaliyobaki kwa faida ya wananchi wa Tanzania. Nirudie kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake nzuri, ambayo wewe mwenyewe ulisema kuwa ni *authoritative, comprehensive and inspiring.* Ni *speech* ambayo imekuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kutokana na utaratibu wetu, napenda nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kushauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Wabunge wapate nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kwamba tulitegemea kwamba *speech* ikishatolewa namna hii, bila shaka ilivyokuwa nzuri namna hii ni pongezi tu zingeendelea kutolewa nchi nzima kama walivyofanya wananchi. Kwa sababu palikuwa na maneno mengi ambayo ni ya ukweli mtupu. Alipoongelea juu ya mambo yote ya mageuzi ya uchumi wetu, ilikuwa ni ukweli, akielezea nchi inatoka wapi, inakwenda wapi, madeni mengi yamefutwa, ilikuwa ni ukweli mtupu, kila mmoja anajua ukusanyaji wa mapato ulivyokwenda vizuri, nidhamu ya matumizi, huduma mbalimbali zote hizo ni ukweli mtupu ambao unaonekana na halikadhalika mambo kadha wa kadha.

Lakini hata hivyo aliendelea kuzungumzia suala la uzalendo ambalo tumelipongeza sana na kwamba katika suala la uzalendo alipokuwa anaongelea juu ya suala la Wanasiasa au Vyama mbalimbali au Vyama vya Upinzani kukomaa kisiasa na kujali uzalendo zaidi, tulimshangilia na ni jambo jema. Alizungumza juu ya lugha ile ya kumwaga damu kwamba haioneshi uzalendo, ni ukweli mtupu na kwamba tujivunie mafanikio yetu yale tuliyoyapata kutokana na mageuzi yetu, ni ukweli mtupu. Kwa hiyo, hizo zote ni kweli tupu.

Mheshimiwa Spika, nilianza kuogopa baada ya kuona *reaction* hasa kwa upande wa wenzetu wa Upinzani. Nimeyachukua matatu tu. Moja, ikaonekana *speech* inadhalilisha, nyingine ikaonekana hela imekwenda kwenye ndege badala ya chakula, nyingine ikaonekana rushwa haikuzungumziwa.

Sasa walipoongea juu ya rushwa haikuzungumziwa na mimi nimepitia mle, lakini nadhani tumezungumziwa tu ila ikanikumbusha habari ya Mchungaji mmoja aliyekwenda kuhubiri na anafahamika. Alikwenda kuhubiria Waamerika, sasa hivi ni Askofu, anaitwa Askofu Alfa Mohamed, ni Askofu wa *Rift Valley* hapa Manyoni. Alipotoa *speech* ile, ilikuwa kali sana na nzuri, *comprehensive and inspiring.* Halafu alivyotoka nje wale Wazungu wakasema *speech* yako ni nzuri, lakini tungeomba uwe unakuja kutuhubiria kila siku. Wewe ungeendelea kuja hapa kila siku kutuhubiria. Yeye akawajibu, suala la kuhubiri sio hoja, hoja ni ninyi kutubu dhambi.

Sasa rushwa inaongelewa kila siku, lakini watu wangependa kusikia rushwa inazungumzwa tu. Suala ni watu kuacha kupokea rushwa au kutoa rushwa kwa sababu kila siku rushwa inazungumzwa! Sasa wanataka arudie rushwa, sisi walimu tunasema ukirudiarudia inakosa *meaning,* kinakuwa kama ni kitu cha kawaida. Lakini amehubiri sana Rais katika hotuba zake zote. Yule Mchungaji akasema nataka muokoke, sio mimi kuja hapa kila siku. Lakini kanikumbusha habari moja ya Biblia, kama mnavyojua sisi wengine tumezaliwa, mimi baba yangu ni Mchungaji, anasema Yesu aliponya wenye ukoma kumi. Walisema tusaidie mzee na kwa kweli akawaponya wote wakatakasika. Lakini walipoondoka hawakukumbuka hata kuja kushukuru. Alirudi mmoja tu ndiye alikuwa anarukaruka kwamba afadhali nimepona. Lakini wengine wote walifurahi na waliondoka hawakuja kushukuru.

Mimi nilitegemea kwamba wenzetu wanaoleta maneno haya wangepongeza na kushukuru sana *speech* hii kwamba kweli ni nzuri kwa maendeleo ya nchi yetu na yametufunua, yametupa mwanga, ingekuwa ni suala la kupongeza, lakini *inshallah* katika kundi lao kuna angalau mmoja au wawili watashukuru, watapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tena kwamba wamesema wenzangu na ninashukuru Waziri amehitimisha vizuri. Unajua utukufu wa kitu na mamlaka ya kitu yanategemea unatumia kitu gani au unajenga nyumba namna gani. Siku zote baba yangu ambaye nam-*quote* kila siku, anasema unajua matatizo ya *RC,* ukiingia mle unapata picha kwamba Mungu yuko ndani mle, jinsi anavyojengwa. Wewe unategemea Rais anaruka na *Helicopter,* ile hadhi ya nchi yenyewe iko wapi? Maana ile hadhi ya nchi inaonesha na vitu ambavyo nchi inavyo. Barabara ya namna gani, majengo ya namna gani, huduma za namna gani.

Sasa kama mtu anakuja na kandege anasema hivi kandege haka ka nani? Eti hako ni ka Rais anayetoka Tanzania. Aah, nini hii maana yake? Ile ni mamlaka na ile siyo ya mtu ni ya nchi, ni ya heshima ya nchi na uzuri zaidi ni kwamba imenunuliwa na fedha zetu wenyewe. Kwa hiyo, nashukuru hizo zimeshapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba hadithi za Biblia ni nyingi lakini kuna mtu katika *speech* hii tumeifurahia. Nasema kuna mtu ambaye alikuwa ni kipofu akaponywa. Mzee nisaidie, akamsaidia akamponya. Habari tunayo, sasa sijui wengi ni Wakristo na hata Waislam walisoma. Yule mtu akafurahi sana akaanza kutembea anafurahi. Lakini kilichotokea, wabaya wa Yesu wakasema aah, lakini kwani aliyekuponya ni mwenyewe, una hakika? Yule akasema ndio ameniponya. Wakasema aah, lakini pengine anatumia nguvu za benezaburi kama mashetani hivi, mapepo hivi, ni kitu cha kusifu hiki! Anasema ndiyo. Akasema aah, huna haja ya kuendelea kurukaruka na kufurahi bwana. Cha msingi wewe nyamaza tu. Kweli tunajua hajakuponya sawasawa, hivi unaona sawasawa wewe! Akasema ndiyo mimi naona. Sasa walipomghasi sana yule akawajibu hivi, akasema yule bwana awe na pepo wachafu, awe na benezaburi mnayemsema mkuu wa mapepo, awe nani, cha msingi ni kwamba mimi ninaona. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mambo mengine yote yanayozungumzwa, cha msingi ni kwamba hotuba ilikuwa nzuri na imekuja kwa wakati muafaka, ndio la msingi. Suala la kuna nini na nini sisi hiyo wala haituhusu. Tunasema hotuba ni nzuri na imetusaidia sana hasa kwenye Majimbo yetu.

Mimi nasema nimepata silaha ya kufanyia kazi. Mara nyingi nilikuwa naogopa nikiwaambia wananchi msipende kutegemea sana Serikali, halafu unasema sijui watakuja kuninyima kura! Sasa maadam kiranja mkuu wa nchi amesema huwezi kuwakomboa watu kwa kuwapa fedha! Mheshimiwa Edson Halinga alikuwa anachekesha sana, alipita kwenye Jimbo lake ndio anakwenda kwangu. Sasa siku moja akakuta watu wanakunywa pombe, wakasema: “Bwana, Mbunge amepita hapa hata pombe hajatuachia.” Lakini Halinga akasema: “Mbunge mliyekuwanaye miaka kumi ambaye wanajua Mheshimiwa Khatib anamfahamu alikuwa rafiki yake ambaye amechukua pale, alikuwa akipita pale anaacha pipa la pombe, lakini kilichotokea barabara haikulimwa kwenda kwao.”

Sasa mimi nilipokwenda pale nilisema tunang’oa miti, tunang’oa visiki, tunalima barabara na barabara imepatikana. Akauliza, nani anayefaa? Aliyewapa pombe lakini hamkuwa na magari ya kwenda kwenu? Lakini huyu amewalazimisha kuchimba hivi visiki na barabara inakwenda kwenu. Nani anafaa? Wakasema, lakini kweli sasa hivi hata bei ya mpunga imepanda, maana magari yanakuja mengi, anafaa kweli.

Mheshimiwa Spika, alichosema Rais ni kwamba usipende kuwadekeza watu, ndio maana yake. Kwamba Watanzania wabadilike, Watanzania wajiingize katika shughuli za kuzalisha mali na kwamba kuwadanganya watu kwamba sisi tukiingia tutafanya hiki na hiki ni kuwadanganya na huo ni ujumbe mkubwa ambao tungeweza kuchangia kwamba watu wetu sasa wabadilike. Watu wetu wajue kwamba Marehemu Mwalimu Nyerere alishatamka kwamba ni lazima mtu ajitegemee katika ujamaa na kujitegemea. Ni lazima watu wajitegemee.

Sasa unafika mahali watu wanataka kutupa mawe tu kwa wenzao lakini wao wenyewe wanakuwa ni Mafarisayo, wanatwisha wenzao mizigo ambayo wao wenyewe hawawezi kupewa wakaibeba kwa vidole vyao wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nilikuwa na jambo lingine ambalo ni vizuri niliseme hapa. Mimi sio mwanamichezo sana, nacheza *indoor games* zinaitwa. Hii michezo ya kukimbia sana, hiyo mimi

sikimbii sana. Lakini napenda sana kuangalia *Television.* Kama kuna mipira yoyote hata kama ni saa nane ya usiku mimi nitaangalia kwa sababu napenda sana kuangalia michezo kama mpira. Mimi nashangaa sana na nimekuwa nikimwuliza Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, nasema hivi hii hali ya michezo nchini mwetu, hivi Ndolanga ni nani? Unajua mimi sijaelewa! Huyu Ndolanga ni *animal* gani ambaye nchi nzima imenyamaza kimya ina-*paralyze* akitamkwa Ndolanga?! Nikamwuliza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya hivi Ndolanga ni nani? *(Kicheko)*

Bado naendelea kuuliza kwa sababu Ndolanga aliitwa hapa na Kamati ya Dada yangu Sophia Simba, wakambana kabisa kwenye kona kwamba sisi kama Bunge tunaingilia *issue* hii. Hatuwezi kuendelea kuonekana Tanzania hatuwezi kucheza mpira. Nchi kubwa na yenye hadhi namna hii ina wachezaji wazuri, wewe unaharibu! Lakini wakamwita wakazungumza naye, watu wa *FAT* akaongea nao, mimi nikamwambia weka kibano, kama ni kujiuzulu, ajiuzulu hapo hapo leo msimuache tu a-*cool down* atawaza upya.

Sijui walivyombana wenzangu, baadaye akasema kweli tumeelewa, nchi hii tunaona mchezo hauendi sawasawa, wananchi wananung'unika, watu hawapendi haya, tumeelewa kabisa. Halafu tupeni muda tukawaze, wakamuachia. *(Kicheko)*

Amekwenda amekaa amesema dah, niachie hapa! Hapana. Amebana. Sasa wenzangu nikawaambia lakini nyie mlikosea. Mimi kwenye Kamati yangu tunaamua pale pale. Ninyi mmeshindwa kuamua? Nikaona nguo zinawacheza ni rafiki zangu, dada yangu Mheshimiwa Sophia Simba, kwa nini hamkumbana pale pale atamke pale pale na muite na vyombo vya habari mtangaze? Sasa amekuwa ni mtu ambaye hashikiki.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo Serikali itusaidie sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Labda nianze kwanza kwa kumtakia pole Mheshimiwa Rais na vile vile kumtakia apone haraka, Mwenyezi Mungu ampe nguvu zote anazohitaji katika kukabilina na maumivu anayoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ningeweza kuijadili kwa sura mbili, moja ni sura ya siasa na moja ni sura ya Mbunge. Naomba nichukue *line* ya kuwa Mbunge na mimi nadhani ndio nafasi ya kujadili hotuba ya Rais ndani ya Bunge kwa sababu tunapata nafasi ya kuijaili kama Wabunge. Kama Wabunge, ningependa kwanza kuzungumzia kipengele cha Serikali za Mitaa kama ilivyo kwenye Kitabu cha Tisa na hasa mahali pale ambapo Rais anazungumzia Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pale Karatu mwaka 2000 tulipogombea tuliuza sera na kwa bahati nzuri kwa dhana ya Serikali za Mitaa, wananchi wakatuchagua kwa wingi kitu ambacho wenzangu wa CCM wanaita kwa kishindo na Karatu tulishinda kwa kishindo. Sasa baada ya ushindi tuliweka ahadi kwamba kazi yetu ya kwanza ni kusimamia na kutekeleza, kwa sababu Serikali za Mitaa iliyoshinda kama sio ya Chama Tawala kazi yake ya kwanza ni kuhakikisha inatekeleza sera ya Chama kilichoshinda Kitaifa na ninairudia tena hii sijui mara ya ngapi ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, ndiyo ahadi ya kwanza. Kila kilichoko na kinachopitishwa na Chama Tawala sisi tunakisimamia na kukitekeleza maradufu zaidi na ndiyo kazi tunayoifanya Karatu.

Mheshimiwa Spika, ahadi yetu ya pili ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati maalum ya kutekeleza yale tuliyoyaahidi kwa ajili ya watu wetu yaani vipaumbele ambavyo sio lazima viwe vya Kitaifa, lakini kuna vipaumbele vinavyohitajika kwa ajili ya mazingira maalum ya Karatu. Kila Wilaya ina mazingira yake maalum.

Ya tatu, tuliahidi kwamba tutaondoa unyanyasaji wa aina zote na hii naisema makusudi kwa sababu kabla ya mwaka 2000 Karatu siasa ilileta uadui na uhasama. Nilishaeleza kwamba ukiingia kwenye gari ya Mbunge unaonekana adui na ulikuwa unajadiliwa kwenye Kamati ya Siasa ya Chama Tawala wakati ule na walimu walihamishwa na watu walipewa adhabu. Kwa hiyo tuliahidi hilo.

La nne, tuliahidi tutapiga vita ubadhirifu wa aina zote. Sasa naomba nifafanue kidogo tu kwa sababu mimi kama Mbunge hotuba sina tatizo nayo kwa sababu yaliyotekelezwa ni yale tuliyokubaliana hapa Bungeni, tumeyapitisha sisi hapa Bungeni, kwa hiyo, sina tatizo ukiondoa ile sura ya kisiasa. Kwa sababu dhana iliyoko katika ibara ya 146 ni dhana pana na ni kubwa sana, ningependa niseme kwamba kwanza tumesimamia vizuri yale ambayo yalitokana na sera ya Chama Tawala na ningeomba kwamba ni vizuri Chama Tawala pia kikawa kinatambua na ninakumbuka kwa hotuba ya kwanza ya Rais alisema tushindanishe Majimbo yanayoongozwa na Wapinzani na yale ya CCM.

Nadhani sasa Serikali ingefanya tathmini ya kina kabisa, ya ukweli na ya uwazi kushindanisha na kuona matokeo ya utekelezaji wa kazi zilizofanyika katika Majimbo ya Upinzani na yale yanayoongozwa na CCM. Mimi nadhani hili linahitajika sana ili tuweze kusema dhana yetu ya demokrasia inakwenda vizuri na kama kuna kasoro na matatizo tujue yako wapi kwa sababu mimi ninafahamu kwamba matatizo mengine yaliyoko yanasababishwa na wale walioko kwenye viti. Tathmini ingejionesha kwa kina na hapo tungesema kwamba hotuba ya Rais imekwenda pia kwa hatua kwa kulinda demokrasia badala ya kusema tu kwamba kuna udhaifu katika upinzani. Udhaifu tunauona wapi?

Mimi nafikiri Rais amesema neno hilo, anazungumzia tu siasa kwenye vyama, lakini kuna siasa inayoshika vile vile maeneo na hilo ningependa liangaliwe kwa makini na lifanyiwe kazi kwa makini sana. Lakini la pili, ni ile mikakati yetu.

Naomba kama Rais alivyojisifu hapa na mimi naomba Karatu tujisifu kwa sababu mmetuambia kwamba kwa kile ulichofanya ni vyema ujisifu. Naomba Karatu tujisifu kwamba tumetekeleza asilimia 80 ya Vijiji vyetu sasa vina maji. Tulipotoka huko nyuma tulikuwa hatuna maji na tuliambiwa Karatu tangu iumbwe na Mwenyezi Mungu haina maji. Lakini tumepata asilimia 80, hatukufanya miujiza. Tulishirikisha wananchi na ninaomba niishukuru sana Wizara ya Maji kwa kutusaidia. *(Makofi)*

Namshukuru Mheshimiwa Waziri tangu Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu mpaka Mheshimiwa Edward Lowassa, tena kwa dhati kabisa, nawashukuru sana kwa sababu Serikali ilitusaidia hata kama ni kiasi kidogo sana, imeongezea kwa wafadhili wetu na wafadhili walipata moyo kwamba miradi hiyo inaungwa mkono na Serikali. Ninasikitika kidogo kwamba kwa upande mwingine Serikali hiyo hiyo iliyotusaidia ikatuweka pembeni, tunapowaomba kuja kuzindua miradi wanakataa, hawaji. Sasa hiyo ni dhana inayoonesha bado wananchi wanajenga picha kwamba kumbe Serikali inakataa kwenda kuangalia maendeleo kwenye Vijiji. Hii ni dhana inayojengeka miongoni mwa watu, ni lazima ifutwe. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Sasa wanaosema sio kweli mimi ndio niko Karatu. Sasa wao wa Kigoma wakisema Karatu sio kweli, maana yake hujui hata unachoongea. Sasa ni vizuri Wabunge wawe makini.

Mimi sina tatizo kabisa na Waziri wangu na ninajua tatizo labda sio la kwake kwa sababu ametuandikia hata barua ya kutupongeza. Kwa hiyo, tatizo haliko kwa Waziri. Sasa hili linahitaji liangaliwe liko wapi, ndio baadhi ya mambo yanayofanya demokrasia katika nchi yetu ionekane ina kasoro na ndio inayoonekana iwe dhaifu. Kwa hiyo, tusiseme tu ni dhaifu, kuna mazingira yanayofanya demokrasia kuwa dhaifu na mimi ningeomba badala ya kulaumu tu, tuangalie na tufanye tathmini ya kina.

Vijiji vyangu karibu vyote na kama nilivyosema tuna Vijiji asilimia 80, sasa hivi tuna kazi inaendelea kule Lusitete, tena kwa ndugu zake Mheshimiwa Edward Lowassa, wale Wamasai na ninawapongeza kwa sababu Wamasai sio kawaida yao kwenda kuchimba na wakaniambia, nani atachimba kwanza? Nikawaambia mtachimba wenyewe. Wakasema sawa bwana na wamechimba na mradi unaendelea. Lakini kazi hiyo inapofanyika na wananchi wanapojitolea, inasikitisha unapoona vile vile viongozi wa Serikali wanapofika na kuanza kugawa wale wananchi.

Mheshimiwa Waziri Mizengo Peter Pinda, nafikiri na Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, bahati mbaya hawapo wote wawili, wanajua malalamiko yaliyotokea sasa hivi. Anapofika kiongozi wa Serikali, ndiye anayesema kwamba mwananchi asilipe. Sisi tumefanya kazi ya kuhamasisha wananchi, wanalipa

shilingi 5/= kwa ndoo. Lakini anafika kiongozi mkubwa wa Serikali anasema wananchi kwa nini mnalipa? Iko kwenye maandishi.

Mimi nafikiri dhana nzima anayozungumzia Rais pia hapa haipo na mimi naungana naye kwamba viongozi wa Serikali sasa wakati umefika wabadilishe mawazo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapofika mahali wananchi wanafanya kitu, kiongozi unatakiwa kusaidia. Lakini kiongozi unapofika mahali unaanza kugawa, tutakuelewa vipi? Nimempa Waziri, nangojea na kama kweli maana hii anayozungumzia Rais mnafikiri ni ya kweli, nadhani Serikali itachukua hatua na tunawapima kwa kipimo hicho na wakati utatokea tena tutakapokuja kuwasema, kwa sababu leo sitaki kuwasema zaidi ya hiyo.

Lakini nataka nitumie nafasi hii nipongeze sana wananchi wote wa Vijiji vyote vya Karatu tangu Kaviwasu, Kata ya Mbulumbulu, Kata ya Rotia, Karatu Mjini, Mangola, Eyasi ambao wako sasa hivi wanatekeleza miradi. Kwa sasa tunapoongea tuna miradi ya maji inaendelea katika Vijiji visivyopungua kumi na ni miradi mikubwa na mingine ni zaidi ya bilioni.

Ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo sasa akikumbuka maombi yetu ya nyuma, wiki ya maji kwa kuwa inakuja, hatatuweka nje ya ratiba yake ya wiki ya maji. Sasa natoa ombi hadharani, mwanzoni ilikuwa kwenye maandishi tu kati yangu na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kulisema hilo, nadhani niseme vile vile kwamba yako mengi ambayo yamefanyika na ziko ahadi nyingi zimetekelezwa, ahadi ya unyanyasaji tumeitekeleza, tumeondoa unyanyasaji, tumeondoa dhana, lakini nadhani kwa upande wa Serikali na kwa upande wa Chama Tawala mpaka Wilayani, wala mimi sifiki mahali nikasema kwamba Chama Tawala tangu juu, mimi siamini kama Rais Benjamin Mkapa anaagiza kwamba watu wahujumu wale wa chini.

Nina hakika kuna viongozi ambao wanafanya kwa matakwa yao tofauti na matakwa ya Chama. Lakini kama Serikali haisimamii toka juu, kama unapeleka taarifa Serikali Kuu na Serikali Kuu haichukui hatua, sisi tunapata imani kwamba ni kweli Serikali Kuu nayo pia inaungana nao. Kwa sababu kama haiungani nao, Serikali Kuu ina uwezo, ina vyombo, ina mamlaka ya kuingilia na kuchukua hatua ili wananchi hawa wasikwamishwe. Hatuwezi kufanya maendeleo kama dhana ya kugawa watu kwenye maendeleo itaendelea.

Mheshimiwa Spika, labda niache hilo kwa muda huu, wahusika watakuwa wamesikia. Lakini niseme mambo mengine madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba wakati mwingine tunapozungumza, sio suala la kusema kwamba mifuko ijazwe, tunapopiga kelele sisi, kwanza ijulikane ni haki yetu ya Kikatiba kutoa upande wa pili wa shilingi. Kwa hiyo, wenzetu wakubali wanapokuwa *criticized,* wapokee mawazo. Kataa mawazo lakini toa taarifa. Ni haki yetu Wabunge wa Upinzani tunaposimama Bungeni kutafuta tafsiri yoyote ya jambo lolote na Katiba Kifungu cha 63(2) kinaturuhusu tumwulize Waziri juu ya jambo lolote lililoko chini yake.

Kwa hiyo, hapa tunatimiza wajibu na wajibu huu ni wa Wabunge wote, lakini sisi tunautekeleza kwa umakini zaidi. Kwa hiyo, tunapohoji ni lazima tuhoji. *(Makofi)*

Kwa mfano, tuna taarifa na Waziri anihakikishie kama ni kweli au sio kweli. Tuna taarifa kwamba kwa mfano, *Amax Resources* mwaka 1997 walipewa leseni ya kuchimba madini kule Nzega. Tarehe 1 Septemba, 1998 wakauza ile leseni kabla hawajaanza hata kuchimba. Sasa hawa ni watu waliokuja, dhahabu wameikuta pale chini iko kwenye ardhi yetu, wameuza ile leseni. Taarifa niliyonayo mimi wameuza kwa milioni *US$*213, zaidi ya bilioni 200. Karatasi tu! Hivi imetuzidi nini?

Tunapopiga kelele kwa Mheshimiwa Rais sio kwamba sisi hatuoni mambo. Tunaona lakini tunasema hivi, huyu mtu kama anaweza kuuza leseni, kwa nini tuhitaji *middleman* wa kwenda kuuza leseni? Kwa nini tusiuze hii milioni 280 tukaipata sisi kabla hata ardhi yetu haijachimbwa?

Lakini watu hao hao 1996 Kampuni nyingine inayoitwa *Sutton* walipata pia leseni na wakaiuza mwaka mmoja baadaye kwa *Barick Gold Corporation* kwa bilioni 280. Nataka Waziri atuambie kama ni kweli karatasi tu inaweza kuuzwa, ardhi ya Tanzania iko pale, ardhi hii ni yetu, wataalam tunao wanaoweza kutambua, ni kitu gani kinatufanya sisi hizi bilioni tuzipoteze mtu mwingine aje tu azibebe hivi hivi na sisi tunaendelea? Ndio maana tunasema hizi fedha kama zingepatikana kwetu, hata hii njaa hatungehitaji kwenda kuomba nje. Ndio kelele zetu na hizi hakuna atakayekataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka Waziri atupe taarifa baadaye kama sio sasa kwa wakati wa Bajeti inayohusika. Lakini tunapopiga kelele kwa Rais kwa sababu ya mambo haya ambayo tunasema kwamba usimamizi wakati mwingine ndio tatizo. Utekelezaji wa mambo anayosema ndio tatizo. Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa ameandika hotuba nzuri sana na vitu vingine vikatekelezwa, lakini vile ambavyo vinatakiwa kurudi ndani havisimamii na sisi ni kazi yetu kupiga kelele, ndio watetezi wa wananchi na Wabunge wote ni kazi yetu, sio Wabunge wa Upinzani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nimalizie na hayo, sipendi kengele ipige tena, lakini narudia kusema kwamba nawapongeza wananchi wa Karatu kwa dhati kabisa kwa jinsi walivyotekeleza yale tuliyoyaahidi, shule tumezijenga. Mara nyingi kuna watu wanafika kule Karatu wanasema Karatu haina maendeleo. Nataka kuwaambia, Vijiji vyangu asilimia 80 vina maji. Tulikuta kuna shule moja tu Karatu, sasa hivi tunapoongea Januari hii tumefungua tatu, mwaka 2003 zilifunguliwa mbili, ziko tano. Ahadi yetu ni tisa zitafunguliwa mwaka 2005. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nami kidogo nichangie kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kama kawaida hata na mimi nilikuwa najua kwamba hotuba yake itakuwa inavutia.

Mheshimiwa Spika, kuna machache ambayo nilitaka nichangie ambayo inaonekana labda tungetaka yawe humu kwenye hotuba lakini sasa hayakuwemo. Vile vile nitachukua nafasi hii kupongeza Waheshimiwa wenye Wizara hizi ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa na Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli. Kwa ujumla vitu walivyofanya ni *tangible,* vinaonekana. Barabara zinaonekana na kwa kweli maji kila eneo wanazungumza kwamba Waziri anajitahidi.

Kwa hiyo, suala la kusema kwamba watu hawaoni wamekaa nyuma ya kiti sio kweli, mbona nimeona hayo? Yanayoonekana yanaonekana na yasiyoonekana tutayasema hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza sana katika mambo mawili. Jambo la kwanza nitakalojielekeza nalo ni kwamba bado mimi nalia na wakulima wangu ambao ndio watu wa huko chini. Tukiangalia hapa katika ukurasa wa 67 wa hotuba ya Rais, inasema: "Ni aibu kubwa kwamba mimi niko mstari wa mbele kudai nchi tajiri zifungue milango kwa bidhaa zetu wakati ambapo bado Tanzania haina bidhaa za kutosha za kuuza." Hii ninanukuu.

Kama hatuwezi kwenda kwenye kulima, kama hatuwezi kuwasaidia wakulima, kwani kwa kweli maendeleo tunayosema yatagawa nchi hii. Yataigawa vipi? Kutakuwa na matajiri sana na kutakuwa na maskini sana. Hilo ndilo jawabu litakalotokea.

Kwa hiyo, nimekuwa nikilia hapa, nikilalamika kuhusu hawa wakulima kwamba bila ruzuku kazi ya kulima ni ngumu. Serikali kwa makusudi leo hii tumetoa shilingi bilioni 24 tunapeleka kwa ajili ya chakula cha njaa, je, hizo bilioni tunazokusanya tunakusanya bilioni 120 za kodi kila mwezi, je, tungekuwa tunatoa hata bilioni mbili, mbili tu, kwenye Mikoa tunasema hizi ni kwa ajili ya wakulima ili waweze kuzalisha na tuweze kuuza, leo tungekuwa wapi?

Kwa kweli tusingekuwa na jambo au tunalosema ni njaa Tanzania, ni aibu Tanzania kusikia kwamba eti kuna njaa. Kwa hiyo, haya mambo au mapungufu haya ambayo tumeyaona ndiyo tunayoyasema hapa, kama hatuwezi kwenda kwa wakulima, kama hatuwezi kurudisha ile njia ya Maofisa Ugani ili wawe karibu na wakulima ili sasa tulime, tuzalishe, tuuze kwa kweli bado tutasema kutwa,

tunaendelea kwa barabara, tutaendelea kwa mambo mengi mbalimbali, lakini bado ule uchumi wa chini, wale watu wa chini ni vigumu kuonyesha sasa kwamba tumepata uchumi wa kutosha kwani hautakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu jambo lingine hapa linalohusu mambo ya ruzuku, ukurasa wa 71, nanukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais: "Tunaziomba sana nchi tajiri wasiishie kwenye kukiri kwamba ruzuku zao zinatuumiza, bali wachukue hatua mapema ya kuzirekebisha na hatimaye kuzifuta."

Mheshimiwa Spika, hawawezi wakafuta hizo ruzuku, wao wanapalilia, wanalea wakulima wao. Sasa unamwambia usimpe mtoto chakula, haiwezekani. Kama wewe nyumbani kwako watoto hawavai viatu, mimi watoto wangu ninawavisha viatu. Huwezi kusema aah, ili tuwe sawa basi usinunue viatu kwa watoto wako ili tuwe sawa, haiwezekani. Ni sisi kujitahidi kununua viatu kwa watoto wetu. Ni sisi kujitahidi kutoa ruzuku kwa wakulima wetu. Siyo kuwaambia wale wafute ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu hii hoja niliipeleka Bangladesh kwa kuwa ulinipeleka Bangladesh. Niliongelea kuhusu nchi za matajiri, nchi tajiri na nchi maskini hazipewi ruzuku. Mimi alilonijibu yule Mkuu wa *World Trade Organization (WTO)* alisema, sasa kama mnataka hivyo basi mkafungue soko lenu kubwa la Afrika badala ya kutegemea hili la dunia. Nami nikasema haiwezekani. Hakuweza kunijibu kwamba watafuta ruzuku. Kwa hiyo, sisi siyo kuwaambia wale wafute ruzuku, hiki ni kitu ambacho hakiwezekani. Ni sisi kuanza kuwapa wakulima wetu ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ningekuwa na mimi najua mabilioni yanayokusanywa hapo Dar es Salaam kwa ajili ya kuongezea bei vitu, bilioni nyingi tu 120 kwa mwezi. Kweli kabisa ningesema kila Mkoa utapata bilioni angalau moja moja kwa Mikoa 25. Ni Mikoa 20 ambayo inalima zaidi, angalau hata Mikoa 10, nichukue Mikoa 10 tu niseme hii inazalisha sana kwa hiyo, nisaidie hii kwanza. Halafu zingine zifanye hizo kazi nyingine ambazo Serikali inafanya. Tutachangamka na tutaendelea na hakuna njaa tena.

Naomba sana, ningepaswa kumpongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, lakini nimeshindwa. Nimepongeza hawa wawili kwanza, kwani katika kupiga makelele tumeletewa bilioni 42, tena Wazungu wametuletea, sisi hatuna ni maskini, *fine.* Sasa wametuletea bilioni 42 haya saidieni wakulima wa Kahawa wanaolialia kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mwaka sasa toka hizo fedha zimefika na hakuna mkulima yeyote anayefahamu chochote. Mimi Thomas Ngawaiya, nafahamu hapa Bungeni tu kwamba kuna bilioni 42. Hakuna hata ile harufu ya kusikia joto la kusikia kwamba kuna bilioni 42 ambazo zililetwa na Wazungu wa *EU* kwa ajili ya kusaidia wakulima wa Kahawa hakuna. Juzi hapa Mheshimiwa Waziri ametujibu, Waziri wa Fedha, amesema fedha ziko kwa Mheshimiwa Charles Keenja.

Mheshimiwa Keenja, atakuambia fedha zinakaa *Treasury* hazikai kwangu. Sasa hizo fedha zinakaa wapi? Ziko wapi? Wakulima wanazitaka zitumike, kama hamtaki kuwapa kwa ajili ya kitochi basi na kama mliahidi barabara zitengenezwe basi zionekane, kama mliahidi pembejeo za Kahawa basi zipelekwe huko. Kama ni miti ya Kahawa basi wapatiwe miche ya Kahawa, mwaka mzima tumekaa na fedha za watu wa *EU* wanaweza wakaamua kuzirudisha.

Maana hazijamfikia yule mlengwa ambaye ni mkulima. Kwa hiyo, mimi katika Bunge hili kwa kweli na nashukuru Mheshimiwa Spika, amenipanga kwenye Kamati ya Kilimo, nasema mimi nitakufa na kilimo na wakulima wangu mpaka nitakapomaliza Bunge hili na naomba Waheshimiwa wanaohusika wanisaidie. Mimi naamini bila kilimo bado hatuwezi kuendeleza vizuri nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo naona kwa nini hayakuzungumziwa ni mambo madogo madogo. Siyo madogo, kuna watu wanaokufa njaa. Nilikuwa nategemea Mheshimiwa Rais katika hotuba yake pamoja na uzuri aliouzungumzia kwamba angesema sasa Tanzania tuanze kilimo cha kufa na kupona kama alivyosema Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere wakati fulani, mpaka tukalima mwaka huo tukakosa hata mahali pa kuweka vyakula. Tulikuwa tunataraji kwamba Mheshimiwa Rais angesema kwamba sasa mwaka huu tufanye kama tulivyofanya mwaka fulani ulikuwa mwaka 1971 au 1972, kilimo cha kufa na kupona. Tungezalisha halafu tungeziba pengo hili ambalo tayari tunaanza kuombaomba vyakula. Ni aibu sana kwa Tanzania kuomba vyakula.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba kabisa, ni methali nyingi sana Mheshimiwa Rais alizozitoa, ni kweli kabisa tulikuwa tunajiona kama tuna-*fit in* Wapinzani. Lakini nataka niseme hapa kwa Viongozi wenzangu na wengine wakubwa wangu, kuna Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, nasema kwamba Serikali ndiyo baba, hakuna ubishi na hilo. *(Makofi)*

Ina watoto, wakati tumepeleka Tume ya Marehemu Jaji Francis Nyalali, ni asilimia 20 tu waliokubali Upinzani Tanzania. Lakini Marehemu Mwalimu Nyerere, Mungu amuweke mahali pema, akasema hapana! Kuna haja ya hawa Wapinzani wawepo, ili waweze kutuchangamsha. *(Makofi)*

Sasa sijui Serikali hii ya Awamu ya Tatu inatulinda namna gani sisi wapinzani na inatusaidia namna gani ikijua kwamba sisi ni watoto wa Serikali hii hii. Kwa sababu tumezaliwa tu, walijua tuko asilimia 20, wanafanyaje sasa ili tuongezeke. Je, tubaki asilimia 20 ile ile? Mnatusaidia namna gani sisi ili tuongezeke, maana mtasema dhaifu. Mnajua kwamba tulikuwa asilimia 20. Sasa hatufikii 20 mnatusaidiaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, badala yake wanatuchukulia Madiwani, wanatuchukulia viongozi ambao tunawaamini, ndugu zetu, kama Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, hatunao tena. Sasa huo udhaifu utaachaje kuwepo katika misingi ya kuanza, kitu unaanza vizuri, unaanza kupanda mimea yako vizuri, unaiwekea maji, je, Serikali hii ya Awamu ya Tatu inatuwekea maji sisi Wapinzani ili tuweze kuwa sasa pamoja, mfano kama huku kuna 20 na huku kuwe na 20. Tunaanza kuvuta kamba, haya anza kuvuta, *tag of war.* Tunavuta, sasa anaeelemewa tunajua kabisa labda hakula chakula jana. Lakini sasa mko wawili, huku mko 100 unategemea nini? Halafu utasema nyie wadhaifu sana ninyi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, anayeweza kuamua kwamba sasa tuangalie kuwa hali nzuri kwa Wapinzani ni Serikali hii hii. Imeamua juzi na mimi ninasema napongeza kwamba sasa kuwe na asilimia 30 ya akinamama Bungeni, mimi napongeza hilo. *(Makofi)*

Sasa Serikali hii ndiyo inayoweza kuamua. Serikali *every President* anaweza akaja na kusema au akaamka tu asubuhi na kusema sitaki kuona Upinzani Tanzania na ikawa hivyo. *Yes!* Kwa sababu Upinzani tuliokuwa nao Tanzania siyo ule wa akina Savimbi wa porini. Upinzani wetu ni wa mezani na kujibishana kwa hoja. Sasa tutakuwa tunapeana vikonzi, tunapigwa vikonzi tu, sasa hatuwezi kwenda.

Hebu naomba Waheshimiwa Wabunge kupitia kwa Mheshimiwa Spika, kwamba hebu tuangalie huu Upinzani tunausaidiaje ili sasa ukishaanza kuwa na nguvu tayari mnaweza mkasema aah, basi tuwaachie sasa, wameshaanza kuwa na nguvu. Lakini sasa siyo kila siku vikonzi, mnatupiga vikonzi kila siku kwa sababu ya uchache wetu, kama leo mnatuchagulia mtu.... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nasema... nashukuru Mheshimiwa Spika, kengele inalia. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Ahsante Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na wewe Mheshimiwa Spika vile vile nakupongeza unafanya kazi ngumu ya kukaa kwa muda mrefu bila kushtuka wala kunywa maji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa hotuba yake safi kama ulivyoipa *title* ya *comprehensive and inspiring.* Ni zaidi ya hivyo, lakini sifikiri kama kuna lafudhi zaidi ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa wazi kueleza kwamba kipindi chake kilichobaki atahakikisha kwamba ndege iliyoko uwanjani inaruka *by targeting the transformation of economy which is a positive step, Honourable Speaker Sir.*

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema ukifeli kupanga, basi ujue unapanga kufeli. Dunia ya leo unapokuwa unafanya mema hakuna anayekumbuka, lakini ukifanya baya hakuna anayesahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukijifanya kondoo utaliwa na simba. Mheshimiwa Rais Mkapa, amenifurahisha sana alivyotumia neno *Inshallah* katika hotuba yake. *Inshallah* maana yake Mwenyezi Mungu akipenda na kwa nini asipende na nia zetu safi Watanzania? *(Makofi)*

Tunapaswa kubadili *gear, gear* ya kwanza najua ina gharama zaidi inakula petroli zaidi. Ndiyo maana tuweke *gear* ya nne iwe gharama kidogo twende mbele. *Full speed ahead,* hakuna Serikali iletayo *Alladin lamp* kwamba ukiisugua tu unasema nataka milioni moja, unapata milioni moja, hakuna.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Anatory Choya, alitoa *quotation* ya Kiingereza. Naomba ruksa yako niitoe ya Kijapani leo. Wajapan wanasema *bimbo hima nash.* Maskini hawana *time* ya kupumzika. Huwezi ukalala ukiwa umekaa tu au ukaamka ukaenda mbio tu ghafla, labda uwe mtoto wa ng'ombe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, usiulize Serikali yako imekufanyia nini? Jiulize wewe umeifanyia nini Serikali yako? Hii ni Serikai ya wananchi iliyofanywa na wananchi kwa ajili ya wananchi.

Kuhusu amani na utulivu, shukrani zote zimwendee Mwenyezi Mungu kwa kutupa amani na utulivu nchini kwetu. Mwenyezi Mungu anasema: *"Atiullah wa Rasul wa ulili amri minkuni"* yaani utii, mtii Mwenyezi Mungu, umtii Mtume na wenye amri juu yako na viongozi wetu tunawatii na inabidi tuwatii. Uongozi mzuri ndiyo ulioleta amani nchini. Lazima tushukuru na asiyemshukuru binadamu, amshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu haiondoi neema mpaka sisi wenyewe tuipige teke na Mwenyezi Mungu atuepushe na jambo hilo. Mimi leo naomba samahani nitatoa mawaidha leo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa sana na namwambia maneno haya yafuatayo: *"Stone and sticks are thrown only at fruit bearing trees."* Mawe na magongo ndiyo inaruhusiwa miti ambayo inazaa matunda. *The pioneers are always kicked, Hounarable Speaker Sir, look at Jesus Christ. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema kelele za chura hazimzuii simba kunywa maji. *Why murder a man who is about to commit suicide?* Tupunguze starehe, tutapata mtaji japokuwa Waingereza wanao msemo wanasema kwamba *spend and God will send.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TRA* kwa kazi ngumu katika mazingira magumu. Kuna habari kwamba baadhi ya viongozi wa *TRA* wamefika mpaka wameuawa. Nawapongeza sana na nampongeza Rais vile vile kwa kutaja kwa uwazi kabisa katika hotuba yake kwamba unyanyapaa uwe mwiko.

Mheshimiwa Spika, tuoe na wanawake waolewe. Tuepukane na matatizo mengi na wala tusiogope umaskini, tukaacha kuoa na kuolewa, bora shida za duniani kuliko za *Akhera.* Nilifurahi Mheshimiwa Rais alipotujulisha wanafunzi waliofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa darasa la saba, Marehemu baba yangu hakusoma na nilitokea kuwa wa 25 chini ya 30, nikaona haya kumwonyesha. Lakini ikabidi nimwonyeshe kwa sababu ilitakiwa saini pale niirudishe skuli. Nilivyomwonyesha akaniambia umetokea wa 25 chini ya 30, kwa nini hawa watano umewabakisha hukuwamaliza? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais Benjamin Mkapa, alipowaasa wanafunzi kuwaambia msipoteze maisha kwa tamaa ya mwili. *Honourable Speaker Sir,* tamaa ya mwili ni moto ambao kila ukitaka kuuzima unazidi kuwaka, mwisho unakumaliza wewe mwenyewe unakuangamiza kabisa.

Mheshimiwa Spika, wale wanaokaa kiti cha nyuma wananikumbusha yule mzee mmoja aliyeua wazee wake wote wawili, halafu alipotaka kuhukumiwa anamwambia Jaji nisamehe, nihurumie mimi ni yatima sasa hivi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, ananikumbusha ile dhana ya *go from possible to impossible,* binadamu hakuumbwa awe kama chaza, akaye ndani tu ajifiche, tujitume zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kuhusu mirungi, imeenea sana Kariakoo, ukija Mombo, ukija Tanga. Natumaini hii mirungi itapigwa vita na wanaohusika. Vile vile waganga wa jadi wanawahadaa akinamama kwa kuwalaghai, wanatumia nyembe na mikasi na kuwahadaa kwamba dawa zikiingizwa mwilini ndiyo zinafanya kazi, wanaeneza Ukimwi. Lazima waganga wa jadi wadhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, watoto yatima wanafukuzwa shule kwa kukosa ada. Wanapinga baadhi ya walimu sera ya Serikali ya kuwafanya watoto yatima wasome bure.

Kuhusu *globalization,* lazima matangazo ya makampuni yanayowekeza nchini mwetu yaangaliwe. Kwa mfano, *ATCL* inasema Serengeti ni *Sahara Desert. Sahara Desert* kuna michanga tu kule na nge, huwezi kufananisha na Serengeti, Serengeti kuna neema ya Mwenyezi Mungu, *green land, fertile land,* hufananisha na *Zanzibar Island* na *Nothern Island, Northern Island* ni jela alikaa Mandela miaka yote kule.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alisema mficha maradhi kilio kitamwumbua. Kuhusu wakimbizi nanukuu, nukuu ya wiki katika Gazeti la Majira la tarehe 21 Septemba, 2003: "Wakimbizi wamekuwa mzigo kwetu, uharibifu wa mazingira, kuingiza silaha, ujambazi, kuvuka mpaka kwenda kufanya uhalifu katika nchi zao." Amesema haya Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, huruma yetu inatuponza. *Honourable Speaker Sir, we have to be cruel to be kind.* Alikuja mkimbizi mmoja Jimboni kwangu Mji Mkongwe pale Bandarini, nikamzuia kwamba wewe huna ruksa ya kuingia humu nchini Zanzibar. Alikuwa mfupi wa futi mbili tu. Nikamwambia wewe mbegu mbaya wewe hufai kuingia humu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, akhsante na nakushukuru, naunga mkono hotuba hii. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Semindu Pawa umesikia vizuri haya mambo? *(Kicheko)*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa na mimi kuchangia hoja ya Rais Benjamin William Mkapa, ambayo ipo mbele yetu. Awali ya yote niseme toka mwanzo kwamba ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Hotuba hii imegusa sehemu nyingi, lakini mimi nitalenga sehemu moja au mbili ambazo zinategemeana nazo nitazielezea moja kwa moja kwenye masuala ya maji, kilimo, mifugo pamoja na umeme. Maeneo hayo hayakuzungumzwa moja kwa moja kwa kuhusisha hoja ya hifadhi ya misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo kinategemea maji, umeme wa Tanzania kwa asilimia 65 unategemea maji na mifugo inategemea maji. Lakini maji haya siyo maji ya bahari, kwa vile maji hayo hayawezi kutumika kwa shughuli hizo, kwa vile maji ya bahari ni maji ya chumvi. Kwa hiyo, tarajio ni kupata maji yanayotokana na mvua. Bila mvua kilimo huathirika, kwa sababu ya ukame, hali inayopelekea njaa na ndiyo tunalia hapa Bungeni.

Kwa bahati nzuri, Mwenyezi Mungu aliumba nchi yetu yenye misitu ambayo imezunguka milima yetu na ambayo ndiyo vyanzo vikuu vya maji. Kwa bahati mbaya sana misitu yetu inavunwa kwa fujo bila utaratibu wowote hasa ukizingatia kwamba sehemu ambazo zinavunwa hivi sasa ni sehemu zile ambazo ni vyanzo vikubwa vya maji, maji ambayo yanatumika kuzalisha umeme na ambayo yanatumika kwa ajili ya *irrigation* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala hili tulilizingatia kwa karibu sana katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa, Mkoani Lindi baada ya kuona kasi ambayo misitu ya Rondo, misitu ya Liwale na jirani zetu Mahenge inavyoyoyoma, ni hatari! Kama kasi hii ikiendelea bila kuchukua hatua za kudhibiti haitachukua

zaidi ya miaka mitano kabla ya kuathiri *Hydro Power* yetu. Aidha, ukame uakuwa umejikita na hivyo kuifanya hali ya upungufu wa chakula iwe ya kudumu.

Nilitiwa moyo sana mwezi Desemba, 2003 wakati ilitangazwa kwamba Waziri mwenye dhamana ya misitu amezuia au kusitisha uvunaji ovyo wa misitu. Lakini nimeshangaa katika toleo la Majira ya tarehe 17 Februari, 2004 inasema, Wakata magogo wampongeza Mheshimiwa Meghji kwamba usitishaji wa uvunaji wa misitu umefutwa baada ya wiki tano sijui.

Mimi nilidhani kwamba usitishwaji wa kuvuna misitu ulifanywa ili Serikali ipate muda wa kutathmini suala hili kwa undani ili kuweka utaratibu muafaka wa kuvuna msitu wetu kwa hali endelevu. Lakini nashangaa Chama cha *TAFOPA,* wanampongeza Waziri kwa kufanya tathmini hiyo haraka haraka sana. Sijui tathmini hii imefanywa lini na wapi? Kwa sababu kutoka Mkoa wa Lindi, hakuna tathmini yoyoye iliyofanywa na kule ndiyo magogo yanayoyoma kwa kasi kubwa. Yule ambaye anataka kuona ukweli huu, aende katika bandari ya Mtwara, Dar es Salaam au asimame kwa muda mfupi tu, pale katika daraja la Mkapa, aone malori kwa malori yaliyojaa shehena ya magogo yaliyokatwa, yanapelekwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Pamoja na kuathiri misitu yetu na vyanzo vya maji, uvunaji wa magogo na kuyapeleka nje, unawanyima ajira watu wetu. Mkoa wa Lindi na naamini Mkoa wa Mtwara vile vile hauna viwanda, nilitarajia kwamba ungekuwepo walau utaratibu wa kuwezesha Mikoa hiyo kutumia maliasili yake kwa kuwawekea viwanda vya kupasua mbao na kutengeneza *furniture* ili wananchi wapate ajira na wakati huo huo kuongeza thamani ya mazao yetu ya misitu. Unapopeleka magogo nchi *unprocessed timber* thamani yake ni ndogo sana. Lakini ukipeleka *furniture* au *processed timber,* thamani ni kubwa kwa hiyo, nchi inafaidika zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi naiomba Serikali itazame upya maamuzi yake ya kuondoa amri ya kusitisha uvunaji holela wa misitu. Kwa sababu uvunaji ambao unaendeshwa hivi sasa ni mbaya sana. Magari yanayochukua magogo yanaharibu barabara na Halmashauri zetu hazipati faida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madaraja yanavunjwa na hali hii ikiendelea ni kwamba siyo tu wavunaji hao wataondoka baada ya kumaliza kuvuna misitu bali wataacha jangwa na nchi isiyo na mawasiliano ya barabara ya kuaminika.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa uchungu sana. Mheshimiwa Mgana Msindai, katika mchango wake alizungumzia juu ya umeme, kwamba hapa ndani kuna Wabunge ambao ni Wakurugenzi wa *TANESCO.* Mimi ni mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, ombi la Mheshimiwa Mgana Msindai, la kupata umeme katika Jimbo lake lilipokelewa na kampuni ya *TANESCO* pamoja na agizo la Mheshimiwa Waziri na kampuni iko mbioni kutayarisha mradi wa kuhitimisha agizo hilo.

Kwa bahati mbaya sana kutokana na athari zilizotokana na ukame ambao umesababisha uzalishaji wa umeme wa maji kupungua na hivyo kulazimika Shirika kununua umeme wa aghali kutoka *IPTL.* Mradi huu unasua sua kwa sababu fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya kupeleka umeme huko sasa imebidi zitumike kulipia kununua umeme *IPTL* ambao ni wa aghali sana.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mgana Msindai, tuwe pamoja katika suala la kulinda misitu yetu ili vyanzo vya maji visiathirike kama nilivyoeleza huko nyuma. Mheshimiwa Mgana Msindai yuko kwenye Baraza la Ushauri la Wizara ya Maliasili na Utalii na anatarajia kuwa atatumia fursa hiyo, pamoja na kutoa ushauri juu ya wanyamapori vile vile kushauri juu ya utunzaji wa misitu, bila hifadhi ya misitu wanyamapori hawatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, nilipokwenda Makerere mara ya kwanza mwaka 1957 ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kupita Shinyanga na Tabora wakati ule kulikuwa na msitu katika maeneo hayo

lakini ikatokea kampeni ya kuondoa Mbung'o, matokeo yake wakulima wale hodari sana walifyeka misitu yote na leo hii ukienda maeneo hayo huamini kwamba zama hizo sehemu hizo zilikuwa na misitu.

Aidha, wale waliosoma Jiografia watakumbuka jinsi gani nchi kama Mali na *Sahalin countries* zilivyokuwa na *Savanna forest* lakini kwa sababu ya uzembe wa kutoangalia misitu ile sasa hivi sehemu kubwa ya nchi hizo ni jangwa. Hapa tusipoangalia misitu yetu hatutakuwa tofauti na wale, tutaingiliwa na jangwa na ndio tutatizamana tukilaumiana.

Naiomba Serikali iwe makini, namwomba Waziri husika asitishe mara moja uvunaji wa misitu hii ambao unafanywa hivi sasa ili tukae chini na wadau wote tuzungumze jinsi gani tunaweza kutunza na kuvuna misitu yetu hii kwa njia endelevu vinginevyo kutakuwa na kusaga meno kama ilivyoandikwa kwenye *Bible,* tusingependa kufika huko. Sisi tulipewa nchi nzuri na wazazi wetu, na sisi pia tunawaachia watoto wetu nchi ya neema.

Mheshimiwa Spika, sipendi kuzungumza zaidi lakini nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na naomba kwa kuwa hotuba hii imesheheni basi Waheshimiwa Wabunge wote waichukue kama hadidu za rejea katika shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika, hongereni sana. *(Makofi)*

Hali kadhalika nimpongeze mama yetu, Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la *SADC.* Bila kumsahau Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kujumuika nasi katika Bunge hili kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa ujumla haina kasoro. Ni hotuba ambayo imeandaliwa kitaalam, ameisoma akiwa ametulia, hana wasiwasi, kwa hiyo, mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiisikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Rais unajiuliza kwamba yeye haya maneno aliyapata wapi na alifanya upembuzi upi wa kuweza kugusa maeneo mbalimbali kwa ufasaha namna hiyo. Lakini unakuja kupata jibu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bahati nzuri aliyopata ya kuwa karibu na Mheshimiwa Rais walichagua timu nzuri ya askari ya miamvuli ndio wanaotenda kazi hiyo na ndio mema yote hayo yanaonekana katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Kwa hiyo, nawapongeza sana maaskari wa miamvuli kwa kazi ambayo wameifanya na hotuba ya Mheshimiwa Rais ikaonekana kwamba ni hotuba nzuri. Kila unachoona kinaelea kimeundwa kwa hiyo, hongereni sana askari wa miamvuli. *(Makofi)*

Napenda niwahakikishieni kwamba huko mliko ni nafasi yenu nzuri na mnafanya kazi vizuri, sisi tuko huku kwa hiyo nawatakieni kila la kheri, malizieni huo muda uliobaki bila wasiwasi kabisa mnafanyakazi nzuri. Sisi tulioko huku na sisi tutunze nafasi zetu vizuri, Waheshimiwa Madiwani na wenyewe waendelee kubaki huko waliko watunze nafasi zao wasiingilie hizi za kwetu hizi, wasituvamie bwana bado tuna nafasi hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha kwa sababu ameleta hoja za namna fulani fulani za kuweza kutafuta mapato ya Serikali amepata, bado tena ameleta hoja ya kuomba hela hizo hizo alizozitafuta ili tumpe idhini ya kwenda kuzifanyia kazi, tumempa. Anatafuta pesa anakuja kutuomba pesa ni *discipline* ya hali ya juu, tunampongeza sana Waziri pamoja na Manaibu Waziri wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia suala la rushwa, rushwa wameigusa watu wengi lakini ifike mahali tuseme kwamba kwa kweli kama ni rushwa kwa Tanzania sasa hivi inapigwa vita ya hali ya juu sana. Hakuna Wizara iliyokuwa na matatizo kama Wizara ya Ardhi, jana Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, alizungumza hapa, mimi nimefanya utafiti katika Wizara hiyo hakuna sasa hivi rushwa kama wamebaki ni wale wapolepole. Nampongeza sana Waziri wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, anafanya kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa usipowapongeza watu wa namna hii unasema bado hawajafanya, hivi Mheshimiwa Wilson Masilingi mpaka ucharaze viboko watu ndio tujue kwamba unafanya kazi. Kazi unaifanya na inaeleweka na tuwasaidieni ili tuweze kutatua tatizo hili la rushwa. *(Makofi)*

Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Pius Mbawala, mnafanya kazi nzuri isipokuwa mmekaa mahali pabaya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nzito sana ina matatizo mengi hali ya hewa ikishabadilika lawama zinakuja kwenu lakini kazi mnafanya. Mambo ya *irrigation* mnajitahidi, mnafanya kazi tunaiona tusipowapongeza jamani tutawaweka mahali pabaya sana. Fanyeni kazi kwa uaminifu, endeleeni kugawa chakula cha njaa katika utaratibu uliopangwa ili angalau watu wetu waweze kunusurika katika tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitagusagusa kwenye Wizara tu, niingie kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nawapongeza sana Mawaziri wako wote wawili wanaokusaidia tukianza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Sera), Mheshimiwa William Lukuvi. Kazi ya kugawa chakula cha njaa ni tatizo kubwa mno Tanzania nzima sasa hivi ina njaa. Kwako kule Mheshimiwa Waziri Mkuu wana tatizo la njaa, Misungwi tuna tatizo la njaa, Shinyanga ndio usiseme, kila mahali wanalia njaa, utagawa wapi na wapi watakushukuru kwa namna ipi?

Mheshimiwa Spika, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tuongezewe pesa nyingine ili angalau tunusuru wananchi wetu, wana tatizo kubwa la njaa katika nchi hii. Tunaomba uongezewe pesa nyingine ili angalau tuweze kupata chakula kingi cha kutosha katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Habari na Utangazaji, tunakupongeza, vyombo vya habari sasa hivi angalau vimeboreka. *TVT* sasa hivi inaonekana kila mahali sasa wewe unataka mpaka iweje jamani tusipokupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, tunakupongeza sana kwa mawasiliano, kazi inaendelea vizuri. Nizungumzie tatizo moja tu la *TRC.* Kwa sasa hivi Mkoa wa Mwanza *cement* ni shilingi 13,000/= hadi 14,000/= baada ya mawasiliano kukatika bidhaa yote ya kutoka Dar es Salaam inapakiwa katika mabehewa yetu yaliyopo Dodoma.

Sasa hivi ukienda pale kwenye ofisi zetu hapa malori ni mengi sana. Kwa hiyo, vitu vimepanda bei hali kadhalika bidhaa kutoka Kanda ya Ziwa kwa maana ya ng'ombe na nyama kwa Dar es Salaam imepanda bei. Mawasiliano ni muhimu sana hebu mjaribu kutupa maelezo kuna matatizo gani kati ya Dar es Salaam na Dodoma mpaka malori yanabeba bidhaa kutoka Dar es Salaam kuja kupakia Dodoma hapa?

Nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, naye anafanya kazi nzuri tu, unajua Waziri Mkuu ulipokuwa unashauriana na Mheshimiwa Rais katika kuteua nadhani ulipata matatizo upande wa Manaibu kati ya Mikidadi mtu wa Dar es Salaam huyo na huyu Naibu aliyepo huyu Dr. Ibrahim Msababa, waliwapa shida sana uchukue yupi wote wana matatizo tatizo hivyo lakini ilifika mahali ukaona ni vema angalau Dr. Ibrahim Msabaha tuwe naye. Naye anafaa lakini tuseme kwamba anafaa na tunataka aendelee, anatufaa sana isipokuwa majibu yake yenye utani lakini ni ya msingi, nampongeza sana kwa kweli anafanya kazi nzuri kama ni umeme unaendelea kuwekwa katika mtandao ambao kwa kweli kila sehemu wanaweza kupata. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na mbolea?

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mmh! Mambo ya mbolea achana nayo hayo, huyo naye anajua ya kwake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisisahau jambo la maana kabisa kumpongeza Waziri wetu wa Elimu na Utamaduni, pamoja na Naibu wake. Kazi iliyofanyika ni za maajabu kuanzia milioni 13 kijijini wanapanga mipango yao ni jambo la ajabu halijawahi kutokea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi Ofisi za kwenye *briefcase* sasa hivi hazipo watu wanaenda kutafuta tenda kwenye vijiji wanalipwa, watu wanaandika *cheque,* ni jambo la ajabu haijawahi kuonekana katika ulimwengu huu. Tunawapongeza sana kwa kutuletea MMEM, Mheshimiwa Rais akumbukwe daima kwenye MMEM kwa kuiokomboa nchi yetu katika dimbwi la umaskini kwa kupitia elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimalizia watu muhimu zaidi ambao nilikuwa nimewabakiza ni Waziri wa Maji na Maendeleo na Mifugo. Kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga ni ukombozi kwa Wasukuma na watu wote. Tulikuwa na matatizo makubwa huwezi kuamini ni kilomita saba tu kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Wilaya ya Misungwi lakini ilikuwa haina maji.

Kitendo hicho ni cha kupongezwa kabisa na tunamhakikishia yeye akipata nafasi, Naibu wake akitembelea kwenye Jimbo letu la Misungwi, Solwa, Shinyanga nina imani kwa sisi Wasukuma kwa jinsi tulivyo na ukarimu ng'ombe wasiopungua 20 anaweza kupata kwa furaha, hiyo ninamhakikishia.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa!

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Aah, lazima tufike mahali tumweleze ukweli. Mimi nasema hivyo kwa sababu sisi wafugaji tumekuwa na matatizo ya ajabu mno. Ninayezungumza hapa, sio lele mama kama ni ng'ombe wanazidi 100 na kuendelea ninao ng'ombe wa kujivunia kwamba kwa kweli nafasi hiyo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Waziri Mkuu napenda kusema kwamba tumemsahau Mheshimiwa Rais katika Wizara anayoisimamia ya Serikali za Mitaa. Barabara nyingi vijijini zimekwama. Tatizo kubwa la wananchi wetu kuwatoa kwenye dimbwi la umaskini ni miundombinu. Wizara hii kwa sababu anaisimamia yeye nadhani imefika mahali basi tumkumbuke, tumpe pesa ili Mawaziri wake wanaomsaidia waweze kufanya kazi kwa ufasaha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nikupongeze Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwa kazi ngumu unayoifanya ya ubinafsishaji, kazi inaonekana kwa sisi tunaolala *Dodoma Hotel* tunajua hali ya *Dodoma Hotel* ilivyo, sasa hivi ni nzuri sana sio ndugu zetu akina George Lubeleje, wanakaa *Dodoma Inn,* hawajui mambo mazuri yanayotendeka kwenye nchi hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji umetusaidia sana, kwa kweli kwa *Dodoma Hotel* ni gharama lakini Mheshimiwa Richard Ndassa anafahamu, Mheshimiwa Paul Makolo anafahamu, ndio wanaolala hapo lakini wengine wanaolala maeneo mengine kwa kweli wana matatizo makubwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ubinafsishaji katika nchi hii umetuletea faida kubwa na nazidi kukupongeza Mheshimiwa Waziri endelea na msimamo huo ili tuweze kuneemeka katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kuhusu hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kwa kweli napenda nikushukuru sana jana ulitutangazia hapa kwamba idadi inaweza kuongezeka na nadhani ndio kwa msingi huo na sisi wengine tumeweza kupata hii nafasi ambayo tumeipata.

Mheshimiwa Spika, ulitoa sifa za hotuba ya Rais, mimi nazikubali kabisa. Mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Siha niliiona hotuba ile kwamba ni ya kijamaa *and one of the most scientific speeches* ambazo nimewahi kuzisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue *item* moja tu ile ambayo Mheshimiwa Rais anataka twende na wakati na tubadilishe fikra zetu. Wako watu wengine wanafikiri kwamba kwa kusema hivi anavyosema tunataka kuondoka katika msimamo. Hapa msimamo ni wa kijamaa imetamkwa ndani ya Katiba ya nchi. Ukiondoa maneno ujamaa katika Katiba ya nchi hii tutakufa, tutakwisha, tutakwenda na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanafikiri kwamba huu mwendo tunaokwenda nao ambao una mwelekeo wa kibepari huwezi ukasema ndani yake ndio unataka uingize mwendo wa kijamaa. Unatakiwa useme nina mwendo wa kijamaa na ndani yake nataka kuweka mawazo ya kibepari lakini nifike kwenye lengo la ujamaa, ndivyo anavyotuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengine wanafikiri kwamba ukiseme habari ya ubebari hivi ni mbaya sana, ngoja nim-*quote* Marx, Marx si ndiye baba mwenyewe wa ujamaa?

**WABUNGE FULANI:** *Correct!*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Marx alisema: *"One good thing about capitalism is that it develops the level of productive forces,"* huyo Marx ambaye ndiye baba askofu wa ujamaa anasema habari ya ubepari anasema kwamba huu una umuhimu wake na ndio maana unawaona Wachina wale wanaukumbatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja anacho-*insist, principles are never compromised,* huwezi ku-*compromise principles* na ndio maana tukiona kuna mahali hapa tunataka kwenda nje ya *principles* aah, ngoja kidogo hapa tunakwenda nje ya *principles* kama hili la ardhi. Hili la ardhi tumesema kwamba ardhi iendelee kubakia kuwa ni mali ya umma. *(Makofi)*

Mimi napenda kumpongeza Rais wetu nataka kujiuliza maswali yafuatayo: Hivi tu-*assume lets take it for granted* kama tusingechukua huu mwelekeo huu tung'ang'ana nchi hii ni nchi ya kijamaa, Azimio la Arusha, njia zote za uchumi ziwe mikononi mwa umma tusiende nje ya hapo, tungekuwa wapi leo, tungelipaje mishahara, tungenunuaje mafuta, wale watoto waliosimamishwa hapa mbele yetu tungewasomeshaje? Mjamaa wa kweli ni mjamaa ambaye siyo *static,* ni *eclectic,* ana-*borrow ideas,* anakwenda na wakati yuko *objective,* anaangalia *the objective realities* anakwenda nazo.

Mheshimiwa Spika, ukifanya hivyo na Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, hii habari ndio nilikuwa nasema pale Kivukoni, mimi ni mtu wa Azimio la Arusha nilikuwa nafundisha Kivukoni pale, hii haimaanishi ukifanya hivyo ndio umekuwa wewe sio mjamaa. Wewe wanakuambia mjamaa ukitoka nje maadui wako hapo halafu wewe unataka kupigwa risasi unasema kwa vile mimi ni mjamaa ngoja niji-*expose,* watakumaliza, akina Che-Guevara walivyofanya.

Mheshimiwa Spika, Che-Guevara alifikiri kwamba anaweza kuhamisha mapinduzi kutoka Cuba akayapeleka kule Bolivia walikwenda wakanyongwa hivi wakavuta ile tai akafaka. Kiongozi mzuri tu alifanya kazi nzuri alisaidia sana pale Fidel Castro na nani lakini nataka kusema kwamba mazingira ya pale Cuba ni tofauti na mazingira aliyokwenda kuyakuta kule Bolivia. Mazingira ya kwetu sisi hapa Tanzania ni mazingira tofauti kabisa na ya *South Africa* na maeneo mengine.

Napenda kuchukua nafasi hii nimesema haya maneno ya mwanzo, kumpongeza Rais kwamba amefika mahali ametuweka katika mwendo wa dunia na kwamba tunakwenda tunavyokwenda. Ni mwelekeo sahihi ndani yake anazungumza habari ya kudhibiti *relations of production* ambazo zinatutoa katika lengo. Ndani yake anazungumza habari ya ushirika ameusisitiza humu ndani kwenye hotuba nikasema hivi, hivi kwa hapa tulipo mimi sioni *problem* yoyote wala sina tatizo kabisa nina hakika kwa mwendo huu tuliokwenda hapa na namna tunavyokwenda Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika nchi yetu imetekelezwa kikamilifu.

Hii huna haja ya kuniambia kwa sababu kule kwangu mimi Siha watu wanakunywa maji, huna haja ya kwenda Chuo Kikuu kwenda kujifunza hivi wanakunywa au hawanyi, wanakunywa. Kama ni barabara zipo, tunaziona pale. Nchi za kihuni hazifanyi haya mambo tunayofanya. Nchi za kihuni watu wanafukuafukua tu hivi kama mihogo inafukuliwa na nguruwe na nini nchi *responsible* ndizo zinazofanya kazi kama hii inayofanyika. Liko daraja hapa kubwa tu, limekwenda Mtwara pale wahuni wangekuleta hapa ripoti ndefu, ndefu tuuu miaka 20 hadi 30 hakuna daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais amezungumza kitu kimoja kikubwa kwamba ile habari ya kwamba tunaiona Dar es Salaam tu 80% ndio tunategemea pale lazima isahihishwe. Hapa leo tunakaa huwezi ukaisaidia Mtwara, Kigoma, Kilimanjaro na Mikoa yote ya Tanzania bila ku-*develop infrastructure* yake, bila miundombinu yake kubadilika huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, changamoto inayoletwa kwetu hapa ni kwamba tufike mahali tuanze kufikiri kwamba tunafanyaje katika kusaidia barabara zetu, tunafanyaje katika kusaidia umeme, maji na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais anazungumzia suala la umaskini anasema yeye hakuahidi mtu yeyote kwamba ataweka hela ndani ya mfuko wake, *it is true* na tukienda nayo hiyo huwezi ku-*defend* hiyo kwa sababu haitatokea kwamba uhusiano wa uzalishaji mali tunaokwenda nao huwezi ukafika mahali ukawakuta watu wamejaza mapesa mfuko hata siku moja. *Relations of production* tunazokwenda nazo sasa hivi zitakuzalishia watu wenye uwezo mkubwa wachache na watu wengi ambao uwezo wao ni mdogo.

Sasa *capitalism* hakuna hata siku moja ukiweka hizo *relations* huwezi kufika mahali eti ukawa na matajiri wengi sana huku Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo hili ni lazima tulitazame kwa undani tujue kwamba tunachosema hapa ni nini. Wenzetu kule Ulaya walifanyaje, wenzetu kule Ulaya walichofanya walifika mahali wakajenga kitu kinachoitwa *Welfare Service* ndio wakatoa maji, barabara, shule, huduma muhimu zote kwa kufanya hivyo ndio unapambana na umaskini.

Mimi kitendo cha watoto wale kuletwa hapa na kuonyeshwa mbele yetu na kitendo cha kwamba jana tumepitisha *mini- budget* shilingi bilioni 2 kwa ajili ya watoto wetu ukitaka ku-*fight poverty* katika Tanzania toa elimu kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mambo aliyosema Rais mimi naondoka na hiki kitabu nakwenda ku-*localize* hii habari yote iliyozungumwa hapa na kuiweka katika mazingira ya Siha. Nitaitumbukiza pale halafu nita-*argue* kesi yangu pale halafu nione mtu atakayenitoa pale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda kuitumia, wenzengu wamesema wataitumia kama Biblia na nini, mimi nakwenda nayo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakwenda kuangalia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilivyotekelezwa katika Jimbo langu la Siha kwa kutumia hii *model* ya Rais hapa. Rai yangu kwa Wabunge wenzangu wote hapa twende na hii kitu, hii kitu hapa ndio salama yetu hii, hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho maana muda unakwenda na mimi hapa niko *fascinated* na hii hotuba hii linahusu Wilaya na Jimbo langu la Siha. Ukienda katika ripoti za Mheshimiwa William Lukuvi, utaona Wilaya ya Hai inaonyesha kwamba ina akiba ya chakula na kwamba ina kitu wanaita *surplus* (ziada). Mimi nataka nieleze nchi nzima kama nchi ukishakuta hatuna chakula cha kutosha hata wale ambao wamelima, wamepata na mvua za vuli na mvua ndefu zilipatikana wanakuwa na wao hawana chakula kwa sababu kitakachotokea pale ni suala la *The Law of Demand and Supply,* ndiyo itakayofanya kazi pale ita-*attract* tu itafika mahali kwa vile chakula hakuna bei zitapanda kinachotokea kwa mwananchi wa kawaida atawashika, atavutika, atauza chakula chote pale.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hii kwamba Wilaya yangu ya Hai na nataka nizungumze Wilaya katika ujumla wake na namsemea na Mheshimiwa Freeman Mbowe, hayupo hapa ndani lakini najua kwamba namsemea kwa sababu Majimbo yetu kule yako mawili, Jimbo la Siha na Hai nawasemea wananchi wa Wilaya ya Hai.

**MBUNGE FULANI:** Siyo Freeman Mbowe!

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Tuna tatizo pale la chakula kwa maana ya kwamba zipo kwanza *pockets,* Mheshimiwa Waziri Mkuu ukienda maeneo ya *West Kilimanjaro* eneo la Roselyn hawana chakula, ukienda maeneo ya wafugaji kama Lekrimuni hawana chakula, ukienda Magadini hawana chakula, ukienda Kandash hawana chakula ukienda Karansi hawana chakula, ukienda Makiwaru hawana chakula, ukienda Donyomoroko hawana chakula, ukienda Kishisha hawana chakula vijiji vyangu vingi vya Siha havina chakula. Nikinyamaza hapa nitakwenda kupata mgogoro ndio maana nakushukuru kwamba umetupa nafasi ya kuzungumza muanze kunisaidia ku-*cover* hiyo na Waandishi wa Habari kusema kwamba tuna tatizo la chakula. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Siha vilivyo vingi vina tatizo la chakula moja ni kwamba kuna *pockets,* kuna maeneo ya wafugaji ambayo kwa kweli yalipata mvua kidogo na kwa hiyo chakula chake kimeonekana ni pungufu lakini kuna pili hilo la kwamba pamoja na kwamba tulifanya kazi ya kusema kwamba jamani msiuze chakula lakini bado watu wengine walivutika na bei kwa hiyo chakula kingi kilitokea.

Napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba naiomba Serikali iangalie, nawasiliana na Mkuu wangu wa Wilaya tutapata takwimu kamili kuonyesha kwamba Wilaya ya Hai ikoje, lakini napenda kusema kwamba kwa kweli msije kuchukua hiyo picha ya kwamba Wilaya ya Hai ina chakula cha ziada halafu watu wakapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya yote, napenda kurudia kusema kwamba nampongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Joseph Mungai, alikuja katika Jimbo langu la Siha mimi nilimweleza kwamba tatizo kubwa lililopo pale kwa upande wa elimu ni nyumba za Walimu. Nyumba za Walimu mpaka sasa hivi tunaweza kufikiri kwamba sio tatizo, ni tatizo kwa sababu kama hakuna nyumba za Walimu maana yake ni kwamba Walimu hawawezi kukaa pale shuleni.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, napenda kumpa pole sana namwombea Mungu aondoke kwenye yale magongo ili aweze kutufikisha hapo anapotaka kutufikisha na atuachie nchi inapaa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ndio tumefika mwisho wa kikao cha asubuhi. Matokeo ya kura tulizozipiga leo asubuhi yameshakuwa tayari lakini kabla sijayasoma nitoe taarifa kwamba kesho na kesho kutwa mimi sitakuwepo Bungeni atakuwepo Naibu Spika kwa sababu ninakwenda kutekeleza majukumu mengine yanayonihusu nje ya nchi. *(Makofi)*

Matokeo ya uchaguzi wa mjumbe atakayeingia katika Tume ya Huduma za Bunge, Waheshimiwa Wabunge waliopiga kura jumla yao ilikuwa 230, mahudhurio mazuri sana, idadi ya kura zilizoharibika hakuna, wagombea wawili walipata kura kama ifuatavyo: Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi alipata kura 25 na Mheshimiwa Asha Ngede alipata kura 205. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Asha Ngede kwamba alimechaguliwa kuingia katika Tume ya Huduma za Bunge. *(Makofi)*

Baada ya hapo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri na nawapongeza Baraza la Mawaziri kwa kufanya kazi nzuri. Nategemea kwamba kama siyo Baraza la Mawaziri hata hii hotuba isingekuwa nzuri namna hii kwa sababu wao ndiyo wamechangia. Nadhani Mheshimiwa Rais alipokuwa akitoa hotuba yake alizungumzia kila Wizara na kila Wizara ilikuwa na mafanikio kwa hiyo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali ya Awamu ya Tatu imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwetu sisi tunasema kwamba wametekeleza asilimia karibu mia kwa mia. Lakini hata wengine ambao ni Wapinzani wanaweza kufikisha asilimia themanini au zaidi kwamba imetekelezwa. Kwa hiyo, mimi ningependa tu kusema kwamba kwa kweli hotuba tunaikubali, ni nzuri na ni mafanikio ya Serikali iliyoko madarakani hasa tukijua kwamba kipindi cha Awamu ya Tatu mwaka 1995, makusanyo ya Taifa yalikuwa ni shilingi bilioni 25/= kwa mwezi. Sasa tuko shilingi bilioni 106 kwa mwezi. Ni mafanikio makubwa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kusema kwamba kazi hii iliyofanyika ni kazi kubwa na tunaiomba Serikali iendeleze kwa sababu ndiyo mafanikio ya Taifa na kama alivyosema Rais anataka kuacha uongozi huku maendeleo ya Taifa letu yakiwa yamepaa na nadhani itakuwa ni vigumu sana kwa Serikali nyingine ya Awamu ya Nne, watapata kazi ngumu kuendeleza haya yaliyofanyika. Hata nadhani atakayepokea madaraka atakuwa tu ni mtu aliyeko katika hiyo ndege sidhani ni ndege itakayoshuka tena ardhini halafu kuandaa kuondoka tena, nadhani ni mtu aliyeko kwenye hiyo ndege apokee hapo hapo bila kushusha aendelee na safari wala bila kupunguza *gear*. Kwa sababu ndiyo wananchi wanaiandaa, nategemea watachagua Serikali ambayo itaendeleza haya yote yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni mtu mkweli na ni mtu mkweli ambaye haogopi. Unajua woga wakati mwingine ni dosari kwa kiongozi. Kama siyo ujasiri wake nadhani ubinafsishaji usingefanyika Tanzania, lakini amesimama kidete na amefanikisha na yameonekana matunda yake. Ningependa kusema kwamba kwa kweli viongozi wawe wajasiri na waitetee Ilani ya Uchaguzi kama walivyopanga wao wenyewe, nadhani Ilani ya Uchaguzi ni Chama cha Mapinduzi ndiyo kilipitisha na wakaiagiza Serikali ifanye na Serikali imetekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, woga ni kitu kibaya sana, nikitoa mfano, kulikuwa na watu wawili walikwenda kulina asali porini, baadaye usiku wakachoka wakalala. Mtu mmoja akamwona simba anakuja karibu yao na moto waliokoka umezimika kidogo. Alivyomwona simba akamgusa mwenzake, akamwambia hebu amka uwashe moto. Mwenzake naye alipofunua kichwa akamwona simba, akamwambia hebu na wewe washa kwa sababu wewe ndiyo upo macho mimi bado nalala. Wote wakabaki kufumba macho hakuna anayetaka kuamka. Sasa woga kama huo ni mbaya sana kwa sababu wameona hatari wote wakalala. Nasi tunataka kiongozi atakayetuamsha, atakayetuambia twende. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulizungumzia jambo moja ambalo naliona kwamba kila siku Serikali inalikwepa na hili suala nadhani Mheshimiwa Rais alilizungumzia katika hotuba yake ukurasa wa 26, nalo ni kuhusu ushirika.

Mheshimiwa Rais alizungumzia mambo ya ushirika. Katika ushirika kuna ushirika wa wakulima, wavuvi, wafanyabiashara na akasema nguvu ya mnyonge ni umoja. Sasa huu umoja Serikali wameandaa Vyama vya Ushirika katika maeneo hayo matatu, lakini katika ufugaji naona Serikali wameacha kabisa sijui kwa nini hasa katika mikopo, wafugaji hawapati mikopo. Mwaka 2003 Rais alisema kwamba ushirika wamepewa bilioni kumi *point* moja, mwaka 2003/2004 wamepewa bilioni kumi na sita *point* tatu. Sasa wafugaji wameachwa. Serikali haitambui wafugaji, hii Serikali haithamini kabisa wafugaji. Nashangaa kwa sababu hii Serikali kama ni wananchi ndiyo wameichagua, wafugaji nao wamo. Wabunge wengi hapa pamoja na Rais mwenyewe walichaguliwa na wafugaji, sasa sijui kwa nini wanasahaulika. Hakuna hata pembejeo, wakulima wanapewa fedha za ununuzi wa matrekta na pembejeo lakini huoni mikopo wanayopewa wafugaji hivi ni kwa nini!

Sasa nashangaa, kidogo nikakumbuka usemi mmoja, siku moja Rais alisema kwamba: "Yeye alianza kumwona ng'ombe akiwa sekondari, akaanza kunywa maziwa akiwa Chuo Kikuu." Nadhani hata katika Baraza la Mawaziri wengi wapo hivyo hivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo inasababisha mifugo inasahaulika kabisa. Sasa ningependa kuikumbusha Serikali kwamba wafugaji jamani na sisi tunataka tupate mikopo na madawa ya mifugo. Pembejeo kwa wakulima na madawa kwa wafugaji, vinakwenda sambamba, sijui kwa nini wanakumbuka pembejeo katika kilimo wanaacha mifugo. Kenya wanawathamini sana wafugaji wao, hata kipindi hiki wanakarabati Kiwanda cha *Kenya Meat Commission* ili wafugaji waweze kupata soko, hivi Serikali ya Tanzania ina nini na kwa nini haiwakumbuki wafugaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Waziri wa Ushirika na Masoko, hebu wakutane waone kwamba watawasaidiaje wafugaji, wasituache hewani na sisi tunataka kuingia katika soko la dunia, tunataka na sisi mifugo ipate thamani, tunataka ngozi. Ngozi nyingi sana hazina bei. Kwa hiyo, ningependa tu kusema hayo katika mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la mwisho ambalo ningependa kulisemea ni suala la umeme. Tarehe 14 Julai, 1997 Mheshimiwa Rais alikuja Longido akaahidi kwamba kabla ya uchaguzi wa mwaka 2000 umeme utakuwa umefika Longido na Namanga. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, akiwa Waziri naye akasema lazima mwisho wa mwaka 1999 umeme utakuwa umefika Longido lakini mpaka sasa hakuna umeme Longido. Tunasema kwamba Rais amesema, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe.

Sasa pale Namanga kuna watu wengi sana ambao sio wakulima wala wafugaji bali wanategemea biashara wanataka kuwa na viwanda vidogo vidogo lakini hawana umeme na ni mpakani, ndiyo mpaka wa Tanzania na nchi nyingine. Mpaka sasa wala hakuna kinachofanyika, ni ubabaishaji mtupu. *World Bank* wamekubali kusaidia lakini sijui nini kilichoko Wizarani, nadhani hicho kigugumizi ambacho Wabunge wenzangu wanasema kwamba kuna kigugumizi nadhani kipo hata katika umeme wa Longido-Namanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia kwa kifupi hotuba nzuri na ya kina aliyoitoa Mheshimiwa Rais kwa Bunge lako Tukufu. Nampongeza sana kwa hotuba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kweli ilikuwa ni ripoti ya kazi kwa kipindi alichokaa madarakani na ilikuwa ni mwelekeo wa kule tunakotamani kuwa na kufika. Kwa kweli ilikuwa ni taarifa nzuri na ya kina isiyokuwa na dosari na hata viongozi wa Upinzani waliokuwa *Speaker's Gallery* walikuwa wanaishangilia kwa kupiga makofi. Sasa nashangaa tu kwamba walipokwenda kuhojiwa wakaanza kutoa makosa ya hapa na pale. Ni hotuba nzuri ambayo ni mwelekeo na dira ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hotuba hiyo naomba tu nitoe ushauri wa bure kwa wale wote wana CCM wanaowania kugombea Urais kwa kupitia tiketi ya CCM waanze kujipima kwa misingi ya hiyo hotuba na kwamba hawatatu-*let down* Watanzania pindi watakapokuwa wamepata hiyo nafasi. Pia kwa Wapinzani mimi nasema kwa jinsi ilivyotolewa kwa umahiri na kwa jinsi inavyoonyesha *success story* ya kazi ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na Chama cha Mapinduzi kwa kweli kama wana raslimali katika kugombea na kuweka wagombea, waanze kujitoa mapema kwa sababu wataangushwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa na ujasiri wa kuwa na sera ya uwekezaji na ubinafsishaji. Wote kama wana CCM na kwa kweli kama wananchi tunaunga mkono hatua ambazo Serikali ya Awamu ya Tatu imezichukua katika kukuza uchumi wa nchi hii. Kwa kweli wale wanaopinga ndiyo wale wanaoitwa vipofu au kwa makusudi hawataki kuona mema yaliyokwishatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika ubinafsishaji lazima kama wananchi na kama Wabunge tutoe ushauri kwa Serikali. Najua kuna takwimu ambazo ni sahihi kabisa ambazo Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, amekuwa akitupa kwamba tusifikirie mwelekeo kuwa ni nchi moja inayonunua tu na kuwekeza katika nchi yetu. Tunakubali kabisa katika hili. Tatizo tusiangalie nchi au ni kiwanda kipi au ni asilimia gani ya uwekezaji ambao umefanyika.

Nafikiri tuangalie *impact* ya vile viwanda au mashirika ambayo yamenunuliwa na hiyo inayodaiwa kuwa ni nchi moja. Natoa mfano tu wa hiyo nchi ambayo imenunua *Breweries,* kama *Breweries* kwa mfano wakigoma kwa siku moja *impact* yake kwa uchumi wa nchi ni mkubwa sana kuliko *HANDICO* wakigoma mwezi mzima na hili ndilo tunalolizungumza kwamba tusielekee huko. Tunaweza kuona ki-*percentage* kwamba si nchi ile iliyonunua, lakini sisi tunachoishauri Serikali ni kuangalia *impact* ya uchumi wa nchi kwa ujumla inakwendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi tuangalie kwamba wale walionunua *NBC, TBL* au *TANESCO* kama watakuja kununua si Nelson Mandela, si Walter Sisulu, ni watu ambao tulikuwa tunawaimba kaburu matata hiya. Yale mawazo waliyokuwa nayo bado yako pale na ndiyo maana tunaona migogoro mingi inajitokeza hata *NBC* na *TBL,* ni kwa sababu *mentality* ya wale watu waliochukua bado iko pale pale.

Sasa pamoja na *success story* ya ubinafsishaji na uwekezaji tungeishauri Serikali kwamba iangalie *impact* kwa uchumi wa jumla inakuwaje kama kukitokea matatizo katika haya. Mimi naamini kwamba Serikali yetu inasikia kwa sababu kiongozi mzuri ni yule anayesikiliza na kujali maoni ya wale anaowaongoza na sisi kama wadau nina hakika tuna haki ya kuikosoa Serikali au kutoa maoni yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege ya Mheshimiwa Rais ipo kwenye *run way* inataka ku-*take off,* tunampongeza sana. Ninachomwomba tu asiwe mwanasiasa na Serikali isiongozwe na wanasiasa na wanasiasa wakaamini kwamba abiria wote yaani Watanzania wote wapo ndani ya ndege, wengine bado hatujapata hata tiketi ya kupanda kwenye hiyo ndege. Wakati tunazungumzia umeme wa vijijini katika baadhi ya maeneo Mkoa wa Kigoma bado hatujawa na uhakika wa umeme kwenye Makao Makuu ya Mkoa. Wakati tunazungumzia kupeleka Hospitali katika maeneo kadhaa, bado Tarafa ya Kasanda haijawa na kituo cha Afya kama Tarafa, sasa Mheshimiwa Rais ajaribu kuhakikisha kwamba wale wadau wote anaotaka kuruka nao katika ndege wote wapo katika ndege ili itakapo-*take off* isije kuwaacha wengine hawajapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yote yanaweza yasiwe na maana kama suala la rushwa hatutalizingatia na kulipiga vita kweli kweli. Mimi bado naamini kwamba Mheshimiwa Rais yeye binafsi ni mwadilifu na bado ni Amiri Jeshi mzuri katika vita hii ya rushwa. Lakini nina tatizo na baadhi ya wasaidizi wake sina hakika na wao kweli wapo *committed* katika hii vita ya kupiga vita rushwa, sijui kama kweli anapata msaada anaouhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu Morogoro, kiongozi mkubwa kabisa wa Jeshi la Polisi anazungumza kwamba rushwa ya askari polisi ni ndogo ukilinganisha na rushwa inayochukuliwa kwenye mikataba. Sasa hapa inaanza kunipa taabu kwa sababu huyu ndiye alitakiwa kupiga vita zote mbili, vita ya rushwa ndogo na vita ya rushwa kubwa.

Sasa unapoanza kulinganisha unaipa asilimia ndogo hii vita ya askari polisi kwamba ni ndogo haina madhara kwa uchumi wa Taifa, sina hakika na *commitment* yako katika kupiga vita rushwa. Kiongozi mwingine kabisa tena wa Baraza la Mawaziri naye anasema kwamba kuwa maskini si uadilifu, si lazima uwe mwadilifu na kuwa tajiri siyo dhambi. Sasa kiongozi anapokuwa anaongea namna hii inaanza kutupa taabu kwamba si wote ambao wanamsaidia sana katika kupiga vita rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani mwaka 1995, alikuwa anahojiwa na Mwandishi wa Habari anaitwa David Martin na yeye katika kusisitiza alisema, naomba kunukuu: "Kama watu hawaachi kukwambia kuwa fulani anafanya hivi na fulani anafanya vile hata kama hakuna ushahidi, lazima uwe tayari kumwita mtuhumiwa na kumwambia ehee, bwana ehee, kwa jinsi ilivyo ni kwamba wewe sasa ni mzigo kwa Serikali, hufai kwa kufuata vigezo vya utawala bora. Kwa hiyo tafadhali jiuzulu. Hili ni suala la ujasiri." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kumekuwa na vitendo vya kuwastaafisha na kuwaachisha kazi baadhi ya watendaji lakini wengi wanasema kwamba *impact* yake bado ni ndogo na wote tunategemea kwamba hii vita haijaisha ndiyo kwanza ime-*take off.*

Kwa hiyo, kama kuna watu ambao wanatiliwa mashaka ndani ya Serikali ili aweze kuondoka na rekodi nzuri zaidi ya hapa alipofika tunategemea kwamba watu kama hao hatasita kuwaondoa na sisi kama Watanzania tunaamini ana ujasiri na tutaendelea kumlinda hata kama atakuwa ametengeneza maadui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda unakwisha labda niishie na *quotation* ambayo aliitoa Rais wa kwenye Mheshimiwa Emilio Mwai Kibaki, wakati anahutubia Bunge la Kenya kwa mara ya kwanza, alisema: *"In the past some of those who are did perceived as most responsible for corruption set in this August Parliament or occupied other positions of Public trust. Corruption start at the top, now the fight against corruption in Kenya will start at the top."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutajijengea utaratibu wa namna hii na kama watakuwa wamo ndani ambao wapo *at the top* tukichukua hatua mimi naamini kabisa kwamba nchi itakuwa imesafishika na watu wataona kwamba tupo *serious* na upigaji vita rushwa. Sisemi kwamba wapo lakini ni vigumu pia ku-*prove,* lakini watu wanapokuwa wanasema watu *very responsible* lazima ujue kwamba kama haya yanasemwa inawezekana kweli yapo. Kwa hiyo, ni juu ya vyombo vinavyohusika kuanza kuchunguza kama kweli haya yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Transparency International* walisema kigezo kimojawapo cha kuangalia rushwa katika Serikali au katika jamii ni kuangalia ni wangapi ambao wana hisa katika makampuni ambayo yamebinafsishwa na kuangalia ni wangapi ambao ni Wenyeviti wa Makampuni kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu labda Mheshimiwa Wilison Masilingi na timu yake watusaidie ni wangapi ambao wapo, ni watu gani *influential* maana yake walisema angalieni watu ambao ni *influential* ambao ni Wenyeviti wa Makampuni yaliyobinafsishwa, labda inaweza kutusaidia kwa *levels* kwa *comparisons* za *Transparency International* kuona kama kweli huu ugonjwa wa rushwa ume-*penetrate* katika jamii yetu kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena kwamba hotuba ilikuwa nzuri, yenye mwelekeo, yenye matamanio makubwa na nina imani kwamba itatufikisha mahali tunapotaka kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuchangia machache juu ya hotuba ya Rais. Kwanza kabisa nampongeza Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo inatutaka tutekeleze na amesema hivyo miezi iliyobakia ishirini itapaswa tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa katika Bunge la Afrika, *SADC* na Mbunge Charles Makongoro Nyerere ambaye amechaguliwa na Rais kuingia Bungeni na leo asubuhi tumepiga kura kumchagua Mheshimiwa Asha Ngede, amepata kura nyingi sana. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kidogo kwa dondoo inayofuata. Asubuhi nimemsikia Mbunge mwenzangu kutoka Moshi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya akilalamika kuwa wanachama wake na Madiwani wanarudi CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nampongeza sana mlezi wa Mkoa ule ambaye ni Waziri Mkuu aongeze nguvu kidogo. Akiongeza nguvu kidogo hata Mheshimiwa Thomas Ngawaiya huyo anaweza kumvuta akaja huku maana yake anaonyesha anaanza kukata tamaa, jambo

ambalo linaweza kumsababisha kurudi na kuja CCM. Nawapongeza na wananchi wote, viongozi wa Kilimanjaro kwa kazi hiyo ya kuwarudisha wanachama ambao wameanza kurudi CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge wale waliokuwepo hapa tangu mwaka 1995, tumeshuhudia Mheshimiwa Rais wetu mwenye sifa za kipekee, mwenye kutetea mamuzi yake na ambaye amehuisha uchumi wetu na wote mnajua kuwa yeye ni muangalifu mkubwa wa kueleza ukweli halisi hata kama unaoumiza. Tumekuwa tukilalamika huko nyuma jinsi Bajeti ilivyokuwa inakwenda hatukujua kama Bajeti baadaye ingeweza kuwa nzuri katika hali hii ambayo imehuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kuwa imeboresha makusanyo ya kodi na imeanzisha Taasisi ya *TRA.* Nampongeza Mheshimiwa Rais na Marais wenzake pia kwa kurejesha Jumuiya ya Afrika Mashariki na kurudisha tena amani katika *DRC,* Burundi na kadhalika. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusimamia ulipwaji wa madeni ambayo yamepelekea kufutwa kwa madeni mengine, jambo ambalo lisingewezekana kama pengine siyo busara zake na umakini wake. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchagua safu nzuri ya Mawaziri ambao yeye aliwaita ni askari wa miavuli na kama alivyosema yeye katika ukurasa wa pili wa hotuba yake naomba ninukuu: "Napenda nianze kwa kurejea kwenye muhtasari nilioutoa kuhusu sura kuu za mwelekeo wa miezi 20 ijayo. Nitasoma kwa kifupi tu, amesema kwanza kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiendeleza. Pili, kujenga na kuimarisha uwezo Kitaifa wa udhibiti, uratibu na usimamizi wa uchumi wa soko. Tatu, kufikiria upya haki za wanyonge wakiwemo wananchi walio katika sekta isiyo rasmi, nne, kuweka kipaumbele kinachostahili kwenye mauzo ya nje ya nchi, na tano, kuondosha vikwazo vilivyo katika njia ya Watanzania walio tayari kujiendeleza."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezisoma hizi kwa kifupi kwa sababu nafakiri sasa wenzetu hawa wasimamizi ambao wamewekwa kama askari wa miavuli wataweza kujenga na kuimarisha uwezo wa Kitaifa na udhibiti huu kama Mheshimiwa Rais alivyosema. Udhibiti wa usimamizi wa soko tunaliita soko huria lisije likaendelea kuwa soko holela, wataweza kusimamia kuzuia mifumuko ya bei ingawa nayo kama mvua hazinyeshi na vinginevyo huwezi ukazuia. Wataweza pia kusimamia au kurekebisha hali ya *interest rate* za mabenki zisiwe zinayumba. Unapokopa wanakutoza riba kubwa sana lakini unapoweka unapewa riba ndogo sana. Wataweza kuboresha *inflation* wakizingatia kushuka kwa mara kwa mara kwa shilingi yetu ambalo ni jambo tumekuwa tukilizungumza sana hapa.

Haya yote ninayosema yanatakiwa kuboreshwa kwa *reserves* zetu za biashara za nje zikue ili kuimarisha *currency* yetu kama tunavyosema. Inabidi kwa pamoja sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na hao wenzetu tushirikiane ili tuweze kuhuisha uchumi wetu uweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, *currency* yetu inapoporomoka *consume prices* zinakuwa juu yaani bei za walaji zinakuwa juu, mkulima naye hafaidiki, na bei za mazao ya kilimo bado zinakuwa ndogo hivyo kuwafanya wananchi walalamike. Mheshimiwa Rais amesema lazima tuweke kipaumbele kinachostahili kwenye mauzo ya nchi za nje ikiwemo kuongeza thamani ya bidhaa ambazo tunazipeleka nje au ziweze kusindikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia Serikali kwa wakati huu itafute uwezekano wa kuwafundisha wananchi jinsi ya kuuza mazao yale ambayo nchi za nje wanayataka mazao madogo madogo kwa mfano hasa vyakula kama wanavyofanya wenzetu wanaleta nyanya toka *South Africa* hapa.

Lakini na sisi tunaweza tukapata masoko mengine ya kupeleka kama Comoro na kwingineko tukapeleka nyanya, vitunguu, asali na vinyago. Inashangaza sana siku hizi nchi jirani zina mabasi karibu matano yanakuja hapa na sisi hatujashtuka, lakini wanakuja wananunua vitu vidogo vidogo tu kama vinyago wanapeleka kule kwao na hapa wananunua kwa *local currency,* lakini wakienda kule wanauza kwa *foreign currency* ambayo inakuwa inaingia kwao. Hili tumelisema sana na hata maua na ipo haja ya Serikali kuangalia sasa pamoja na ndege nyingi kuingia nchini kuwepo na ndege zinazoweza kubeba bidhaa za biashara mahsusi kwa wananchi ambao watakuwa wameelekezwa jinsi ya kufanya ili tu mradi tuweze kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee juu ya elimu, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha MMEM, madarasa mengi mazuri yamejengwa, kinachohitaji ni watoto waende shule. Naupongeza Mkoa wa Mbeya pia kwa ajili ya wanafunzi kufanya vizuri na hasa pia shule zangu kule kwa miaka miwili ya nyuma shule yangu ya *Ngwara Prison* imekuwa ikiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ngwara Prison* ni Gereza ambalo lilijengwa zamani kwa ajili ya wafungwa watukutu, tulifikiri ni mbali sana sasa hivi ni karibu, wale wafungwa watukutu walikuwa wanapelekwa kule. Namshukuru Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa sifa za shule hiyo ameweza kufika kule. Inasemekana Mheshimiwa Waziri wa kwanza kufika kule alikuwa Hassan Moyo ni siku nyingi sana. Hili Gereza lilianzishwa na *Comrade* Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru na eneo lile la Ngwara limekuwa zuri, sasa hivi kwa sababu kuna shule hizo mbili za *Primary* ambazo hiyo mojawapo imekuwa ikifanya vizuri na mwaka huu kidogo imetetereka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamekuja kwenye Jimbo langu akiwemo Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Daniel Yona na Mheshimiwa Joseph Mungai. Natarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye safari hii shughuli za Bunge zikimalizika labda unaweza kupanga kututembelea kwa sababu wananchi wana hamu sana na wewe. Kwa hiyo, tunakukaribisha uje ututembelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango huu wa MMES unaokuja baada ya kujengwa kwa madarasa haya ya elimu ya msingi maeneo yetu mengine yamekuwa hayana shule za sekondari kama walivyosema wenzangu ni kwamba tungeomba Serikali iangalie upya ili iwezeshe maeneo yale yaweze kupewa fursa ya kujenga shule nyingi za sekondari.

Lakini yapo matatizo ya msingi katika shule za msingi na shule za sekondari. Kuna wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda Mtwara akawaambia wanafunzi wote waliotoroshwa, waliopewa mimba warudi shuleni na tukasikia wamerudi. Hili ni tatizo kubwa katika shule nyingi hapa nchini. Tunaomba kama kutakuwa na kauli hiyo ili wanafunzi waweze kwenda kuzijaza zile shule za sekondari kwa sababu kujenga tu shule za sekondari pasipo kuwa na wanafunzi kuwepo inakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuishukuru Wizara ya Ujenzi kwa kuboresha barabara zangu, karibu Bunge nzima nimekuwa nikilalamika juu ya barabara na juzi niliuliza swali langu hapa. Pia kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa kusogeza umeme kwenye Mji wa Mkwajuni. Ninalo ombi rasmi kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ule Mji wetu wa Mkwajuni tulijenga siku nyingi kwa kuuandaa kuwa Wilaya, yapo majengo mazuri na tulikuwa na sababu za msingi kuujenga kwa sababu sisi tuko mbali sana na Wilaya, tulitegemea kuwa pengine kwa kujenga yale majengo tungeweza kupewa angalau Wilaya ndogo, lakini kwa sababu ya fedha kuwa kiasi kidogo hatujafikiriwa ombi hilo. Bado nalileta ombi hilo kwa Serikali na nafikiri itakuwa rahisi zaidi kiutawala kama utakuwa karibu na wananchi. Ningependa kwa kweli ombi hilo Serikali ilichukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema ukweli Serikali imefanya kazi ambazo huwezi ukazisema zote hapa Bungeni . Ukianza kuorodhesha zitachukua muda wako wote ambao unaweza kuzungumza. Kitu ambacho nataka kusema ni kwamba tunaiomba Serikali kwa muda huu uliobakia kuangalia maeneo yale ambayo bado tunalalamika Waheshimiwa Wabunge hapa ili waweze kutusaidia tukayaboresha ili kusiwe na matatizo mengi na tukidhi matarajio ya wananchi na hasa kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita anayefuatia niseme tu kwa orodha ambayo nimepata hapa ni wachangiaji 42 na kama mlivyosikia hoja hii inaisha siku ya Ijumaa. Kwa hiyo bado kuna nafasi ya leo, kesho na Ijumaa kabla Mheshimiwa Waziri Mkuu hajamaliza Bunge jioni, basi hawa wataendelea kuchangia. Lakini nina hakika kwa leo na kesho wote mtachangia.

Kwa hiyo, wachangiaji nilionao hapa ni 42 kwa orodha ambayo nimepewa. Sasa walionipa barua, wengine wameshangaa nawajibu kwamba sioni majina yao na ni kweli siyaoni inawezekana hawakuandikwa au waliandikwa lakini majina yakaonekana hawa 42 ndiyo wachangie. Kwa hiyo, sasa tunaendelea. Anayefuatia ni Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, simwoni. Mheshimiwa Ruth Msafiri atafuatiwa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Halima Kimbau, pia ajiandae.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami naungana na wenzangu katika kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa Bungeni hapa tarehe 12 Februari, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa yeye ni mtu mwenyewe shughuli nyingi, anashughulikia mipango ya ndani ya nchi na ya nje ya nchi, majukumu yake ni mengi na makubwa. Lakini bado aliona umuhimu wa kutenga muda wa kuja kuzungumza na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaonyesha ni kwa kiwango gani Mheshimiwa Rais anavyolithamini Bunge hili aliloliita Bunge ni mshirika wake mkuu katika kazi anazofanya. Mheshimiwa Rais wetu ninaomba kabla hajamaliza miezi 20 iliyobaki basi apange tena muda aje azungumze nasi ili tuweze kufaidika na hekima na busara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu ilikuwa ni zito sana na ilijaa wingi wa maelekezo, lakini zaidi ilionyesha taarifa ya kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya kwa kipindi chote cha miaka minane. Kwetu sisi kama aliowaita washirika wake, kwetu ilikuwa kama ni maelekezo ama ilikuwa ni kama twende tukafanye kitu gani. Kwa upande wetu sisi tumeipokea kwa namna mbalimbali, lakini zaidi wote tumeipongeza kwa sababu ilikuwa ni hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie maeneo machache tu. Nianze na eneo la wananchi wanapokuwa wamemuelewa kiongozi wao, wanapokuwa wamemuamini, wanapokuwa wana imani kwamba hayo anayokusudia kuyafanya ambayo amewaeleza hakika ataweza kuyatekeleza.

Kwa hiyo, uaminifu, uadilifu na uwazi wa Mheshimiwa Rais wetu ndiyo umewezesha mafanikio haya yote ambayo ameyafanya. Kwa hiyo, hata katika kipindi hiki ambacho sasa tunaelekea katika mabadiliko ya uongozi kuelekea mwaka 2005 kutoka uongozi uliopo kuelekea uongozi ujao ama kuingia katika kufanya uchaguzi tena, ni wakati ambapo wananchi watapaswa kuyapima hayo, kuupima uadilifu wa kiongozi wao, kuupima uaminifu wa kiongozi wao, kupima ukweli wa hayo ambayo anayazungumzia na uwekezano wa kutekelezeka kwake. Si tu kumtazama mtu na kumuunga mkono kwa maneno pengine mazuri anayoyazungumza, lakini lazima imani kwa kiongozi iwe wazi, lakini imani hiyo ielekeane kwamba yeye nguvu za kuyatekeleza hayo anayayozungumzia atazipata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameyafanya haya baada ya kuwa amefanya juhudi kubwa sana ama za kuomba tusamehewa madeni, kuimarisha ukusanyaji wa kodi na mapato yakawa mazuri, na sisi sasa leo tumeweza kwenda kifua mbele tukishangilia kuboreshwa kwa elimu yetu. MMEM tumeiona na bado ipo, tukishangilia mazingira mazuri ya elimu tangu shule za msingi, usajili wa watoto na hata wanavyoweza kuhitimu masomo yao na mahudhurio mazuri darasani yametokana na juhudi za Mheshimiwa Rais wetu.

Lakini vile vile tumeona uboreshaji wa huduma za afya umekuwa mkubwa ambacho nakiomba sasa hivi huduma hii ya afya iongeze upanukaji wake uwe mpana mpaka kufikia maeneo yote ya vijijini ambapo wananchi walio wengi bado hawajafikiwa ipasavyo na huduma ya afya. Hata pale ambapo huduma ipo wananchi wanatembea mwendo mrefu kwenda kuifuta na bado wakati mwingine dawa hazitoshelezi zinaisha kabla ya wakati. Lakini kwa kweli huduma ni nzuri na tungeliomba hii ikaboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushukuru kwa hali nzuri ya mawasiliano. Wakati mimi nachaguliwa kuingia katika Bunge hili nilikuwa siwezi kupata simu nikiwa kijijini wala nikiwa Makao Makuu ya Wilaya kama si kwa simu za *TTCL*. Leo naweza nikazungumza katika kata zangu 12 na ninaweza nikapata mawasiliano katika vijiji vyote 118 kasoro vijiji vitatu tu ambavyo nami naamini katika muda si mrefu hali itakuwa imeweza kuwa nzuri zaidi. Hali hii inaonyesha kwa kiwango gani ambavyo

Mheshimiwa Rais wetu ana juhudi za kusimamia uchumi na kipindi anachokusudia kuondoka ni kweli ataacha Tanzania inapaa. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie masuala mengine tu ambayo mimi nayazungumza kama ni njia ya kuchukua tahadhari kwamba kuna mambo mengine ambayo tumeyazoea kuona yanazuka katika nyakati za uchaguzi. Tunapoingia katika wakati wa kutaka kuchagua viongozi kuna mambo mengi ambayo yanajitokeza kwa namna fulani si mambo mazuri ambayo yanafaa kunyanyamazia na kwa kuwa tumepata kipindi hiki cha kuzungumza kabla hatujafikia katika kipindi chenyewe cha uchaguzi ni vyema tahadhari hizi zikachukuliwa kuanzia sasa.

Wenzangu wameyazungumzia, lakini na mimi nayadokeza tu sina kusudio kubwa la kuweza kuyasema kwa undani. Lakini lipo tatizo linalojitokeza wakati wa uchaguzi la masuala ya udini, masuala ya ukabila, masuala ya umaeneo, masuala ya ujinsia, masuala ya utajiri na umaskini na masuala ya rushwa kwa msingi huo. Kwa sababu unapoanza kusema maskini na tajiri, maana yake mwenye fedha anazitoa na asiye nazo hana kitu. Kwa hiyo, kura zitaenda kwa aliyetoa fedha, tayari sasa unaanza kuingiza watu wenye fedha ndiyo waingie. Lakini katika masuala haya kwa kipindi hiki mimi naomba haya yadhibitiwe mapema kabisa na yawekwe wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ambacho sisi Waheshimiwa Wabunge tuko hapa Bungeni, mazungumzo sasa yalikuwa makubwa katika Majimbo yetu na taarifa tunazoziletewa hapa ni jinsi ambavyo kuna maandalizi makubwa ya watu kuandaa sherehe, kuandaa vyakula, mikutano isiyo rasmi, semina zisizoeleweka ilimradi tu watu wanatafuta wawape nini wananchi kama njia ya kujiwekeza ili baadaye waweze kuomba uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi haupatikani kwa njia hiyo. Uongozi haupatikani kwa mtu kupita tu na kufanya ulaghai. Wananchi wa sasa siyo wale wa zamani, wananchi wa sasa wanaelewa tunaposema mtandao umekwenda mpaka vijiji vyote vya Muleba Kaskazini miaka mitatu tu iliyopita, basi na uelewa wa wananchi umekua haraka vilevile. Wananchi waliokuwa wakidanganywa kwa kuambiwa mambo ambayo ilikuwa ni vigumu kujua Muleba kuna nini, Bukoba mjini kuna nini, Dodoma kuna nini, Dar es Salaam kuna nini, Uingereza kuna nini na wapi kuna nini leo yamepitwa na wakati, kwa dakika moja unapata mawasiliano dunia nzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wananchi wamekwishakuelewa kwamba hawataendelea kuchagua viongozi walaghai, viongozi wanaojitembeza kwa misingi ya udini, kwa misingi ya ujinsia, kwa misingi ya umaeneo, kwa misingi ya fedha na misingi yoyote ile wanachojali ni uadilifu na uaminifu wa kiongozi ambaye atakwenda kuwa ni muaminifu na atakayeweza kutimiza haja zao kwa kadri ya mahitaji ya watu wa eneo lile. Kila eneo bado lina matatizo yake, wengine wanahitaji elimu, lazima wamuamini kiongozi huyu anayesema mimi nitaboresha elimu kwa njia gani? Kuna matatizo mengi ambayo wananchi wenyewe wanayapima. Nilipenda niitoe kama rai ili wananchi hao ambao wameanza kujisumbua wafahamu kwamba huo wakati umekwisha na wakati uliopo wananchi ni waelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni masuala yanayotishia amani. Amani yetu ni nzuri na imedumu kwa kipindi kirefu, lakini kwa kipindi hiki tumeona tumekuwa na tatizo kubwa la njaa. Njaa ni vita, njaa ni mapambano ambayo lazima mtu ashinde, kwa sababu bila kushinda njaa maana yake unakaribisha mauti, na baada ya mauti ni kuzikwa kwa hiyo unatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza njaa tunawagusa moja kwa moja wakulima. Sasa mimi napenda kujua kwamba ni kwa kiwango gani sasa ambavyo tunajiandaa kuwa karibu na hawa wakulima. Kitakapofika kipindi cha Bajeti tutapewa taarifa za jinsi fedha tulizozibajeti zilivyotumika kwa kuinua kilimo. Lakini utakuta katika eneo lile tutapewa taarifa ya masuala yanayohusu makongamano, tutapewa taarifa za watu kwenda masomoni, lakini hatutapewa taarifa ni kwa kiwango gani kijiji fulani kilikwenda kupata elimu kuweza kujielimisha namna ya kulima.

Mwenzangu jana hapa aliuliza swali lake, akasema kuhusu mpunga kwa kiwango gani ambacho wananchi wanaelimishwa na kilimo cha mazao ya chakula. Mimi nitapenda kujua ni kwa kiwango gani kijiji changu fulani katika Jimbo langu kimeelimishwa ukulima mzuri wa buni, wameelimishwaje ukulima

mzuri wa migomba? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri katika kipindi hiki, haya makongamano yapungue sana na semina hizi zipungue sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mwananchi wa kawaida ambaye ndiye anayehusika moja kwa moja na kilimo afikiwe yeye mwenyewe na yeye afaidike na masomo yale moja kwa moja na zana sasa ziwepo angalau kuwe na maeneo machache ambayo ni maeneo ya mfano ya kuweza kutusaidia na kuweza kuinua hali hii ili tuweze kubadilika kwa wakati tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kulikuwa na wataalamu wakipita katika vijiji wakiwaelimisha wakulima namna ya kulima, utunzaji wa mazao, uvunaji na utunzaji wa akiba, kwa kipindi hiki sasa wananchi wameachiwa huru, mkulima ana uhuru kuvuna na kuuza popote atakapo.

Sasa ni vyema hii ikaendelea katika wakati tuliokuwa nao, lakini ni lazima mkulima anapoamua kuuza awe tayari ana hakika kwamba anayo akiba yake ya mwaka ule na ikiwezekana awe na akiba anayotegemea kwamba hata baada ya kuwa ameuza anapokwenda katika msimu wa pili bado awe na chakula cha kumtosheleza katika mwaka unaofuata hata katika kusubiri mazao yake yanapokuwa mashambani mwake kabla hajavuna mara ya pili. Hali hii itaweza kutusaidia kuweza kutuondolea hali nzima ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yetu yanaambatana na kujitegemea kwa chakula. Kwa hiyo, ni suala ambalo nimeona nilizungumze ikiwa ni kama changamoto ambayo sisi wote tumeiona na tunakubaliana kwamba njaa ni vita, njaa ni adui na lazima tupambane na njaa ili tuweze kusimamia maendeleo yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naomba nikushukuru tena na niseme ninaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika kwamba Mheshimiwa Rais alipotuhutubia hakutaka kwamba tunaposimama tuwe tunampongeza na kumsifia bali pengine alitegemea yeye kama mtu mmoja licha ya kupata ushauri wa wataalamu wake angeweza kupata mawazo mengine mbadala na mengine kinzani, lakini yenye kuelekeza kujenga hoja ili kuweza kuwa na wingi wa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo nitajaribu kuzungumza hivyo. Labda nikiri kwamba siku moja nilikuja hapa nimevaa suti yangu ya kijani imepauka, sasa akanikumbusha Mheshimiwa Aisha Magina hapa, akaniambia wewe unatuabisha, Mbunge kijana na suti yako hiyo! Kwa kweli sikukasirika na sasa hivi sijaivaa tena. *(Kicheko)*

Lingine alikuwepo Waziri wa Fedha hapa wakati wa Bajeti, mwaka fulani alikuwepo Mheshimiwa Erasto Tumbo, akamwambia wewe unakuja na suti hiyo Waziri wa Fedha huoni hata aibu. Iko kwenye *Hansard* na kwa kweli sijawahi kumuona ameivaa tena, hata jana alikuwa amevaa vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nayasema hayo kwa sababu mtu hata kama si rafiki yako sijui nini, lakini anapokwambia kitu ambacho unaona ni cha msingi inabidi umshukuru badala ya kunung'unika. Sasa kwa mantiki hiyo mimi ninatoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, sijui kama nitalaumiwa kwa yale nitakayoyasema, lakini nadhani nitaongea kwa taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Rais ametueleza katika hotuba yake kwamba anakusudia kuhakikisha kwamba kunakuwa demokrasia, na demokrasia kasema ni kupeleka madaraka kwa wananchi na aka-*quote* Ibara 146 ya kifungu kidogo cha kwanza cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba madhumuni ni kuwapa Serikali za Mitaa na kupeleka madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili ukiliangalia na akaendelea akazitaka Halmashauri za Wilaya na Miji ziweze kuvutia wawekezaji. Sasa katika hili kwa mchango wangu sasa najiuliza kama Halmashauri hizi kweli zimepewa madaraka kwa sababu mimi siyaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa mujibu wa Katiba, Serikali za Mitaa zina madaraka yake, lakini Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Mkuu wa Serikali hii Kuu bado ndiye Waziri wa Serikali za Mitaa. Sasa ile inanishangaza inavyokuwa kwa sababu licha ya kwamba sasa yeye ndiye anayeteua Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata, sasa wananchi umepewa madaraka gani kwenye Serikali yao ya Kijiji ambapo haiwezi kumteua Afisa Mtendaji?

Najua kuna watu wataguna. Huwezi kusema Halmashauri ya Kasulu, Halmashauri ya Karagwe, hazikuvutia wawekezaji wakati hakuna umeme, wakati hakuna barabara, hakuna maji vitu ambavyo wanavipenda wale wawekezaji na hizi Halmashauri haziwezi kuvipata kwa sababu hazina mapato, kwa sababu kodi zote zimekuwa za Serikali Kuu na tumefikia utaratibu ambako Serikali Kuu inataka iwe inaenda inawagawia fedha halafu wao wenyewe wanashangilia.

Sasa *autonomy* na madaraka tuliyowapa, unawapa madaraka wazi bila kuwawezesha. Kwa hiyo, hii ni kasoro ambayo ni lazima Mheshimiwa Rais aione na twambie na kuwalalamikia kwamba hajafanya chochote ni sawa sawa na ng'ombe ana mimba, lakini kile kitoto ndani kinapata maziwa kupitia nadhani kitovu, lakini analalamika kwamba hakili nyasi, sasa kitakula nyasi kikiwa ndani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi Serikali za Mitaa hatuwezi kusema tumewapa madaraka Mheshimiwa Rais ndiye Waziri na nini na licha ya hayo kuna Wakuu wa Mikoa pale. Sasa kama wanagongana huko wanakwenda kwa nani? Kama kuna *conflict* kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu wanakwenda kwa nani? Kwa hiyo, hilo nilitaka niliseme kwamba kitu ambacho katika utaratibu wa kidemokrasia wa nchi yetu lazima tukiangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ya msingi ya ujenzi wa Taifa. Mimi nilipokuwa CCM, imani ya sisi katika CCM ilikuwa kwamba binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja na Watanzania ni wamoja. Lakini sasa hivi CCM ile baada ya mimi kuiacha imebadilika sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza juzi na katika dunia hii ukitaka ukosane na mtu ulizungumze kabila lake ulitukane, utukane dini yake, utukane imani yake au itikadi yake ya chama mtakosana na ndiyo maana kumekuwa na vita.

Urusi sijui wanaeneza Ukomunisti, sijui Marekani wanalinda sijui vitu gani. Ndiyo maana watu wengine wanasema sisi siasa kali. Sasa haya niliyoyasema kwa kujua kwamba tumetoka katika ile misingi tunaanza kuonana hawa wako kwenye Upinzani hawa ovyo na iko kwenye Katiba. Huyu wa chama gani aah hawa hawana point, tena hata mtu mwingine mtu mzima anaona kama nyinyi wendawazimu hivi.

Sasa pale misingi hiyo imekiukwa ya wanadamu wote ni sawa imebaki kwamba msingi ni chama na walioko katika Chama cha Mapinduzi ndio walioumbwa kutawala nchi hii na ndivyo inavyoelezwa huko kote. Sasa kama mnasema Wapinzani nyinyi hawa hawafai hamna kitu, yaani walioko Upinzani hamna kitu ndiyo maana yake. Lakini Chifu Fundikira akirejea kule Mbunge na anaweza kuwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Dr. Lamwai akirejea kule anaweza kuwa Waziri wa Sheria, Mbunge, Rais anamteua. Wako wengine sasa ile dhambi ya mtu kutofaa ni kule kuwa kwenye Upinzani. Hivi huo Upinzani tuliruhusu tunautaka au tunataka mambo ya kitoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani haya tulitaka tuyafikishe. Nchi ni yetu sote tuache kujenga imani ya uchama ambayo itatupeleka kwenda kugombana. Kwa sababu hata wanachama wetu wanachukuliwa unakuta mtu ame-*confuse* mtu *fanatic* mzima eeh eeh. Nini wewe? Chama kiko wapi,.CCM iko wapi. Tuna njaa katika nchi CCM inalala bila kula. CCM haitibiwi hospitalini inaumwa. *CUF* inaumwa, *CUF* haipeleki mtoto shule, ina mtoto. Sasa tuzungumze mambo ya msingi kama Watanzania mtu analeta uchama. Kwa hiyo, nilitaka kuonya juu ya hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametuonya na akasema kutakuwa na walevi. Sasa nilikuwa nasoma biblia wakasema kwa mujibu wa msingi wa biblia kwanza kule Israel ulikuwa mtoto unatahiri ndio unakuwa Mkristo pale. Sasa nikauliza mbona sisi vipi kutahiri ni moja ya masharti, mtu akaniambia hapana sio kutahiri kule bali unatahiri roho yako na kumkubali Yesu Kristo ndiyo unakuwa Mkristo safi. Kumbe ndiyo tafsiri hiyo, akasema ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ameen!

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukija katika hii hoja ya mlevi ni nani na mlevi ni nani. Mheshimiwa Waziri alipokuwa akizungumzia na Mheshimiwa Kwaang'w ameliweka vizuri akasema Rais hakuwa anawasema Vyama vya Upinzani wala nini. Mlevi anaweza kuwa sisi alikuwa anahutubia kama Wabunge kwa ujumla na viongozi wa Serikali. Kwamba katika utawala wa nchi hii tunaweza kulewa madaraka ukiambiwa unavimba kichwa Tunaweza kulewa ukitaka kusifiwa, ukisifiwa bega unalipeleka juu unasahau. Na mambo kadhaa wa kadhaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliendelea kutueleza wengine wanakaa kule nyuma ya viti wengine wanakaa kule mbele. Lakini ina utaratibu wake kwa sababu kuna watu kwenye magari anataka akae mbele mbele. Anakaa mbele dereva anaendesha gari akimshangalia na watoto wa shule anakimbia mpaka mashimo yote hayaoni gari lote analibwaga chini na watu anawaumiza. Lakini lazima tuwe na utaratibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais alipokuwa akizungumzia masuala ya kukubaliana. Alisema katika nchi ya kidemokrasia kwa kweli hatuwezi kukubali watu kutaka kutumia fujo tu kwenda madarakani. Ni kweli kabisa. Wewe unataka kwenda kwa nguvu pale kwa nini. Lakini katika nchi ya kidemokrasia watu huwezi kutaka kung'ang'ania kukaa kwenye madaraka kwa kutumia mabavu. Rais alikumbusha juu ya muafaka na akasema watu kwa kweli watafanya utafiti na pengine wapate *doctorate.* Mimi ningelitaka kufanya katika *political science.* Ningesema muafaka ni nini. Ni makubaliano kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi *(CUF)* kuhusu yaliyotokea Zanzibar. Kuhusu nini? *CUF* walikuwa wanalalamika waliibiwa kura mwaka 1995 na 2000. Halafu ikawaje? Walikuwa hao wanatumia Mkuu wa Wilaya na Polisi wanabeba masanduku. Halafu ikawaje? *CUF* wakakataa matokeo wakawa wanafanya fujo. Halafu ikawaje? Wakaandamana. Hiyo kwenye *hypothesis* yangu. Walipoandamana ikawaje? Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikatuma Polisi watu wakauawa 27. Halafu ikawaje? Jumuiya ya Kimataifa ikasema Tanzania imepoteza sifa ya kuwa na amani. Halafu ikawaje? Viongozi wa *CUF* na CCM wakakaa chini. Halafu ikawaje? Wakakubaliana kwamba iweje? Tuunde Tume Huru. Halafu iweje? Usimamizi uwe wa haki. Halafu iweje? Kura zikipigwa pale hakuna kubeba masanduku. Halafu iweje?*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu iweje? Wakakubaliana Tume ya Uchaguzi kura zikapigwa kwa kweli matokeo yalivyotoka hakuna aliyeibiwa kura hata pale waliposimama CCM peke yao na wale wengine wakapata asilimia 20 na dunia nzima ikajua kwamba sasa mambo yamekwisha wamekubaliana. Fundisho ni nini? Fundisho ni kwamba *peace does not come except by the point of the sword (Makofi )*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi *point of the sword* kwa sababu *I am a fanatic.* Lakini yako mambo mengine alikuwa anasema *Frants Fanon* anasema :*"In order to bring the last to be the first and the first to be the last violence should be used and I do not advocate violence for its own sake otherwise I would have been a homicidal maniac* .Angelikuwa tu anataka kuua watu.

Sasa kama demokrasia hii kule amekubaliana na muafaka. Tume huru wakaweka wajumbe. Huku tukubaliane Tanzania hamna. Sasa mnataka watu waandamane. Tukubaliana kubadilisha Katiba hamna na tunaitana. Nakumbuka hadithi moja mtu mmoja aliwaambiwa watu malaika mkubwa wa Mungu amekuja wafalme na matajiri wote mje kumwona. Akatengeneza kachumba hivi halafu akaweka meza hapo na pazia na sandles hapo yale makubazi halafu akatoka nje akawaambia kila asiyekuwa na dhambi akiingia atamwona yule malaika na kwa kweli wataongea. Sasa wakajipanga wafalme na wenye fedha walipofika wa kwanza akakuta sandles malaika hayupo akaona hapa ana dhambi. Alipotoka nje akawaambia nimemwona tumeongea akaenda nje. Akaja tajiri mwingine akafika pale haoni mtu akaona sandles akatoka

nje akaulizwa umeona nini. Akasema tumeongea vizuri sana yule malaika mtu wa ajabu. Akaenda hataki kusema hakumwona kwa sababu atakuwa na dhambi. Sasa ikaendelea hivyo.

Mheshimiwa Rais amewaita Wenyeviti wa Vyama vya Siasa njooni munishauri, tuzungumze nchi hii. Wamezungumza wanatoka mmoja anatoka anakwenda. Sasa ilipokuja kaitika kubadilisha Katiba wanakaa Chama cha Mapinduzi mlikuwa na *Central Committee* na kadhalika wakasema mgombea binafsi hamna, wakapendekeza hapa halafu wanakuja wanasema haya mabadiliko tutakuwa tunapendekeza sisi CCM ni ya kwetu. Sasa kwa nini unawapuuza hawa Wapinzani hawana mawazo. Wapinzani unatuita halafu unatufanyia mchezo wa namna hiyo. Kwa hiyo tulitaka kupeleka ujumbe huu najua kuna watu watakuwa wanaguna. Kwamba nchi hii ni yetu sote isiwe kila kinachotoka tunataka kupeleka huku. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais aione kwamba kuna watu wa Vyama vya Upinzani kama alivyowaita hapa anavyowaita awaite wazungumze mtu asifanye fujo tuweze kufika mahali tujue tunakwenda. Lakini hii ya kutuhumiana kwamba ninyi dhaifu dhaifu na kudharau ina mambo yake. Ni kwa sababu muda haupo ningeeleza kidogo lakini niache.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuishia hapo ningependa kusema kwamba tunaomba ujumbe huo afikishiwe Mheshimiwa Rais na kwa sababu anakaribia kustaafu ayaone hayo. Lilikuweko moja hili la mambo alikuwa anawatuhumu Marekani wanawapa watu ruzuku sasa wasipowapa watakuwa na njaa kama sisi na sisi hatuwapi tuna njaa. Na Zaire haiwapi ina njaa na *Mozambique* haikuwapa ina njaa, Urusi haikuwapa, ina njaa, Korea Kaskazini haiwapi ina njaa. Sasa mnataka na wao wasiwape mna njaa nyinyi mtawalisha nini mchanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nawashukuruni.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ambayo kwa kweli mimi nasema sio tu kwamba wale wenye macho sasa hivi wataona lakini kwamba watabaki wachache ambao wana macho hawataki kuona na wana masikio hawataki kusikia. Sasa watu wa aina hiyo basi tuwaache kama walivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wenzetu wote ambao wamepata bahati ya kuteuliwa kwenye Bunge letu hili la Jamhuri ya Tanzania ambaye ni Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na wale ambao wanatuwakilisha kwenye Bunge la Afrika na Mheshimiwa Sophia Simba ambaye anatuwakilisha kwenye Bunge la *SADC* wote hao nawapongeza. Lakini na leo nampongeza zaidi Kamishna mpya Mheshimiwa Ngede ambaye ameingia kutokana na Kambi ya Upinzani. Hongera sana kwa kupita kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba nielekeze muda wangu kuchangia kwenye hotuba ya Rais. Moja ambalo ni kubwa na ninawajibika na hasa nikizingatia kwamba kuna kipindi fulani, mahali fulani, wakati fulani Mheshimiwa Rais nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Makundi Maalum alisema tutaangalia na tutaagana vizuri. Sasa leo nimeamini kwamba kweli Mheshimiwa Rais ni mkweli na muwazi kwa kutuongezea ile asilimia 30 ya wawakilishi ya wanawake katika Bunge letu. Namshukuru sana na kwa niaba ya wenzangu nina hakika kwamba wote tutakubaliana kwamba Mheshimiwa Rais hadanganyi amefanya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kupongeza yale yote ambayo yamefanyika kwenye afya, maji, elimu na mengi mengineo. Kwani najua wengi wanaofaidika ni kinamama. Ukiongea habari ya afya najua wengi ambao tunafaidika na zahanati ambazo ziko kila mahali ni wanawake. Ukiongea habari ya maji vijijini wengi tunaofaidika ni wanawake. Ukiongea hata barabara za vijijini wengi tutakaofaidika ni wanawake. Kwa hiyo namshukuru tena kwa kuhakikisha kwamba yale yote ambayo yalikuwa ni mizigo mizito kwa wanawake sasa hivi mzigo ule umepungua kwa kiwango kikubwa. Namshukuru sana kwa hayo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi napenda kuongelea habari ya kuondoa umaskini. Ni muda mwingi na hata Mheshimiwa Rais ametuhakikishia kwamba miundombinu ni nyenzo mojawapo ya kuondoa umaskini. Ndiyo maana barabara zetu, reli zetu, mawasiliano ya simu yote hayo tunayafanyia jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba mawasiliano yanakuwa mazuri na miundombinu ili wenzetu wa nje waweze kuja kuwekeza lakini na sisi wa ndani tuweze kuwekeza na pia kufanya miradi yetu iweze kuwa rahisi na kuweza kujiondoa katika wimbi la umaskini.

Najua kwa Kitanzania nashukuru sana lakini nafikiri nitakuwa sitendi kosa nikiongelea mahali ambapo mimi naishi na si pengine ila Mafia. Tuliongea habari ya Mafia nadhani wengi wetu tutakuwa mashahidi kwamba Mafia tangu iumbwe tangu wananchi wa Mafia wawepo katika ulimwengu huu bado wanalia na kulalamika juu ya ghati. Sasa hivi tuna karne na karne tunaongea neno moja tu ghati. Sasa kwa mimi wa Mafia nikiongea habari ya kusema Miundombinu itanisaidia pamoja na wananchi wenzangu wa Mafia kutuondoa katika umaskini nasema hili sisi bado. Naongea hivyo kwa masikitiko makubwa sana. Nafikiri Mheshimiwa Rais ataliona hili angalau katika miezi 20 iliyobaki ya utawala wake basi tuone kwamba angalau na Mafia inapata ghati. Naomba sana. *(Makofi)*

Tunajua tunaongelea habari ya barabara ya Mwanza mpaka Mtwara. Lakini barabara yetu sisi ya kutoka Mafia kufika Dar es salaam ni kujengewa ghati ili meli ziweze kwenda kwa raha na sisi tuweze kupata maendeleo katika kisiwa chetu cha Mafia. Najua inawezekana kabisa kwamba huko nyuma kulikuwa na sababu ambazo ziliifanya Mafia wasipate ghati kwa haraka. Lakini pia naweza nikajua kwamba inawezekana Serikali kwa wakati huo wa nyuma ilikuwa haina uwezo ya fedha za kutosha kujenga ghati Mafia.

Lakini sasa hivi tukizingatia haswa kwamba suala zima la utalii wa ufukweni na Mafia kama kisiwa chenye fukwe safi ambacho kinaweza kikaleta utajiri wa nchi na mafanikio ya wananchi wa Mafia kwa kuwa na mahoteli mengi ya kitalii kwani wengi baadhi ya watalii wetu wamechoka kuona wanyama pori sasa hivi wanataka kuona wanyama walio baharini. Bahati nzuri Serikali imeshandaa mazingira mazuri katika hili. Tunayo *Marine Park ya kw*anza Tanzania ambayo iko Mafia. Kwa hiyo, nina hakika kuona hili Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mawaziri wenzake wameona kwamba kweli kabisa sasa hivi utalii Mafia lazima utiliwe mkazo. Sasa katika hali ya kukosa ghati sisi kweli haya mambo tutafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema kama ni miundombinu ambayo inaondoa watu katika janga la umaskini na kama kweli watu wa Mafia ni sehemu ya watu wa Tanzania basi namwomba sana Mheshimiwa Rais tena sana kabla hajaondoka katika kiti chake na kabla *Cabinet* iliyo nzuri na maaskari wa miamvuli hawajaondoka kwenye viti vyao washirikiane kwa nia moja. Kwa sababu, sababu tayari ipo na nina hakika uwezo tayari Serikali unao sasa waweke nia ya uhakika ya kutujengea ghati Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ningeliongelea hata kutwa lakini nadhani limeeleweka na nina hakika wote nyinyi mtatuunga mkono katika kutuonea huruma na kutunga mkono kuona kwamba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Mkapa, anatutekelezea hilo moja ambalo ni kero kubwa na wala sio kero dogo la kutupatia ghati watu wa Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ningependa kuongelea suala zima la Uvuvi. Nikirejea pale pale kwamba sisi watu wa visiwani ukiondoa zao la mnazi na mkorosho mazao mengine yote yako baharini. Tunashukuru kwamba tunawahamasisha vijana kujiunga katika vikundi vya ushirika. Tunahamasisha waombe mkopo ili waweze kupata nyenzo za kuvua kwa usahihi. Mradi wa uvuvi sio kama mradi wa Mama Ntilie wala sio kama mradi wa biashara ndogo ndogo. Vijana hao wakijiunga katika vikundi kuweza kutaka kupata mradi wa uvuvi wanahitaji si chini ya shilingi 15 milioni. Hiyo ndiyo katika uchache wake. Kwani leo kuunda kijiboti kidogo kunahitaji karibu mamilioni. Kununua injini ndogo tu ya *horsepower* 15 kunahitaji mamilioni ya shilingi, kununua nyavu na viboya kunahitaji mamilioni. Sasa sisi kama viongozi tunahamasisha. Tunajaribu kuwahamasisha wenzetu wa nje kuja kuwekeza Mafia. Pamoja na hayo tunakwama katika hali hiyo. Miradi yetu sisi si miradi kama ninavyosema ya Mama Ntilie ya Shilingi 20,000 au laki moja au mbili hata milioni moja haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kupitia kwako na Mheshimiwa Rais kuwaelekeza wenzetu wanaotoa mikopo na hasa hii mifuko yetu ambayo inatoa mikopo kwa vijana na wanawake

walione hili ili waongeze kiwango cha mafungu ya mikopo kwa vijana na hasa vijana wa Mafia ambao ukiondoa zao la minazi ambalo miaka mia ukishapanda shughuli imekwisha na mikorosho hali kadhalika bado tuna shamba kubwa ambalo uvunaji wake unahitaji mikopo ya fedha nyingi kidogo. Kwa hiyo naliomba suala hili lifanyiwe kazi ili vijana wetu wa Mafia waweze kujiondoa katika wimbi la umaskini, wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Mafia utawakuta wanavua mwisho wanafunga makumbi, vipande vya makumbi kwenye vipande vya vijinyavu na vijingarawa atavua nini mtu huyu. Anakwenda kukesha baharini anarudi na vidagaa. Kwa hiyo, haya mambo sio ya utani. Wala ndugu zangu nyinyi wa Bara ukiondoa ndugu zangu wa visiwani Zanzibar ambao wao tayari wana kila kitu mjue hali ya wenzenu Mafia kwa kweli ni ya kusikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho najua kengele ya kwanza imelia lakini ndiyo naongelea mawili mazito na kama tunavyojua kila mtu kwanza anafagilia kwake anapoishi. Kiongozi bora kwanza atahakikisha kwake na kuongoza na anapokaa ili pawe katika hali nzuri. Najua ni Mbunge wa Viti Maalum lakini kwa wanawake mengi nimeyaongelea kwamba tunashukuru. Sasa bado nahitaji na Mafia ipige hatua kwa hiyo na mimi nitajisikia raha vijana wangu, ndugu zangu, wenzangu wakiishi katika raha pamoja nikiwemo na mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa narudia kusema nampongeza Mheshimiwa Rais lakini namwomba kabla hajaondoka basi hayo niliyomuomba kwa nia nzuri kabisa na ndugu zangu ambao wananiangalia pale ebu wekeni nia uwezo mnao na sababu tayari mnazo. Sasa wekeni nia ya kutusaidia ndugu zenu wa Mafia ili ile ndege itakaporuka basi turuke pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ambayo imejaa maneno mengi ya Mac Beth ya kila aina ya *literature* inaonekana alikuwa na lengo na lengo hasa kama wengine wanavyosema *may be* kama ni shule, lakini hasa natumaini alikuwa anawaeleza Watanzania wote namna gani wajiweke sawa. Lakini katika mazungumzo yote amezungumzia kitu kimoja akasema wale wanaosema wakamwage damu wapeleke damu yao Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sidhani kama maneno hayo yanasemwa na Upinzani tu. Maneno ya namna hii yanasemwa na Chama cha Mapinduzi tena watu wakubwa. Juzi tu hapa mtu anasema vijana kaeni imara kuwadhibiti Wapinzani, piga baadaye wapelekeni Polisi. Haya yamesemwa na wanaendelea kuyasema. Sisi watu wa Bara tunasema nchi hii ni ya Watanzania wote na lazima Watanzania wote waishi kwa sheria zilizopo na taratibu zilizopo. *Irresponsible Statements* kama hizi za piga halafu peleka Polisi zinatupeleka katika hali ambayo italeta vurugu na Rais natumaini alipokuwa anakemea hili alikuwa anakemea na pia na wale waliopo upande wa pili kwamba wasifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hili linanipa matatizo mengi sana. Tumeshuhudia mara nyingi sana Wapinzani wanasingiziwa kesi za kila aina tangu kwenye ngazi za vijiji wanatengenezewa kesi, wakienda kwenye chaguzi ndogo ndogo ndiko kule wanakopigwa, wanakobezwa. Uvumilivu una kikomo chake. Hata ile hadithi ya Godiath na David ndiyo hiyo hali ambayo iko kati ya Upinzani na wale ambao wanasema wao ni Chama Tawala cha miaka 40 ambacho kwa kusema kweli leo hivi Chama cha Mapinduzi sio mshindani wa *UDP, CUF* wala *TLP*, mshindani wetu kwa sasa ni Polisi, Dola ambayo inabeba Chama cha Mapinduzi ndiyo maana tunapigwa, tunabezwa. Wanaambiwa pigeni pelekeni Polisi. Hii ndiyo hali ambayo inaonyesha kudhoofika kwa Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema uvumilivu una mwisho. Unaambiwa msitari huu unasimama huku unajaribu kujitetea unasingiziwa kesi. Unajaribu kujifanya wewe ni mtaratibu na mpole unafuata sheria unachokozwa kwa hili, hiyo ndiyo iliyomfanya Davi and Godiath na mwishoni naye akaona David naye ajitetee kwa kutupa jiwe kwa kutumia Wasukuma wanasema *Lutagoo* akapiga, hivi akamgonga akadondoka. Mimi naamini katika hali hii kama kweli haiwezi kuwa *arrested* upande wa pili

wa Upinzani kila siku wanachokozwa na vineno na kusingiziwa kesi ya kufanya hivi hatuwezi kufika popote pale.

Juzi tulikuwa kwenye uchaguzi wa kata ya Nkoma. Baada ya kuona kwamba uwezo wa chama cha Mapinduzi ulikuwa haupo wakatumia Polisi. Wakachukua *OCID Bariadi* na askari wawili wakaenda vijijini wakatisha watu wakaenda kumvamia mama mmoja nyumbani kwake Christina Salum akapigwa na Polisi mpaka mimba yake ikatoka.

**WABUNGE FULANI:** *Shame!! !shame!!!*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Na leo ametoka hospitali, amekuwa *discharged* leo. Mimba imetoka tumesema hili tutalichukulia hatua na yule Polisi tunampeleka Mahakamani *as an individual* kwa sababu siamini kama Jeshi la Polisi lilimwagiza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Hii inafanya watu kule chini kwenye *grassroot* kwenye vyama vya siasa waogope kujiunga na Vyama vya Upinzani kwa sababu wanajua kabisa kwamba Chama cha Mapinduzi kwa kusaidiwa na dola watu hawa hawatakuwa na amani Vijijini. Hii inanipa juzi nilikuwa nasoma jedwali moja la kijani linaitwa: "Mkereketwa". Ni *partnership* ya Polisi, Vyombo vya dola na Chama cha Mapinduzi ndiyo chanzo kikubwa cha kudhoofisha Upinzani ambapo Rais anasema tumedhoofika. Anasema: "Najivunia chama changu kwa sababu ya uhusiano mwema uliojengeka kwa miaka 40 kati ya chama changu na vyombo vya dola na Polisi ndiyo maana vinatumika na Usalama wa Taifa *to suppress the opposition in the country. (Makofi)*

Sasa hii tulikuwa nafikiria Mheshimiwa Rais angeona kwamba uwanja wa mapambano kati ya Chama cha Mapinduzi na Vyama vya Siasa hauko *levelled.* Vyombo vya dola kama *Police, Intelligence* na wengine wote wasijihusishe na Vyama vya Siasa. Twende kwenye mapambano, twende kwenye jukwaa pamoja. Uwezo wa kusimama kwenye jukwaa na kulihubiri tunao, uwezo wa kuwa-*convince* wananchi wafuate sera zilizopo tunao. Tulisema nilipokuwa naangalia kile kinachoitwa Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2000 katika eneo la elimu, Chama cha Mapinduzi walisema katika ilani yao waende wakaitafute waisome inasema: "Kila mwananchi atalipia elimu ya mtoto wake". Sisi tulisema kama mkitupa nafasi ya kutawala nchi kila mtoto wa Kitanzania atasoma darasa la kwanza mpaka la saba bure. Sasa juzi wanasema ninyi mna kauli ya kubeza beza, mna tabia ya kunyakua sera za watu *it is in black and white.* Katafuteni sera zenu labda mbadilishe jana. *(Kicheko)*

Tunasema sisi baada ya uchaguzi ulipokwisha tuna jukumu moja tu la kujenga maendeleo ya watu wetu. *Regardless who is in power* tukasema suala la elimu kama tulivyolitetea tutahakikisha kwamba watu wetu wanajenga *Primary Schools,* madarasa na nyumba za walimu kama tulivyokuwa tumepanga. Miaka ya nyuma tulifanya hivyo tulitumia fedha ya Kata kujenga nyumba za walimu na madarasa. Imekuja ile ambayo tulikuwa tunaisema mapema kwamba watoto wetu watasoma darasa la kwanza mpaka darasa la saba na tukabezwa wapuuzi hao watapata wapi fedha.

Sasa fedha imepatikana sisi tunasema fedha mnayo lakini mnaitumia vibaya na iko *reference* hapa. Pelekeni kwa ajili ya elimu hiyo imetusaidia leo Wilaya ya Bariadi ni ya kwanza katika kujenga madarasa na nyumba za walimu nchi nzima. Hii imo hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Julai amesema Wilaya ya kwanza kujenga nyumba na madarasa mengi ni Wilaya ya Bariadi. Iko na imeandikwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu wakati wa hotuba ya Bajeti.

Fedha zilikuwepo sio kwamba hazikuwepo isipokuwa ni matumizi mabaya tu. Matumizi mabaya yako Serikalini hata nashangaa watu juzi au jana sijui kuzungumza nini bila ya kuwa na *proper controls* ya fedha katika matumizi ya Serikali kila siku tutakuja na *Supplementary Budget* hapa. Mmezungumza kasomeni ripoti ya *Auditor General* ambayo imetolewa, *a recent one,* Serikali haiwezi ku-*account* ama fedha zimelipwa bila maelezo zaidi ya 90 bilioni *in form of imprest and advances about 46 billions improperly and un-vouched expenditures* na mengine mengi tu yako mle ndani.

Sasa ninachosema ni kwamba, tukiweza kujizatiti na kuweza kuviweka vitabu vyetu sawa Tanzania tuna uwezo mkubwa wa kuweza kuwasomesha watoto wetu bure *Primary One up to Secondary School. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais hakuzungumzia juu ya rushwa, sijui inampendeza! Lakini naona kwamba, kama unataka uzuie rushwa ni lazima ndani ya nyumba yako kwanza uzuie hiyo rushwa isiwepo. *(Makofi)*

Nimemsikia rafiki yangu Mrema analalamika, anasema Madiwani wake wamenunuliwa, Bariadi wakanunuliwa kwa shilingi milioni tatu. Aah, basi Mwenyezi Mungu awasaidie, lakini ninaamini kati ya wale Madiwani tisa walionunuliwa na kuhamia Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na yule aliyewaongoza, sidhani kama kweli watarudi kuwa Madiwani. *(Makofi)*

Watu wa Bariadi wamekasirishwa na hicho kitendo na mimi narudi kule naenda tena kuhubiri na nitahubiri, nitahubiri mpaka dakika ya mwisho, kati ya wale Madiwani 9 tisa hakuna watakaorudi kama Madiwani. *(Makofi)*

Sasa hiyo ni hali ya rushwa, kama rushwa inatoka ndani ya Chama cha Mapinduzi kwenda kuwahonga watu wa Chama kingine waingie CCM basi tuanze...

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, kifungu gani?

**WAZIRI WA AFYA:** 50(8).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ukisema kuhusu utaratibu unapaswa kusema kifungu.

**WAZIRI WA AFYA:** Nimeshataja.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu cha ngapi?

**WAZIRI WA AFYA:** Nimekwishataja, kifungu cha 50(8).

**NAIBU SPIKA:** Kaa kwanza ili tukisome hicho Kifungu.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu cha 50(8) kinasema hivi: “Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kutumia lugha ya kuudhi, kutumia haki yake ya kusema kwa maudhi, madhumuni ya kutaka kuchelewesha Shughuli za Bunge, kumsingizia Mbunge mwingine yeyote kuwa ana nia mbaya na kumshambulia binafsi isipokuwa kwa kutoa hoja mahsusi inayohusu mwenendo wa Mbunge huyo, kujiingiza katika mambo ya kusema wenzake au kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge.” Hicho ndicho kifungu. Sasa namruhusu Mheshimiwa Waziri ili atoe ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba msemaji athibitishe kama CCM ilihonga hizo Shilingi milioni tatu na alihonga nani. Ni lazima atoe hapa uthibitisho ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, umetakiwa uthibitishe hilo ulilolisema ndani ya Bunge kwamba CCM ilihonga Madiwani shilingi milioni tatu.

**MBUNGE FULANI:** Ni hapo sasa.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu hicho sijataja mtu, nimezungumza mazingira yale ambayo yamejionyesha...

**NAIBU SPIKA:** Samahani, samahani. Wote tumekusikia, umesema CCM ilihonga milioni tatu.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *may I withdraw that* ili niweze kuendelea mbele. Kama unataka uthibitisho nitaeleza jinsi mazingira yale yalivyokuwepo na dalili za rushwa zilizokuwepo, kwa sababu ushahidi unaweza kuwa ni wa mazingira ama wa kidhibiti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa, hebu tujue moja. Una-*withdraw* au bado unasisitiza una ushahidi wa kutoa?

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *I withdraw the statement.*

**NAIBU SPIKA:** Unafuta usemi.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Nafuta ule usemi, lakini naendelea na hotuba yangu. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, yale nimeyasema na kama nilivyokueleza, niliyoyaeleza naweza kuwa nimeyasikia, lakini hali hiyo ipo na inaweza kuendelea. Kuna rushwa nchi hii na hiyo rushwa imeandikwa tena imeandikwa na vyombo vingi, hata vitabu vinazungumza juu ya rushwa. Leo nilikuwa nasoma kwenye magazeti kuwa *traffic* anazungumza juu ya rushwa, lakini Rais hakuzungumza juu ya rushwa na jinsi hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niishie hapo juu ya rushwa, lakini niseme hali halisi ya kisiasa jinsi ilivyo nchini. Ninafikiria kwamba, Mtukufu Rais angeona Upinzani ni kioo chake na kama ni kioo chake kinamwambia kuna hiki, basi achukulie kwamba hiyo ndiyo sura yake, asichukue kiatu akakivunja kioo eti kwa sababu kimemwonyesha hali halisi ilivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijamwita mchangiaji anayefuatia, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah aliomba kutoa hoja yake binafsi jioni hii na Mheshimiwa Waziri anayehusika alikubali na alisema angeijibu. Kwa hiyo, mchangiaji nitakayemwita sasa hivi ndiyo atakuwa wa mwisho halafu tutatoa hoja ya Kuahirisha Bunge na Mheshimiwa Rished Abdalla atapata nafasi.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii niwe mchangiaji wa mwisho katika somo lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuzungumza lolote kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, naomba nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wameitumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliochaguliwa katika Bunge hili kuwa katika Bunge la Afrika. Lakini pia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kutuwakilisha. Ataungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kutuwakilisha katika *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Asha Ngede, ambaye amechaguliwa leo kuwa Kamishna wa Huduma za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijihusishe na Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Niungane na Waheshimiwa wenzangu kumpongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo amekuja kutuhutubia juzi hapa Bungeni. Lakini niseme kwamba, si hotuba hii tu, ni kwa hotuba zake zote ambazo amekuwa akizitoa toka amekuwa madarakani iwe nje ya nchi hii ama ndani ya nchi hii na katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba za Mheshimiwa Rais ni nzuri sana na ni fundisho na zinatuelimisha katika mambo mengi. Ninakumbuka sana mwaka jana Mheshimiwa Rais alialikwa na

Viongozi wa Chama cha Wafanyakazi pale uwanja wa Taifa kwenye Sikukuu ya Wafanyakazi, hapo ninataka kuzungumzia zaidi jinsi gani hizi hotuba zake zilivyo za makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawa Mbunge, nilikuwa ni Kiongozi ngazi ya Taifa katika Chama cha Wafanyakazi. Sasa, tukiwa na suala letu na hasa la kupandisha mishahara Wafanyakazi, tulikuwa na utamaduni wa kumwalika Kiongozi ngazi ya Taifa ambaye ana maamuzi ya mwisho tukitarajia kwamba lile tunalolitaka kwa Wafanyakazi wetu basi litatamkwa siku hiyo ya Wafanyakazi. Sasa, tumekuwa tukifanya hivyo toka Rais amekuwa madarakani na sasa hivi wenzetu Viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wamemwelewa sana Mheshimiwa Rais Benjamin W. Mkapa. Tumejifunza kwamba mwenzetu huyu hakuwa na utamaduni wa kutangaza ama kuwapandisha mishahara Wafanyakazi katika siku ile ya Wafanyakazi, hana utamaduni huo. Ni kwa nini ametumia hilo? Alijua kwamba mambo yote yanapangwa kwenye Bajeti. Kwa hiyo, masuala yake ya kuongeza mishahara Wafanyakazi yeye amekuwa akiyapanga katika kipindi cha Bajeti akijua hayo yatatekelezeka. Kwa hiyo, hilo sisi tumejifunza na Wafanyakazi wamejifunza, tunampongeza sana kwa utamaduni huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipofika mwaka jana katika sherehe hizo za Mei Mosi, Wafanyakazi walikuja kwa nia ya kusema leo baba atatamka nini kuhusu masuala haya, kwa sababu risala ambayo alikuwa amesomewa ilikuwa ni pamoja na kuomba kuongeza mishahara, lakini Mheshimiwa Rais aliweza kuzungumza mengine ambayo yalikuwa yakituhusisha sisi. Moja ya ambalo nililichukua na kitabu hicho kwa kweli ilibidi nikae nacho na huwa ninakisoma mara kwa mara, wakati ule tulikuwa tuko katika suala zima la Ubinafsishaji wa Mashirika haya ya Umma. Kwa hiyo, agenda yake kubwa katika Mkutano ule wa Wafanyakazi yeye alizungumzia suala zima la ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyo na utamaduni wake mzuri, anapenda kutoa mifano mbalimbali akasema kwamba: "Suala la ubinafsishaji ni suala ambalo tulikubaliana sote na tuliulizana na kisha tukatuma wenzetu wataalam kwenda kujifunza sehemu mbalimbali na walipokuja walikuja kutushauri na mimi kama msemaji wa mwisho ilibidi niitangazie nchi hii kwamba tutaingia katika mfumo huo wa Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma." Sasa, inapokuwa tumekwenda tukafikia mahali labda hatukufanya kwa kiwango kile cha kuwaridhisha Wananchi, lawama inakuja kwamba: "Unaona sasa Rais hapa amefanya nini? Shirika amebinafsisha imekuwa hivi na vile." Kitu ambacho Rais alikuwa anasema kwamba tusimwachie mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, alitolea mfano kwamba, kuna bwana mmoja alikuwa anajifunza kuogelea, (hilo kwa kweli nimelikariri sana), akaenda baharini kujifunza kuogelea, kufika kule akazamia kwenye maji akameza maji, akanyanyuka akatoka mara tatu, mwishowe akaokolewa akatolewa nje, akatupiwa michanga kifuani akatapika maji mpaka akatapika damu. Baadaye bwana yule akazungumza kwamba: "Looh, kumbe kujifunza kuogelea ni kazi ngumu namna hii, sitarudi tena kwenye maji mpaka nitakapojua kuogelea."

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema, huyu ni mpumbavu mmoja. Unawezaje kujua kuogelea bila kwenda kuingia kwenye maji na kujifunza kuogelea? Hili lilikuwa linatufundisha nini? Lilikuwa linatufundisha kwamba, tunapopanga masuala yetu tukubaliane kwamba tutafikia mahali yapo ambayo tutafanikisha na yapo ambayo tutashindwa kufanikisha, lakini tuelewe kwamba wote tupo kwenye jahazi moja tunajifunza, hakuna ambaye anafahamu kila kitu kwamba hiki ninapokianzisha kitakwenda vizuri moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni somo zuri sana ambalo ninalikumbuka katika historia toka Mheshimiwa Rais amekuwa kiongozi kwenye madaraka yake na anatufundisha kwamba, tunapofanikisha tupige makofi wote kwa kushangilia kwamba hili tumefanikisha. Lakini pia tunapo-*fail* tusije tukamtupia mzigo kiongozi hasa Rais ama Mawaziri kwamba kwa nini hili hatukufanikisha? Tukubaliane sote kwamba hapa tulijifunza vibaya na hapa tulijifunza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niingie upande wa suala zima la kumpongeza Rais katika kipindi chake. Suala ambalo tutamkumbuka sana Watanzania na tunaendelea kumkumbuka na kumpongeza ni suala zima la *TASAF. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameanzisha kitu kinaitwa *TASAF* na kwa kweli nilishawahi kumpongeza mara nyingi kila ninaposimama kuchangia. *TASAF* imetuondolea umaskini Watanzania na napenda nichukue nafasi hii tena kurudia kumpongeza sana kwa sisi Wananchi wa Wilaya nzima ya Temeke. *TASAF* ilipoanza, Temeke ilipewa kipaumbele kuwa ni ya mfano na kama itafanya vizuri basi *project* hii ingeendelea kwenda katika Wilaya zingine na kwa kweli tulipewa mtihani. Sasa, tulichofanya ni kufanya ushirikishwaji wa pamoja ili tuweze kufanikisha masuala yote haya ya *TASAF* ili na wenzetu waweze kufaidika na mradi huu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wananchi wa Temeke kwa kuwa washindi wa kwanza katika mbio za mwenge. Ni kwa nini tumekuwa washindi wa kwanza kitaifa? Tumekuwa washindi wa kwanza, kwanza kutokana na huu mradi wa *TASAF* kwa kuwa ulikuwa uko kwetu, tumefanya miradi yenye thamani kubwa sana kuliko Wilaya zingine nchi nzima.

Pia, kutokana na mradi huu wa *TASAF* tumeweza kujenga. Tuliwapeleka wale wakimbiza mwenge kwenye shule ambayo tumejenga madarasa 15, huwezi ukaamini. Lakini si hilo tu, kubwa zaidi na ambalo halikuwahi kufanywa na Wilaya zingine tumeweza pia kujenga barabara ya lami yenye urefu wa kilomita nane. Kwa hiyo, haya yote yametokana na mradi huu wa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine na kubwa zaidi, Temeke tulikuwa na matatizo sana ya maji. Tumeweza kuchimba visima na mradi huo walikuwa wakibuni wenyewe Wananchi ili kuweza kuufanikisha. Kwa hiyo, wakagundua tatizo kisha wanazungumza kwamba sisi tunataka tuwekewe maji au sisi tunataka tufanye hivi. Sasa hivi Wananchi wa Temeke wanafaidika na maji. Pia, kuna barabara moja inaitwa barabara ya Mwinyi iko Kata ya Makangarawe na Kata ya Vituka. Hawa wamechimba visima vingi sana na sasa hivi wako kwenye kusambaza maji ili yaweze kutoka pale kilipo kisima na kuwafikia Wananchi kule walikosehemu ile. Lakini mafanikio haya yote yametokana na mradi huu wa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema kwamba, suala ambalo tutaendelea kumkumbuka Mheshimiwa Rais ni huu mradi wa *TASAF* na kwa kweli tumefanya vizuri na ndiyo maana sasa hivi tumeambiwa tutabaki kuwepo katika mradi huo na wenzetu Wilaya zingine watanufaika. Lakini naomba waje waangalie mfano katika Wilaya ya Temeke ili wasije wakakwama baadaye. Pia, tumeweza kujenga zahanati zikiwemo pia na nyumba za Madaktari kupitia mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema suala hili, naomba sasa nizungumzie suala zima la uwanja. Nizungumzie Uwanja wa Kisasa wa Taifa. Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba kabla hajamaliza muda wake na nilikuwa nawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo anasema kwamba: "Itakapofika mwaka kesho mwezi wa 5 uwanja utakuwa tayari." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba, Mheshimiwa Rais anatuongoza vizuri sana, tatizo tulilonalo ni katika utekelezaji wa mambo. Tutafikia mahali tutamwingiza Mheshimiwa Rais wetu katika kuonekana kwamba ni mwongo. Kwa nini tutamfikisha hapo? Ni pale tutakaposhindwa kumsaidia kutekeleza yale yaliyopangwa kwa muda muafaka uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika Bajeti ya mwaka jana imetengwa pesa za kutosha kabisa na tukaambiwa mwezi Novemba mwaka jana uwanja huu ungekuwa umeishaanza kujengwa. Cha kusikitisha mimi ninaishi Temeke, ni hatua chache kutoka nyumbani kwangu kwenda uwanja wa Taifa, uwanja ule umefungwa, wamewekwa Maaskari, hakuna chochote kinachoendelea wala kugongagonga tu mawe hawajaanza, lakini wanamichezo wanapata tabu na kuambiwa kwamba kule ndani uwanja unajengwa. Hakuna chochote kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Kazi niulize kuna nini kinachochelewesha? Nimemwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi ananiambia: "Ooh tunangoja twende Afrika Kusini sijui tukaangalie ..." Ni nini kinachoangaliwa wakati pesa ilishatengwa na muda unapita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana tusije tukamfikisha kiongozi wetu sehemu ambayo yeye hatakiwi kufika pale, tunatakiwa tumzawadie kwa kumsaidia kufanya kazi hizi. Watendaji wake waliopewa dhamana hii ninaomba wasimamie sana suala hili. Nina wasiwasi kama kweli uwanja ule utakuwa tayari kwa muda uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo nimalizie, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba kabla hajamaliza muda wake asilimia 30 ya akina mama watakuwa kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Kwa kweli tunampongeza na Mheshimiwa Mama Halima Kimbau amelizungumza hili. Siku moja ametualika nyumbani kwake, amekwenda kutueleza hili nitalisimamia na kwa kweli amelisimamia na ninampongeza sana.

Sasa, ninaomba nitoe wito kwa wanawake wenzetu waliopo nje ya Bunge hili, wajiandae kuingia katika nafasi mbalimbali zikiwemo nafasi za Udiwani, nafasi za Ubunge na nafasi za kila sehemu, elimu ya kutosha wanayo ili tuweze kufika sehemu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kwamba hotuba za Mheshimiwa Rais ni nzuri na tunahitaji kuzitumia ili ziweze kutuelimisha zaidi. Naunga mkono hoja na nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kama nilivyosema, huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho, sasa namwita Mheshimiwa Waziri atoe Hoja ya Kuahirisha Bunge.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA MUDA WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kanuni ya 21(6), naomba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

## HOJA BINAFSI

## UHARIBIFU WA MAZAO ULIOFANYWA NA WANYAMAPORI KATIKA WILAYA YA PANGANI

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Kanuni ya 21(9) ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa maelezo binafsi kuhusiana na matukio yaliyojitokeza kwenye Jimbo la Pangani ambayo yameleta athari kubwa kwa baadhi ya wakulima wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekumbwa na hali ya hewa ambayo imeathiri shughuli za kilimo na kusababisha njaa katika maeneo mengi ya nchi yetu ikiwemo Wilaya ya Pangani. Vile vile, imesababisha kukauka kwa mabwawa ya maji ambayo yanategemewa na binadamu, mifugo na wanyama wa porini. Kwa kuwa Wilaya ya Pangani imepakana na hifadhi ya wanyamapori inayojulikana kama *Saadani Game Reserve* na Serikali ina mpango wa kuifanya hifadhi hiyo kuwa Hifadhi ya Taifa na kwamba maandalizi ya awali ya kusimamia hifadhi hiyo kupitia Shirika la Taifa *TANAPA* yamekwishaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukame uliojitokeza na kukauka kwa mabwawa ya maji ndani ya hifadhi pamoja na kupungua kwa majani kwa ajili ya malisho kwa wanyama hao, makundi mbalimbali ya tembo yamevuka mipaka ya hifadhi na kuingia katika maeneo ya Vijiji na kufanya uharibifu mkubwa wa mazao ya wakulima katika mashamba yao. Mazao yaliyoharibiwa ni minazi, migomba, mihogo na mengineyo. Takwimu zilizopatikana kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Pangani zinaonyesha kama ifuatavyo: Idadi ya minazi iliyoangushwa na tembo hao ni minazi 8,699. Idadi ya migomba iliyoharibiwa ni 1,053, idadi ya mashamba ya mihogo ni ekari 31/2, idadi ya mikorosho ni 45, idadi ya

miwa ni 255, idadi ya mibaazi 20, michungwa 75 na miembe minane. Wakulima walioathirika ni 197, Vijiji vilivyoathirika ni kama ifuatavyo: Vijiji Vya Mkwaja, Mikocheni, Makorora, Sange, Kipumbwi, Sakura, Stahabu, Mikinguni, Ushongo, Mwera na Kikokwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa maeneo hayo ya Vijiji nilivyovitaja wameathirika vibaya kiuchumi kwani mategemeo yao ya kila siku yanatokana na mazao haya ya nazi kwani ndiyo yanayoendesha familia zao na kupata chakula cha kila siku, kusomesha watoto wao na mahitaji mengine mbalimbali ambayo zinahitaji familia hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matukio hayo imeonyesha wazi kuwa, Idara ya Wanyamapori katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani haina uwezo wa kukabiliana na hali kama hii inapojitokeza na hii ni kutokana na kutokuwa na zana za kutosha kupambana na hali hiyo. Vile vile, hakuna Mabwana Nyama wa kutosha pamoja na silaha na risasi. Vile vile, hakuna usafiri wa kuweza kufuatilia. Wilaya ya Pangani ina Bwana Nyama mmoja tu, bunduki moja ya aina ya *rifle 458* na risasi chache. Bwana Nyama huyu anatembea kwa baiskeli na kwa miguu anapoingia porini, hali ya utendaji kazi inakuwa ngumu sana.

*TANAPA* kwa mujibu wa sheria hawahusiki wakati tembo wanapoingia katika mipaka ambayo siyo yake. Aidha, mtaalam huyo hana mafungu ya kutosha kuweza kusaidia *operation* kama hizo zinapojitokeza mpaka hapo itakapopitishwa kisheria ya kuwa *Saadani National Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yangu kuwa kwa vile tembo hawajui mipaka ya hifadhi na ya Halmashauri ya Vijiji wanayokaa wananchi, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha usalama wa Wananchi na mali zao.

Kwa kuwa Wananchi wa Vijiji nilivyovitaja wameathirika sana kiuchumi hivi sasa kutokana na uharibifu uliofanywa na tembo na kwa kuwa mali zilizokuwa zikitegemewa kuendesha maisha ya familia hizo zimetoweka na kunahitajika siyo chini ya miaka saba ili kupanda mnazi mwingine na kuanza kutoa matunda, wamekuwa katika hali ya umaskini zaidi kuliko hapo awali. Napenda niiombe Serikali ifikirie yafuatayo na ifanye yafuatayo:-

(i) Iwafikirie wakulima wote walioathirika kwa kuvamiwa mashamba yao na tembo walipwe kifuta machozi ili waweze kupata nguvu ya kuanza upya kuendeleza mashamba yao na vile vile wawe na imani na Serikali yao kuwa inawajali. *(Makofi)*

(ii) Iongeze idadi ya Mabwana Nyama pamoja na vifaa vyote vya lazima ili kukabiliana na hali iliyojitekeza. *(Makofi)*

(iii) Itenge fungu maalum la fedha kusaidia *operation* kama hizi. *(Makofi)*

(iv) Iwapatie usafiri wa uhakika Idara ya Wanyamapori Pangani ili kurahisisha shughuli zao na kuweza kuokoa maisha ya Wananchi wetu na mali zao. *(Makofi)*

(v) Shirika la *TANAPA* liongeze juhudi kwa kusaidiana na Idara ya Wanyamapori Wilaya ya Pangani, ili kudhibiti kwa haraka zaidi panapotokea hali kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, minazi ambayo tembo hawa wameharibu ni minazi laki sita kati ya miezi miwili/mitatu ambayo imeshaanza kukosekana katika Wilaya ya Pangani yenye thamani ya Shilingi milioni 30 kwa Wananchi hawa wachache walioharibiwa minazi yao na Halmashauri inakosa wastani wa Shilingi milioni 2 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yangu kuwa Serikali itatoa ushirikiano mkubwa kwa haya niliyoyasema. Naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kama ilivyo kawaida ya hoja hii tutamwita Mheshimiwa Waziri anayehusika, kama ana jibu basi atatoa, kama hana anaweza kuomba muda zaidi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Pangani amewasilisha Hoja binafsi kuhusu Uharibifu wa Mazao ya Wanavijiji katika Vijiji 11 vilivyoko katika Wilaya ya Pangani uliosababishwa na tembo. Vijiji hivyo kama alivyovitaja ni Mkwaja, Mikocheni, Makorora, Sange, Kipumbwi, Sakura, Stahabu, Mikinguni, Ushongo, Mwera na Kikokwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwanza kabisa kupitia Bunge lako Tukufu, kuwapa pole Wananchi wote walioathirika na uharibifu wowote uliotokana na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amebaini kuwa jumla ya minazi 8,699, migomba 1,053, mikorosho 45, michungwa 75 na miembe minane iliangushwa. Aidha, mibaazi 20, mashina 255 ya miwa ililiwa na jumla ya ekari 3.5 za mashamba ya mihogo ziliharibiwa na kusababisha jumla ya wakulima 197 kuathirika vibaya kiuchumi kutokana na uharibifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyobaini, chimbuko la tatizo hili ni hali ya ukame uliosababisha kukauka kwa mabwawa ya maji na upungufu mkubwa wa malisho ya wanyama ndani ya hifadhi ya Saadani. Hali hii imesababisha wanyamapori mbalimbali hususan tembo kuvamia maeneo ya Wanavijiji.

Aidha upungufu wa watumishi, vitendea kazi na Bajeti finyu katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, kumechangia kuongezeka kwa tatizo hili kwa kushindwa kulidhibiti ipasavyo kwa wakati unaotakiwa. Napenda kukubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge, kuwa uharibifu huo umesababishwa hasa na mabadiliko ya hali ya hewa ya ukame ambayo yapo nje ya uwezo wa binadamu pamoja na uwezo mdogo wa kiuchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Aidha ni kweli *TANAPA* hawana jukumu la kupambana na wanyama waharibifu nje ya maeneo ya Hifadhi ya Taifa. Jukumu hilo ni la Halmashauri ya Wilaya husika na pale ipasavyo inasaidiwa na Idara ya Wanyamapori.

Pamoja na hayo sheria ya kuhifadhi wanyamapori namba 12 ya Mwaka 1974 inawatambua askari wa *TANAPA* kama *Authorized Officers* kifungu cha 2 (1) (b). Kutokana na uhusiano mzuri kati ya *TANAPA* na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, uongozi wa *TANAPA* uliopo Saadani na Uongozi wa Wilaya Pangani yaani Kamati walifanya kikao mwezi Desemba mwaka jana kilichozungumzia suala la wanyama waharibifu hususan wanyama tembo. Kufuatia kikao hicho Halmashauri ya Wilaya na *TANAPA* walishirikiana kuendesha doria ya msako wa tembo waharibifu tarehe 27 mpaka 28/12/2003 katika eneo la Mikocheni hadi Mkwaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya wanyamapori dhidi ya wananchi na mali zao yameongezeka miaka ya hivi karibuni. Wilaya ambazo zimeathirika kutokana na tatizo hili ni Singida Vijijini, Ulanga, Kibaha, Ngorongoro, Monduli, Karatu, Moshi Vijijini, Hai, Rombo, Bunda, Tarime, Serengeti, Bariadi, Kahama na Nzega. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na Halmashauri husika kwa kutuma askari wanyamapori kukabiliana na wanyama hao mara tunapopata taarifa za wanyamapori kuingia katika maeneo ya wananchi. Vile vile Wizara inahakikisha upatikanaji wa risasi kwa ajili ya kudhibiti wanyama waharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata maelezo ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Pangani, Wizara yangu imechukua hatua ya haraka kwa kuwatuma Maafisa Wanyamapori wawili yaani Wakurugenzi Wasaidizi, kwa ndege tarehe 14 Februari, 2004 kwenda Wilaya ya Pangani, kuonana na Viongozi wa Wilaya, pamoja na kuona kiwango cha uharibifu ili kuchukua hatua stahili kulingana na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Maafisa wa Wizara yangu kutembelea maeneo husika hasa yaliyodaiwa kuathirika zaidi na pia kuonana na Viongozi wa Wilaya ya Pangani akiwemo Mheshimiwa Dhafa Hatibu Jumbe, Diwani wa Kata ya Mkwaja na Bwana Shehoza Mhina, Afisa Maliasili wa Wilaya, Pangani ilithibitika kwamba uharibifu ulikuwa umefanyika ingawa si kwa kiasi cha kutisha. Takwimu zilizotolewa na Mheshimiwa Diwani, zinaonyesha kiwango cha uharibifu wa miaka mitatu hadi minne iliyopita. Kwa hiyo, takwimu ni za muda mrefu.

Uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, kuhusu ulinzi na usimamizi wa wanyamapori, ikiwa ni pamoja na kudhibiti wanyama waharibifu ni askari watano kwa kweli. Kwa hiyo, takwimu hapa kidogo ni tofauti. Bunduki nane za aina mbalimbali, risasi 165, za aina mbalimbali na pikipiki moja ingawa idara ya Maliasili inazo pikipiki zaidi ya 4. Idara ya Maliasili ilichukua hatua kadhaa za kukabiliana na hali hii ikiwa ni pamoja na kununua risasi 165 za aina mbalimbali, kuua tembo wawili waharibifu na kufanya msako wa tembo waharibifu kwa kushirikiana na *TANAPA.* Minazi mingine ilikuwa kwa kweli imeanguka kutokana na kuwa na mashina hafifu, pia udhibiti mdogo wa moto. Kwa hiyo, ilikuwa imeungua mingine na hivyo kuwa rahisi kuangushwa hata na upepo. Pia minazi yenye hali hiyo ina mazao duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi wangu wamepiga picha na picha ninazo kwa hiyo hata Mheshimiwa Mbunge, akizihitaji ninazo kwenye begi hivi sasa. Kwa hiyo, baadhi ya minazi na mingi pia iko kwenye vichaka na maana hiyo, kwamba palizi haifanyiki ya minazi hiyo. Baadhi ya minazi imeathiriwa na magonjwa kiasi kwamba sehemu ya juu ya minazi hii imekatika na kuacha shina likiwa limesimama. Kwa hiyo, siyo minazi, lakini ni mashina ambayo yaliyosimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuanguka kwa mimea ya mazao kumesababishwa siyo tu na wanyamapori, bali pia na moto usiodhibitiwa ipasavyo ambao kwa kweli hudhoofisha mimea kwa kiasi cha kuweza kuangushwa na upepo mkali na pia maangalizi duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge, ametoa maombi kadhaa ambayo mengi kwa kweli ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya yake, kama vile kuongeza ajira ya kuajiri askari wanyamapori, kutenga mafungu ya fedha kwa ajili ya kukabiliana na wanyama waharibifu na pia ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Wizara yangu inahusika zaidi na usimamizi na uendelezaji wa Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba. Pamoja na hayo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Pangani, kuwa kama inavyofanyika kwa Wilaya nyingine kufuatia taarifa inayoletwa kwa wakati muafaka, Wizara yangu itachukua hatua stahili kulingana na sheria ya kuhifadhi wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 katika kufuatilia na kudhibiti tatizo la wanyama waharibifu Wilaya Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa shughuli zetu kwa leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Kicheko)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 1.05 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 19 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*